Wakati wa Mwisho



Yaliyomo

USHUHUDA WA MITO MIWILI……...4

HAKUNA JAMBO JIPYA CHINI YA JUA……... 8

HISTORIA YA MPITO……...11

WAFALME WA KUSINI NA KASKAZINI……..16

WAKATI WA MWISHO……... 21

NCHI YA UZURI YA KISASA…… 27

Epuko KUU…….…….... 32

EDOMU, MOABU NA AMONI…… 36

KUREJEA KUTOKA KWA WAFU…… 41

HABARI ZA TAABU……...45

HAKUNA WA KUMSAIDIA…… 48

Gazeti la *Wakati wa Mwisho* limesahihishwa na kuhaririwa kwa chapisho la tatu.

Gazeti hili limeandikwa na Jeff Pippenger na kuchapishwa na *Future for America*. *Future for America* hutoa na kupeleka kwa posta jarida la kila mwezi pamoja na kuwasilisha habari za kusikika kwa lugha za Kingereza na Kihispania. Kwa habari zaidi kuhusu somo hili, au kulihusu jarida hilo letu la kila mwezi, waweza kuwasiliana na ndugu wafuatao ambao pia hujumuika katika kazi hii:

Future News
Sanduku la posta 7
Bonnerdale, AR 71933
Simu: 888-278-7744

Meneja wa Usambazaji—Kathy Pippenger
Mhariri & Mnenaji—Jeff Pippenger
JeffPippenger@msn.com

Mhariri wa Makala—Pat Rampy
Patrick.Rampy@juno.com

Mhariri wa Makala —Dean Ferrell
Seventhseal@firstVA.com

Idara ya Uhispania—Al & Lupe Perez
Sanduku la posta 353
Glenwood, AR 71943
Simu: 870-356-7049 aperez77@alltel.net

Future News—Canada
Phyllis Vallieres
RR 3, 2552 Cooper Road
Madoc, Ontario, K0K 2K0, Canada
Simu: 613-473-5332
FAX 613-473-5630 phyllisv@primus.ca

Future for America—Great Britain
Russell & Charmaine Williams
29 Lascelles Close
Leytonstone, London
Simu: 208-279-6903
judicium@aol.com

KAULI YA WITO

Huduma ya *Future for America* ni kuutangaza ujumbe wa onyo la mwisho wa Ufunuo 14 kama ulivyotambuliwa ndani ya unabii wa Biblia na Roho ya Unabii. Utimilifu wa unabii wa Biblia kuhusu nyakati za mwisho sio tena wa siku zijazo – kwani hayo yanatendeka sasa mbele ya macho yetu. Ule ufahamu wa kihistoria na wa kinabii wa Uadventista wa Siku ya Saba sasa umekuwa ni ukweli uliopo. Sisi ndio kizazi cha mwisho. Mkazo wetu juu ya neno la unabii unajumuisha mashauri yote ya Neno la Mungu. Kuyafahamu yaliyo mbele yetu ni bure iwapo hatutaumiliki ule ujuzi wa kusimama hasa nyakati hizi za taadhima. Kupitia utiifu kwa sheria za Mungu, na imani kwa ahadi za Neno la Mungu, tutaupokea ujuzi huo.

Pamoja na ujumbe huo wa kinabii, *Future for America* hutilia mkazo vipengele vyote vya kazi ya umisionari wa kimatibabu. “Kabari ya kupenyeza” – yaani umisionari wa kimatibabu – sharti utekelezwe na wale watakaoikamilisha kazi ya Mungu katika masaa haya ya mwisho.

Katika kipindi hiki, kuishi mashambani huwa muhimu hata zaidi kadri muda unavyozidi kuyoyoma. *Future for America* huushikilia na kuupendekeza ukweli huu wa nyakati za mwisho. Watu wa Mungu sharti wajiandae kwa dhoruba ijayo, nayo matayarisho hayo huujumlisha ujuzi wa kujifunza jinsi ya kuendelea kudumu kwa njia ya kawaida, mbali na vitovu vikuu vya wingi wa watu.

Future for America hunuia kuchapisha na kuyasambaza maandiko yaliyojaa ukweli, huku wakisaidia katika kuanzisha kazi ya uchapishaji wa watu wa kawaida katika baadhi ya sehemu za shamba la Bwana ambamo ndugu waaminifu hawana namna ya kuanzisha kazi ya uchapishaji kwa rasilmali zao wenyewe.

Ushuhuda Wa Mito Miwili

Katika mfululizo wa makala yafuatayo tutajifunza Danieli 11:40-45. Aya hizi sita za kitabu cha Danieli ziliachwa bila kusuluhishwa hadi wakati wetu. Ni kizazi chetu ambacho kina wajibu wa kutambua utimilifu wa aya hizi.

Tutajitahidi kuonyesha kwamba aya hizi zina mlolongo wa matukio ambayo huongoza hadi kufungwa kwa rehema ya wanadamu. Tutaona kwamba Danieli 11, ambayo imepanuliwa katika Ufunuo sura ya 13-18, inaelezea shughuli ambazo Dada White alisema kuwa ni "harakati za mwisho."

Angalau mapendekezo manne yanastahili kutajwa kabla ya kuanzisha fundisho hili:

Kwanza, ushuhuda mkubwa wa unabii kwa ujumla hutuongoza kuamini kuwa sisi ni kizazi cha mwisho cha wana wa Mungu katika ulimwegu huu—kizazi kile ambacho watakatifu na manabii wa kale walitamani kukiona.

Pili, mfululizo wa mwisho wa matukio tayari ushaanza kwa kuanguka kwa Umoja wa Soviet (SOVIET UNION), lakini Uadventista kwa ujumla umelala.

Tatu, Mungu alikusudia aya hizi kuwa kichocheo cha kuleta mwamko wa mwisho kwa watu wa Mungu.

Hatimaye, aya hizi huonyesha mfululizo wa matukio ambayo kwa mara nyingi Dada White anaonya yatakuwa ya kasi mno.

MANDHARI

Tunapoanza fundisho hili hebu tubainishe ikiwa kipindi cha muda kinachohusiana na harakati za mwisho za Danieli 11 kimefika au bado. Wakati ambao tunaishi umewekwa wazi ndani ya Biblia na Roho ya Unabii. Kifungu kimoja kinachoelezea hali ya wakati wetu chapatikana katika juzuu ya tisa ya *Testimonies for the Church*:

> "Tunaishi katika wakati wa mwisho. Ishara za nyakati zinazotimia kwa kasi zinaonyesha kuwa kuja kwa Kristo kumekaribia. Siku ambazo tunaishi ni za makini na muhimu. **Roho wa Mungu anaendelea kuondolewa duniani taratibu.** Mapigo na hukumu tayari yanaanguka juu ya wale wanaodhihaki neema ya Mungu. Maafa ardhini na baharini, hali isiyodhihirika ya jamii, dhalili za vita, ni ya ajabu. Yanatabiri kuwa matukio makubwa zaidi yanakaribia.
>
> "**Mashirika ya uovu yanaunganisha nguvu zao na kuimarishana.** Yanaimarishana kwa mgogoro wa mwisho mkubwa. Mabadiliko makubwa yatafanyika hivi karibuni duniani, na harakati za mwisho zitakuwa za kasi.
>
> "**Hali ya mambo duniani** inaonyesha kwamba nyakati za shida ziko kwetu sasa. Habari za kila siku zimejaa dalili za mgogoro mkali katika siku zijazo hivi karibuni. Uvamizi wa kimabavu ni tukio la kila mara. Migomo ni ya kawaida. Wizi na mauaji yanatendeka kwa mikono ya kila mtu. Watu waliopagawa na mapepo wanachukua maisha ya wanaume, wanawake, na watoto wadogo. Watu wamepumbazwa na ufisadi, **na kila aina ya uovu u**naendelea**…**
>
> "Hakuna wengi, hata miongoni mwa wakufunzi na wasimamizi wa serikali, wanaoelewa chanzo cha hali ya sasa ya jamii. **Wale wanaoshikilia nyadhifa za serikali** hawawezi kutatua tatizo la utomvu wa kimaadili, umasikini, uhasama, na uhalifu unaoongezeka. **Wanajitahidi bila kufaulu kuziweka shughuli za kibiashara kwa misingi salama zaidi.** Ikiwa wanadamu wangeyatilia maanani mafundisho ya Neno la Mungu, wangeweza kupata suluhisho la matatizo yanayowafadhaisha."
>
> "Ulimwengu unakabiliwa na roho ya vita. **Unabii wa sura ya kumi na moja ya Danieli umekaribia utimilifu wake kamili.** Karibuni matukio ya taabu yaliyonenwa kwenye unabii yatatendeka.*"Testimonies, vol. 9, 11-16. (Msisitizo wote umeongezwa kama haikutajwa vinginevyo).*

Je, kifungu hiki kinazungumzia siku zetu? Angalia mandhari ambayo yanayoonyeshwa na Dada White anapotujulisha kwamba " sura ya kumi na moja ya Danieli umekaribia utimilifu wake kamili." Hii inaashiria wakati wetu, kwa hivyo, Danieli 11 itakamilika hivi karibuni.

ROHO KUONDOLEWA

Je, hatuoni Roho wa Mungu akiondolewa duniani kupitia kwa hukumu zinazofuata kuondolewa kwake? Hakika matukio ya Septemba 11, 2001, tetemeko la ardhi, mafuriko, mlipuko wa volkano, vimbunga, vita, mabomu, mauaji, njaa, na magonjwa yote yanathibitisha kuwa ule ushawishi unaozuia wa Roho wa Mungu unaondolewa kutoka kwa wakazi wa sayari hii.

Mashirika ya uovu katika unabii ambayo yanafaa kuungana na kuimarishana yako katika hali tatu. Ni ya kiuchumi (huwezi kuuza wala kununua), kidini (sharti uwe na alama), na kijeshi (tishio la kifo). Tunaona muungano wa ulimwengu wa kidini katika harakati ya ekumeni. Waprotestanti kamwe hawapingi Rumi – wanafuata Rumi. Kiuchumi tunaona biashara ikiungana na kuwa mashirika makubwa, mataifa ya Ulaya yaungana kuuda fedha moja, kutia sahihi mikataba kama GATT na nafta ili kuunda ushirikiano wa kiuchumi kwa minajili ya soko moja la ulimwengu; huku majeshi ya dunia yanaungana chini ya NATO na Umoja wa Kimataifa (UN).

Twayaonna matatizo ya binadamu sasa yamewekwa katika vyombo vya habari vya dunia kama matatizo ya “kimataifa” Huku Umoja wa Kimataifa ukiinuka kama utawala unaofuata kulingana na unabii wa Biblia, ukikusudia kusukumwa juu na utawala wa Marekani.

Hakika uhalifu wa siku zetu unatimiza utabiri wa Dada White, na tamko kwamba viongozi wa taifa hili "wanajitahidi bila kufaulu kuziweka shughuli za kibiashara kwa misingi salama zaidi" inaelezea kwa ufanisi shida ya sasa katika mji mkuu wa taifa letu. Pia hutuonya kwamba kile tunachopaswa kufanya lazima tukifanye kabla ya pesa zetu kukosa manufaa. Ingawa kwa onyo hili, huja faraja kwamba Mungu yuko katika udhibiti. Maelezo yaliyotolewa na Dada White kuhusu shida ya kiuchumi ambayo inakabili viongozi wa taifa hili hayakumpata Mungu kwa mshangao. Pia ni hakika kwamba "roho ya vita" yaweza kuoekana kwa urahisi wakati huu.

Hadithi Iliyo Mara Mbili

Katika mandhari haya Dada White anatuonyesha kwenye kilele cha Danieli kumi na moja, huku akiutambulisha uzoefu wa namna mbili, yaani utamu na uchungu.

“Haiwezekani kutoa maoni yoyote ya uzoefu wa watu wa Mungu ambao watakuwa hai duniani wakati **utukufu wa mbinguni na mateso** ya zamani yatakapojirudua yakiwa yamechanganywa. " ibid.:16.

Vitu viwili halisi viko mbele ya watu wa Mungu--utukufu unaoandama wale ambao huonyesha na kutetea ukweli katika saa hii ya mwisho ya historia ya dunia, na mateso yanayoadimishwa kwa watu wa Mungu na nguvu za uasi ambazo hupinga ukweli katika mwisho wa dunia. Dada White anatambua ujumbe huu wa mara mbili mahali pengine, huku tena akituelekeza kwenye sura ya kumi na moja ya Danieli:

> "Mwanga ambao Danieli alipokea kutoka kwa Mungu ulikuwa hasa wa siku hizi za mwisho... Maono aliyoyaona katika kingo za Ulai na Hiddekeli, ile mito mikuu ya Shinari, sasa yako katika harakati ya kutimizwa, na matukio yote yaliyotabiriwa yatatimia hivi karibuni." *Testimonies to Ministers,* 112-113.

Njozi juu ya kingo za Ulai ni njozi ya Danieli nane, na sehemu pekee ya njozi ya Ulai ambayo ilikuwa haijatimizwa wakati Dada White alisema maneno haya ni Danieli 8:14, ambayo ilianza kukamilika mwaka wa 1844. Hata hivyo, ilikuwa, na bado iko, “katika mchakato wa kutimizwa.” Wakati Ulai unatiririka kuingia ndani ya bahari, unakoma kuwepo. Vivyo hivyo, wakati Kristo atakapomaliza kazi Yake mahali patakatifu mno, ujumbe wa injili ya milele utakuwa umekamilisha kazi yake.

Ile njozi ambayo ilikuwa "sasa katika harakati za kutimia," ambayo alipewa Danieli akiwa Hiddekeli, ni njozi ya aya sita ya mwisho za Danieli kumi na moja-sehemu pekee ya Danieli kumi na moja ambayo bado ilikuwa haijatimizwa wakati Dada White aliandika maneno hayo. Wakati Hiddekeli unatiririka na kuingia ndani ya bahari unakoma kuwepo, hivyo pia wakati “mfalme wa kaskazini” anaufikia “mwisho wake” na "hakuna wa kumsaidia" ujumbe wa Danieli kumi na moja umefikia mwisho wake.

Mito miwili ikitiririka kuingia kwa mikusanyiko miwili ya maji kiishara-Ulai kuelekea bahari ya kioo; Hiddekeli kuelekea ziwa la moto. Njozi mbili zikionyesha hadithi ya waliokombolewa na hadithi ya waliopotea. Mito hii inapotiririka na kuingia baharini, ujumbe wake unauvuka mpaka wa rehema ya wanadamu-milele ukitenganisha wenye haki na waovu.

> “Lo, ni nani atawaelezea maombolezo ambayo yatatokea katika ule mpaka ambao hutenganisha wakati na milele, Hakimu wa haki atainua sauti yake na kutangaza, ‘Mmechelewa sana.’ Kwa muda mrefu malango pana ya mbinguni yamekuwa wazi na wajumbe wa mbinguni wamealika na kusihi ‘Yeyote atakaye, ayatwae maji ya uzima bure.’ Ufunuo 22:17. 'Leo kama utaisikia sauti yake, usifanye moyo wako mgumu. ‘Mwenye kudhulumu, na azidi kudhulumu; Na mwenye haki, azidi kuwa na haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa. Ufunuo 22:11.’ *In Heavenly Places*, 362.

Udhui hili la mara-mbili katika hadithi ya mito hii miwili inaonyeshwa vile vile katika ujumbe wa malaika watatu wa Ufunuo kumi na nne. Sio kwamba ujumbe huu huonyesha mwanadamu injili ya milele kuhusiana na hukumu inayofanyika mahali patakatifu mno tu, bali ujumbe huu pia hutambulisha utawala wa adui ambaye atapinga ujumbe huu wakati wa huu wa hukumu ya mwisho.

Dada White anatujulisha kuwa vitabu vya Danieli na Ufunuo hukamilishana:

> "Katika Ufunuo vitabu vyote vya Biblia hukutana na kufikia hatima. Hapa ndipo nyongeza kwa kitabu cha Danieli. Kimoja ni unabii na kingine ni ufunuo. Kitabu kilichotiwa muhuri sio Ufunuo, lakini sehemu ile ya unabii wa Danieli inayohusiana na siku za mwisho. Malaika aliamuru, 'Lakini wewe, Eh Danieli, yafunge maneno haya, na ukakitie muhuri kitabu, hata wakati wa mwisho.' Danieli 12:4." *Acts of the Apostles,* 585.

Danieli na Ufunuo **huongezeana** katika sehemu nyingi, ikiwa ni pamoja na ujumbe wa mito miwili, ambayo hutumika kutambua ujumbe wa mwisho wa ulio mara-mbili katika kitabu cha Danieli. Mito hii pia hupata mifano yake ya kiaina katika mito miwili ya Ufunuo. Huko tunapata mto wa uhai unaowakilisha ahadi ya uzima kwa wale wanaokubali injili ya milele, wakati pia tunaona Yufrati iliyokauka inayoonyesha kufilisika kwa ibada ya Babeli.

Tunapoyanywa maji ya uzima, yatupasa kuwahimiza wale wanaokunywa maji chafu ya Yufrati watoroke kutoka kwenye chemichemi zilizotoboka za Babeli ambayo imeanguka. Kitabu cha Danieli kinao ujumbe wa mwisho wa onyo katika saa hii ya mwisho ya historia ya dunia. Ujumbe huu wa mwisho unaoashiriwa ndani ya zile njozi ukingoni mwa mito ya

Hiddekeli na Ulai huitambulisha ibada bandia ya "mfalme wa kaskazini" na ibada ya kweli ya yule Mfalme ambaye kwa sasa yuko ndani ya Pahali Patakatifu Mno huko juu.

Uhuisho Mkuu

Njozi zilizopeanwa ukingoni mwa Ulai na Hiddekeli ni sehemu ya hadithi ya Danieli, lakini zina umuhimu gani kwetu sisi leo?

> "Wakati vitabu vya Danieli na Ufunuo vitaeleweka ipasavyo, waumini watakuwa na uzoefu tofauti kabisa wa kidini." *The Faith I Live By*, 345.

Twajua pia ya kuwa hitaji letu kubwa ni uhuisho huu uje kwa watu wa Mungu:

> "Uhuisho wa utaua wa kweli miongoni mwetu ndilo hitaji kuu na la dharura zaidi ya mahitaji mengine yetu yote. Kutafuta jambo hili yafaa kuwa ndiyo kazi yetu ya kwanza." *Selected Messages*, Kitabu 1, 121.

Kuelewa kuwa hitaji letu kuu ni uhuisho halisi, na kuwa uhuisho huu utaambatana na ufahamu wa vitabu vya Danieli na Ufunuo, haitambulishi ile hadithi ya mito ile miwili kama ufunguo kwa uhuisho huu. Inaweza kutambuliwa kirahisi, japo, kwamba njozi ya Ulai, ikizungumzia kazi ya Kristo Mahali Patakatifu Mno, hakika ina uhusiano na uhuisho huu ambao umesubiliwa mno, maana hakuna uhuisho wa kweli utatenganishwa na kazi ya Kristo huko juu.

Wakati watu wa Mugu wataigia katika uzoefu wa mahala Patakatifu mno wataona kuwa uhusiano katika yao na Mungu ni "karibu na umeamliwa" jinsi Kristo alivyoudumisha mshikamano alipokuwa miogoni mwa wanadamu.

> "Jambo moja hakika litaeleweka kutokana na kujifunza Ufunuo – ya kuwa uhusiano kati ya Mungu na watu wake ni wa karibu na ulioamriwa." *The Faith I Live By*, 345.

Ile njozi iliyopeanwa kando ya mto Ulai inao uhusiano na uhuisho wa mwisho, lakini njozi ya Hiddekeli haizungumzii hekalu, bali adui anayeutupa ukweli chini. Je, ujumbe wa mto huu huchangia kwenye uzoefu wetu hata ukaleta uhuisho? Ndio! Kama vile onyo la malaika wa tatu dhidi ya kuipokea chapa ya mnyama ni sehemu ya injili ya milele, vivyo hivyo, ujumbe huo wa Hiddekeli. Ni kwa kuuelewa ujumbe huu watu wa Mungu wataandaliwa kusimama.

"Kitabu kilichotiwa muhuri sio kitabu cha Ufunuo, bali ni ile sehemu ya unabii wa Danieli inayohusiana na siku za mwisho. Maandiko yanasema, 'Lakini wewe, Ee Danieli, yafunge maneno haya, ukakitie muhuri kitabu, hata wakati wa mwisho; wengi watakwenda mbio huko na huko, na maarifa yataongezeka.' Danieli 12:4. Kitabu hicho kilipofunguliwa, tangazo lilifanywa, 'Hapatakuwa na wakati tena.' Soma Ufunuo 10:6. Kitabu cha Danieli sasa kimefunuliwa, nao ufunuo uliotolewa na Kristo kwa Yohana waja kwa wakazi wote wa duniani. **Kupitia kwa ongezeko la maarifa, watu wataandaliwa kusimama siku za mwisho.**" *Selected Messages*, Kitabu 2, 105.

Tambua hapa ya kuwa kutakuwepo na "ongezeko la maarifa," na ni kupitia kwa "ongezeko la maarifa" ndipo "watu wataandaliwa kusimama." Je, "Ongezeko la maarifa" ni nini ambalo litatuandaa kusimama? Katika sehemu hiyo hiyo, aya mbili kwenda chini, twalipata jawabu:

> "Katika ujumbe wa malaika wa kwanza, watu wanahimizwa kumcha Mungu, Muumba wetu, aliyeumba nchi na vyote vilivyomo. Wameiabudu **asasi ya kipapa**, na kuifanya **Sheria ya Yehova isiwe na umuhimu**, lakini litakuwepo **ongezeko la maarifa kuhusu swala hili**." Ibid, uk. 106-107.

Ongezeko la maarifa ambalo litawaandaa watu wa Mungu kusimama ni ufahamu kuhusu Upapa na sabato yake ya bandia. Ufahamu huu unahusiana moja kwa moja na lile onyo la malaika wa tatu katika Ufunuo kumi na nne – na huu ndio ufahamu upatikanao ndani ya ujumbe uliopeanwa kando ya mto Hiddekeli katika Danieli 11:40-45 – kwa kuwa "mfalme wa kaskazini" katika fungu hili ndio Upapa. Twaambiwa:

> "Matukio yale yanayohusiana na utenda kazi wa mtu wa dhambi ndizo ishara za mwisho kufunuliwa wazi katika historia ya dunia hii." Kitabu kile kile, uk. 102.

Danieli 12:1

Twajua kuwa aya sita za mwisho za Danieli kumi na moja zafuturi matukio ya mwisho ya "historia ya dunia hii," kwani katika aya ifuatayo, yaani Danieli 12:1, twapata kufungwa kwa rehema ya wanadamu. "ishara za mwisho" katika "matukio" haya zahusiana na "yule mtu wa dhambi" na jitihada zake za kuuleta ulimwengu mzima chini ya utawala wake kupitia kupitishwa kwa sheria ya Jumapili. Yule "mfalme wa kaskazini" ambaye ndiye mhusika mkuu katika aya sita za mwisho za Danieli kumi na moja, ndiye "mtu wa dhambi."

> "Wakati yule aliye mtakatifu atazidi kutakasika milele, na wakati yeye aliye mchafu atazidi kuwa mchafu milele, wakati Yesu atasimama; wakati kazi yake itakwisha pale Patakatifu Mno, hapatakuwa na mwali mwingine wa nuru kwa ajili ya mwenye dhambi.
>
> "Lakini Shetani amewarai wengine, kupitia watumishi wake wateule, kama alivyomrai Hawa huko Edeni: Hakika hamtakufa, na kuwaambia ya kuwa patakuwepo na kipindi cha kutubu, muda wa neema, ambapo wale wachafu wataweza kusafishwa. Wanaofanya kazi pamoja na Shetani na malaika zake huibeba nuru hadi enzi za usoni, huku wakifundisha kuhusu muda wa toba hata baada ya kurudi kwa Kristo, hivyo kumpotosha mwenye dhambi, na kumwelekeza yule mwenye moyo baridi kwenye usalama bandia. Huwa mzembe na asiyejali, huenda akijikwaa katika muda wa rehema yake. Nuru hufanywa kufika mbele sana, ambamo kuna giza totoro. **Mikaeli anasimama**. Badala ya huruma, mwenye dhambi huyo aliyepotoshwa huihisi gadhabu isiyochanganywa na huruma. Nao huamka wakiwa wamechelewa sana kwa sababu ya udanganyifu huu wa kufisha. Mpango huu aliufanyia utafiti Shetani, nao hutekelezwa na wale wachungaji waugeuzao ukweli wa Mungu kuwa uwongo." *Spiritual Gifts*, juzuu ya 2, 275–276.

Danieli 12:1 ni kufungwa kwa rehema, ambayo hutendeka huku Danieli 11:44–45 ikizidi kutimia. Aya hizi sita za mwisho zauzungumzia utenda-kazi wa yule "mtu wa dhambi", na ndiyo ile njozi kando ya Hiddekeli ambayo "sasa yaendelea kutimia." Njozi hiyo yasimulia matukio ya mwisho yanayomhusisha yule "mtu wa dhambi," ambayo tuaambiwa, "litakuwepo ongezeko la maarifa," ambalo kupitia kwake, "watu wataandaliwa kusimama."

Aya hizo sita za mwisho za Danieli kumi na moja ni mchoro wa maonyesho ya mwisho ya historia ya dunia. Kimsingi, aya hizi zaitenga hadithi ya Upapa, wakati jeraha lake la kufisha limepona, na kukirejelea kiti cha enzi cha ulimwengu, na hatimaye "kuufikia mwisho wake."

YATUPASA KUFAHAMU NINI?

Tumeambiwa kuwa Danieli kumi na moja sasa yaendelea kutimia, na kuwa kupitia vitabu vya Danieli na Ufunuo kitakuja kichocheo cha uhuisho uliosubiriwa kwa muda mrefu. Tumearifiwa ya kuwa kutakuwepo na ongezeko la maarifa kuhusu Upapa, na alama ya mamlaka yake, ambayo yatasaidia kuwaandaa watu wa Mungu kusimama. Pia tumeshauriwa ya kuwa ni sharti tuyafahamu matukio haya:

> "Yale yote ambayo Mungu katika historia ya kinabii aliyataja kutimia hapo kale yalitimia, na yote ambayo bado yanakuja katika mpangilio wake, yatakuwa. Danieli, yule nabii wa Mungu, anasimama pahali pake. Yohana anasimama pahali pake. Katika Ufunuo, Yule Simba wa kabila la Yuda amewafunulia wanafunzi ule unabii wa kitabu cha Danieli, na hivyo ndivyo Danieli asimamavyo pahali pake. Anao ushuhuda wake, yaani yale aliyomfunulia Bwana katika njozi kuhusu **matukio makuu na ya muhimu ambayo sharti tuyajue**, kwani sisi twasimama upeo wa utimilifu wake." *Selected Messages*, kitabu 2, 109."

Amri zote za Mungu ni ahadi, na kwa vile aamuru kuwa "sharti tuyajue" matukio haya, hivyo basi utambuzi na ufahamu wa matukio haya, wameahidiwa wale watakaochunguza:

> "Wakati umewadia wa Danieli kusimama pahala pake. Wakati umefika ile nuru aliyopewa iende ulimwenguni hata zaidi. Iwapo wale ambao Bwana amewatendea mambo mengi watatembea katika nuru, ufahamu wao kuhusu Kristo na **ule nabii unaomhusu utaongezeka zaidi** kadri wanapoukaribia mwisho wa historia ya dunia hii." *The Seventh- day Adventist Bible Commentary, Vol* 4, 1174.

Tunapoendelea na somo hili yatupasa kuikubali kwa dhati amri hiyo ya kuuchunguza unabii huu na kuomba kwa unyenyekevu ile nuru tuliyoahidiwa, ambayo itapatikana kwa wale watakaojitahidi kuwa miongoni mwa wenye hekima.

Kibinafsi, yatupasa tulitambue jukumu letu la kuutangaza ujumbe huo wa onyo unaoashiriwa na mto Hiddekeli, ambao humtambulisha yule mfalme wa kaskazini kama Upapa. Jambo muhimu zaidi, ni sharti tulitambue na kulitimiza jukumu letu la kuwa na uzoefu wa ujumbe unaoashiriwa na mto Ulai, ambao hutuelekeza kwenye ile kazi ya mwisho inayoendelea kwenye hekalu la mbinguni. Iwapo hatutaki kuingia kwenye huo uzoefu unaoashiriwa na mto Ulai, basi ujumbe wa Hiddekeli una manufaa ndogo kwetu. Bila ule uwezo utokanao na ujuzi ambao huingia ndani ya pazia la Pahali Patakatifu Mno, ujumbe wowote wa onyo tutakao utangaza utakuwa na athari ndogo kwa wale watakaousikia, nao hautakuwa na manufaa yoyote kwa wokovu wetu kibinafsi.

Inawezekana kuwa na uzoefu halisi pamoja na Kristo ndani ya Pahali Patakatifu Mno bila ya kuufahamu ule ujumbe wa Danieli 11:40–45. Vilevile yawezekana kuifahamu Danieli 11:40–45 bila ya kuwa na ujuzi pamoja na Kristo. Ile hadithi ya mito miwili ndani ya kitabu cha Danieli yatuita ili tufahamu na kuwa na ujuzi wa yote haya mawili. Jumbe hizi mbili zimetakaswa zifanye kazi maishani mwetu, ili tuweze kuimariza kazi hapa ulimwenguni kwa kuutangaza ujumbe wa onyo la mwisho kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Bila pingamizi – ishara za nyakati zashuhudia ya kuwa Kristo yu tayari kuitamatisha hadithi ya mito hiyo miwili. Je tuko?

> "Kitabu cha Ufunuo, kwa uhusiano na kitabu cha Danieli, hasa chahitaji kuchunguzwa." *Education*, 191.

Hakuna Jambo Jipya Chini ya Jua

Danieli na Ufunuo vinao ujumbe ambao wenye "hekima" **wata**elewa.

"Tunapokaribia mwisho wa historia ya ulimwengu huu, unabii ulionakiriwa na Danieli wahitaji uangalifu wetu maalum, kwa kuwa wahusiana na wakati huu tunaoishi. Pamoja nao wafaa kuunganishwa na mafundisho ya kitabu cha mwisho cha Maandiko ya Agano Jipya. Shetani amewaongoza wengi kuamini kuwa sehemu za unabii wa maandishi ya Danieli na Yohana yule wa ufunuo haziwezi kueleweka. Lakini ahadi i wazi kuwa mibaraka maalum itaandamana na uchunguzi wa nabii hizi. 'Wenye hekima wataelewa' (Danieli 12:10), ni maneno yaliyosemwa kuhusu zile njozi za Danieli ambazo zingefunuliwa siku za mbeleni; na pia kuhusu ule ufunuo ambao Kristo alimpa mtumishi wake Yohana ili kuwaongoza watu wa Mungu kwa karne zote, nayo ahadi ni, 'Heri yule asomaye, na wale wayasikizayo maneno ya unabii huu, na kuyatunza mambo yaliyoandikwa humo ndani.' Ufunuo 1:3." *Prophets and Kings*, 547–548.

Pengine mwelekeo ulio muhimu sana ambao twafaa kuutambua, huku tukijaribu kuuelewa unabii huu, ni ushauri ule tuliopewa kuwa tuifahamu historia takatifu.

Matukio Makuu Na Ya Dhati

"Yale yote ambayo Mungu katika historia ya kinabii aliyataja kutimia hapo kale yalitimia, na yote ambayo bado yanakuja katika mpangilio wake, yatakuwa. Danieli, yule nabii wa Mungu, anasimama pahali pake. Yohana anasimama pahali pake. Katika Ufunuo, Yule Simba wa kabila la Yuda amewafunulia wanafunzi ule unabii wa kitabu cha Danieli, na hivyo ndivyo Danieli asimamavyo pahali pake. Anao ushuhuda wake, yaani yale aliyomfunulia Bwana katika njozi kuhusu **matukio makuu na ya muhimu ambayo sharti tuyajue, kwani sisi twasimama upeo wa utimilifu wake."** *Selected Messages*, kitabu 2, 109."

"Twasimama **upeoni mwa matukio makuu na ya dhati.** Unabii mwingi waelekea kutimia katika mfululizo kwa kasi. Kila kiungo cha nguvu ki karibu kuanza kazi. **Historia ya kale itarudiwa,** mabishano ya jadi yatafufuka upya, nao watu wa Mungu watapatwa na hatari katika kila upande. Ukuu unaishika jamii ya wanadamu. Unapenya ndani ya kila kitu duniani…

"Chunguza Ufunuo kuhusiana na Danieli, **kwani historia itajirudia …**

"Tunapoukaribia mwisho wa historia ya ulimwengu huu, unabii unaohusiana na siku za mwisho hasa wahitaji uchunguzi wetu. Kitabu cha mwisho cha Maandiko ya Agano Jipya kimejaa ukweli ambao twahitaji kuuelewa. Shetani ameyapofusha mawazo ya wengi kiasi kwamba wao hufurahia kijisababu chochote cha kuwawezesha kutofanya Ufunuo somo lao." *Testimonies to Ministers*, 116–117.

Kusimama kwenye "upeo" wa matukio makuu na ya dhati inamaanisha kuwa yangali bado mbele yetu. Tumeamriwa kuyajua matukio haya. Ili tuyatambue, twaelekezwa kwenye historia ya watu wa Mungu kama marejeleo:

"Biblia imerundika na kufunganisha pamoja hazina zake kwa ajili ya kizazi hiki cha mwisho. **Matukio yote makuu na shughuli muhimu za historia ya Agano la Kale zimekuwa, na zaendelea, kujirudia kanisani katika siku hizi za mwisho…** Hapo rundikizo lote la ukweli latolewa kwetu kwa nguvu ili tufaidike kwa mafundisho yake." *Selected Messages*, kitabu cha 3, 339.

Ni kwa kuchunguza historia ya kanisa ambapo Roho Mtakatifu hupeana maarifa na utambuzi unaohitajika kuyatambua matukio hayo muhimu yaliyo mbele yetu. Ni kwa kuifahamu historia ya uhusiano wa Mungu na watu wake ambapo twalipata hakikisho letu:

"Kwa kuitafakari historia yetu ya awali, tukiwa tumesafiri kila hatua ya mwendo hadi pale ambapo tumesimama, ninaweza kusema, Mungu Asifiwe! Niyaonapo yale Mungu ameyatenda, najawa na mshangao, na ujasiri kwa Kristo kama kiongozi. **Hatuna jambo la kuhofia kuhusu yajayo isipokuwa kama tutasahau jinsi ambavyo Bwana ametuongoza."** *Testimonies to Ministers*, 31.

Uamsho Wa Zamani

Tukitambua kuwa hitaji letu kuu ni la uamsho, na ya kuwa uamsho utakuja kutokana na ufahamu wa vitabu vya Danieli na Ufunuo, sio vigumu kutazama nyuma katika historia ya kanisa letu na kugundua wakati ambapo ufahamu wa vitabu hivi ulileta uamsho. Tukio kama hili lilishuhudiwa mwanzoni mwa harakati ya Wanamiller.

Harakati hiyo ilianza na ongezeko la ufahamu wa kitabu cha Danieli, hasa kuhusu njozi ya ukingoni mwa mto Ulai, kama ilivyonakiliwa kwenye sura ya nane ya Danieli. Ijapo msingi wa harakati ya Wanamiller ulikuwa ni ufahamu wa zile siku 2300 za Danieli 8:14, haukuwa hadi ndani ya harakati, kufuatia "ongezeko la maarifa" juu ya swala lilo la siku 2300, kwamba kukatendeka na uamsho wenye uwezo mkuu.

"'Wakati bwana arusi alipokawia, wote walisinzia na kulala usingizi. Lakini usiku wa manane, kelele ilipigwa, Tazama, bwana arusi anakuja; tokeni nje mkamlaki. Ndipo wale wanawali wote wakainuka, wakazitengeneza taa zao.' Mathayo 25:5-7. Katika majira ya kiangazi ya mwaka wa 1844, nusu ya katikati ya muda ambao mwanzoni ulidhaniwa siku 2300 zingefikia mwisho, na majira ya kupukutisha mwaka uo huo, ambazo baadaye zilionekana kwamba zimetima, ujumbe ulitangazwa kwa maneno yaleyale kabisa ya Maandiko:' tazama Bwana arusi anakuja!"

"Kile kilichofanya badiliko hili kulikuwa ni kugundua amri ya Artashasta kwa ajili ya kujenga upya Yerusalemu, ambayo iliweka Mwanzo wa mahali pa kuanzia kwa kipindi cha siku 2300, ilitekelezwa katika majira ya kipupwe ya mwaka wa 457 B.C; na siyo mwanzoni mwa mwaka, kama ilivyokuwaimeaminiwa hapo awali. Ukihesabu kuanzia majira ya kipupwe ya mwaka 457, miaka 2300 hukomea katika majira ya kupukutisha ya mwaka 1844." *The Great Controversy*, 398-390.

Je, ujuzi huu wa nuru iliyoongezeka waweza kuwa ni historia itakayojirudia katika wakati wa mwisho? Je, kunayo nuru zaidi itakayofunuliwa kuhusu nabii zizi hizi ambazo tumezitangaza kuwa zilifunuliwa mnamo 1844? Jambo kama hili laweza kutarajiwa, kwani, kama tulivyotaja katika sura ya kwanza, itakuwa ni kupitia kwa "ongezeko la maarifa" yapatikanayo ndani ya unabii wa Danieli na Ufunuo ambapo watu wataandaliwa kusimama.

"Kitabu cha Danieli sasa kimefunuliwa, na ufunuo ule ambao Kristo alimwonyesha Yohana utawafikia wakazi wote wa dunia. Kwa ongezeko hilo la maarifa, watu wataandaliwa kusimama **mnamo siku za usoni…**

"Katika ujumbe wa malaika wa kwanza, watu wanahimizwa kumcha Mungu, Muumba wetu, aliyeumba nchi na vyote vilivyomo. Wameiabudu asasi ya kipapa, na kuifanya Sheria ya Yehova isiwe na umuhimu, **lakini litakuwepo ongezeko la maarifa kuhusu swala hili**." *Selected Messages*, kitabu 2, 105–106.

Wanawali Wa Kwanza Kumi

Wakati nuru mpya iliwajia wafuasi wa Miller ikitambulisha Mwanzo ufaao wa zile siku 2300, watu walianza kuutangaza ujumbe, "Haya, Bwana arusi yuaja!" Huu ulikuwa ndio mwanzo wa mwamko mkuu wa enzi zao, na ulikuwa ni utimilifu wa fumbo lile la wanawali kumi. Uliuongeza msukumo ujumbe wa pili, uliowaita watu watoke Babeli.

Kulingana na tamaduni za Mashariki, bwanaharusi huja mwanzoni na pia mwishoni mwa mfuatano wa harusi. Kwanza, huja nyumbani kwa biharusi, kisha huja nyumbani wake mwenyewe. Bwanaharusi huja mara mbili. Je, hii yaweza kuwa sehemu ya fumbo lile, sehemu ya historia ambayo itajirudia?

Ujuzi Wa Watangulizi Kurudiwa

"Mara kwa mara mimi huelekezwa kwenye lile fumbo la wanawali kumi, watano ambao walikuwa werevu, na watano wajinga. **Fumbo hili limekwisha timia na litatimia kikamilifu,** kwani linalo matumizi maalum wakati huu, na pia, sawa na ule ujumbe wa malaika wa tatu, umewahi kutimia na utazidi kuwa ukweli wa leo hadi mwisho wa wakati." *Review and Herald*, August 19, 1890.

Dada White anena wazi kuwa kutakuwa na kujirudia kwa fumbo lile la wanawali kumi, ambalo, lilipotimika mara ya kwanza mnamo majira ya kiangazi ya 1844, kilikuwa ni kichocheo cha ujuzi wa mvua ya awali wakati wa harakati ya watangulizi. Yeye pia huzungumzia usawia uliopo kati ya ujumbe wa malaika wa pili na wa nne:

"Niliona malaika wakiharakisha hadi na kutoka mbinguni, wakishuka duniani na kurudi mbinguni, wakijiandaa kwa utimilifu wa tukio la muhimu. Kisha nikaona malaika mwingine ameamriwa kushuka duniani, kuunganisha sauti yake pamoja na malaika wa tatu, na kuupa nguvu ujumbe wake. Nguvu na utukufu mkubwa ulipewa kwa malaika huyo, na aliposhuka, dunia ilikuwa iling'ara kwa utukufu wake. Mwanga uliohudhuria malaika huyu ulipenyeza kila mahali, alipolia kwa nguvu, na sauti yenye kuu, 'Babeli mkuu umeanguka, umeanguka, na kuwa makao ya pepo, na umiliki wa kila roho mchafu, na ngome ya kila ndege mchafu na mwenye chuki. Ufunuo 18:2. Ujumbe wa kuanguka kwa Babeli, kama ulivyonenwa na malaika wa pili, unarudiwa, na kutajwa zaidi kwa uasi ambao umeingia makanisa tangu 1844. Kazi ya malaika huyu inakuja kwa wakati mwema wa kujiunga na kazi kubwa ya mwisho ya ujumbe wa malaika wa tatu unapoendelea na kuwa kilio kikuu. Na watu wa Mungu wamejiandaa kusimama katika saa ya majaribio, ambayo wataikutana karibuni. Niliona mwanga mkubwa juu yao, nao wakaungana na kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu bila hofu.

"Malaika wengine walitumwa kumsaidia malaika yule mwenye mamlaka kuu, aliyetoka mbinguni tena nilisikia sauti iliyokuwa ikienea pote ikisema hivi; "Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake. Kwa maana dhambi zake zimefika mbinguni, na Mungu amekumbuka maovu yake." (ufunuo 18:4-5). **Ujumbe huu ulionekana kuwa ni nyongeza katika ujumbe ule wa malaika yule wa tatu. Ukiungana nao kama vile kilio cha usiku wa manane kilivyoungana na ujumbe wa malaika wa pili mwaka 1844.** Utukufu wa Mungu uliwakalia watakatifu waliovumilia wakingoja, nao wakalitoa onyo la mwisho kwa ushujaa, wakilitangaza anguko la Babeli, na kuwaita watu wa Mungu watoke kwake, kusudi waweze kutoroka maangamizo yake ya kutisha.
Early Writings, 277–278.

Ushauri kwetu tujiandae kwa ajili ya siku zijazo kupitia ufahamu wa historia ya zamani inayohusu utimilifu wa kihistoria wa lile "fumbo la wanawali kumi" miaka ya 1840, hutambulisha kuwa uamsho unaotarajiwa na kanisa utakuwa sawia na yale mabadiliko ya watangulizi. Twafaa kutarajia ongezeko la nuru kuhusu ujumbe uo ambao tumekuwa tukiutangaza kwa zaidi ya miaka 150. Ujumbe huo ndio ujumbe wa malaika wa tatu unaoleta onyo kuhusu ile Sheria ya Jumapili. Danieli 11:40-45 yalitambulisha tukio linalofuata katika unabii kama sheria ya Jumapili kule Marekani!

Kwa wale watangulizi, habari mpya ilikuwani ule Mwanzo wa siku zile 2300 za Danieli 8:14. Nuru mpya kuhusu ujumbe waliokuwa wakiutangaza hapo awali. Kabla ya ile nuru mpya iliyousababisha ule uamsho wa "kilio cha usiku wa manane" kulikuwa na tukio la kihistoria lililokuwa limetambulika na kutangazwa, ambalo lilikuwa limeongeza msukumo kwa harakati ya Wanamiller.

Kichocheo Cha Unabii

> "Katika mwaka wa 1840 utimilifu mwingine uliowazi uliamsha shauku kuu iliyoenea kila mahali. Miaka miwili kabla, Josiah Litch, mmoja wa wachungaji viongozi waliohubiri marejeo, alichapisha tafsiri ya Ufunuo 9, ikitabiri kuanguka kwa ufalme wa Ottoman. Kulingana na kukokotoa kwake, utawala huu ulikuwa upinduliwe, katika mwaka wa 1840 BK; wakati Fulani katika mwezi wa Agosti, na siku chache kabla ya kutimia kwake aliandika: "Akitambua kipindi cha kwanza cha miaka 150, kuwa kimetimia kikamilifu kabla ya Deacozes kupanda kwenye ufalme wa idhini ya uturuki, na kwamba miaka 391, ssiku kumi na tano, ilianza mwishoni mwa kipindi cha kwanza kitaishia tarehe 11 Agosti, 1840, wakati utawala wa Ottoman katika Constantinople unapotarajiwa kuvunjwa. Na ninaamini hili litakuwa kweli".
>
> "Katika muda ule ule uliotajwa uturuki, kupitia mabalozi wake, ilikubali ulinzi wa falme za muungano za Ulaya, na hivyo kujiweka yenyewe chini ya utawala wa taifa la Kikristo. Tukio hilo lilikamilisha utabiri kwa uhakika. Wakati ilipojulikana, watu wenngi waliaminishwa na usahihi wa kanuni za kutasfsiri unabii zilizotumiwa na Miller na wenzake, na msukumo mkubwa ulitolewa kwenye harakati za marejeo. Wasomi na watu wenye vyeo walijiunga na Miller, kwa njia zote kwa kuuhubiri na kuchapisha mtazamo wake, na kutoka mwaka 1840 hadi 1844 kazi ilikuwa imeenea sana." *The Great Controversy,* 334–335.

Mambo mawili yanatambuliwa kuambatana na utimilifu wa utabiri wa Litch. Sio kwamba harakati hiyo ilipata msukumo wa ajabu pekee, lakini pia kanuni za utafsiri wa kinabii alizozitumia Miller pia zilithibitishwa kuwa ni kanuni halisi katika mafunzo.

Wakati sisi, kama wale watangulizi, tunapozifuata tafsiri za kinabii ambazo zakubaliana na zile kanuni alizozitumia Miller na washiriki wake, hapo tutakuwa na vifaa vya kuaminika kutuwezesha kuuelewa unabii. Iwapo Waadventista leo wangezishikilia kanuni hizo kikamilifu, wala sio zingine, yawezekana kuwa nusu ya yale mafundisho ya uongo yanayolikabili kanisa letu leo yangetoweka kama vile ukungu wakati ya kiangazi.

Lakini la taadhima ni swali hili la jadi – Je ingekuwaje? Je, ingekuwaje kama tungetambua na kutangaza – **kabla ya 1989** – ya kuwa ungekuwepo muungano wa siri kati ya Vatican na Marekani ambao ungepelekea kuanguka kwa Muungano wa Sovieti? Je, tungedhihakiwa, kama walivyotendewa wale walioutangaza utabiri wa Litch? Ni nini kingetokea wakati hatimaye yalipotimia? Utabiri wa Litch kuhusu kuanguka kwa Milki ya Uturuki ulileta uwezo mkuu kwenye ile harakati ya awali ya Uadventista.

Mungu alikusudia unabii wa Danieli 11:40 kazi maalum ya "msukumo wa ajabu" sawia ulivyoletwa na utabiri wa Litch. Mungu angeweza kuwa na watu wake kuutambua na kuutangaza ujumbe huo kabla ya kuwa historia ya kale.

> "Wale wanaojitia chini ya utawala wa Mungu, kuongozwa na kuelekezwa naye, **watauelewa msululu wa matukio yaliyoamriwa Naye kutendeka.**" *Testimonies*, volume 7, 14.

Mabadiliko ya mwisho sasa yaendelea. Ingawa, kinyume na kile kichocheo uliopewa ujumbe huo na utabiri wa Litch kabla ya kuanguka kwa Milki ya Uturuki, kuanguka kwa Muungano wa Sovieti siku zetu kulitoa tanafusi kidogo tu kwa watu wa Mungu. Ujuzi wa harakati ya wale waanzilishi ulikusudiwa kurudiwa siku zetu, lakini sisi katika Laodekia tumezidi kulala. Hakika wakati umewadia wetu sisi kuamka!

> "Siku ambazo tunaishi zina matukio mengi na pia zimejaa hatari. Ishara za kuja kwa siku za mwisho zazidi kuwa nzito pande zote, nayo matukio yatatendeka ambayo yatakuwa na sura ya kutisha kuliko yote yaliyowahi kushuhudiwa na ulimwengu. 'Kwa kuwa watakaposema, Amani na salama, ndipo uharibifu utawajia kwa ghafla.' Lakini wale walio na nuru, imeandikwa, 'Bali ninyi, ndugu, hammo gizani, hata siku ile iwapate kama mwivi. Kwa kuwa ninyi nyote ni wana wa nuru, na wana wa mchana; sisi si wa usiku, wala wa giza. Basi tusilale usingizi kama wengine, bali tukeshe, na kuwa na kiasi.' 1 Wathesaloniki 5:3-6, 'Naam, tukiujua wakati, kwamba saa ya kuamka katika usingizi imekwisha kuwadia; kwa maana sasa wokovu wetu u karibu nasi kuliko tulipoanza kuamini. Usiku umeendelea sana, mchana umekaribia, basi na tuyavue matendo ya giza, na kuzivaa silaha za nuru.' Warumi 13:11-12. 'Kesheni basi, kwa maana hamjui ajapo bwana wa nyumba, kwamba ni jioni, au kwamba ni usiku wa manane, au awikapo jimbi, au asubuhi; asije akawasili ghafula akawakuta mmelala.' Marko 13:35-36." *Review and Herald,* November 22, 1892.

Historia ya Mpito

Katika sura mbili za kwanza za mfululizo huu, tulitoa ushahidi uliodhihirisha kwamba Mungu ametushauri tuifahamu historia. Katika enzi zilizopita, watu wa Mungu wameangamizwa kwa kukosa maarifa.

> Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa: kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa, mimi nami nitakukataa wewe usiwe kuhani kwangu mimi, kwa kuwa umeacha kuijali sheria ya Mungu wako mimi name sitawajali watoto wako. Hosea 4:6.

Angalau sehemu ya maarifa yatakayotukinga tunapozikaribia saa hizi za mwisho wa historia ya dunia, ni ufahamu wa yale yaliyopita. Katika sura ya pili, tuliiangazia historia iliyojiri wakati wa ujumbe wa malaika wa pili na wa tatu mnamo 1843-44. Tuliutambulisha ujuzi huu kuwa ni mfano wa ule uamsho wa mwisho wakati wa mvua ya masika.

Sasa tutautazama wakati fulani katika historia ambao pia umetambulishwa kuwa ni muhimu kwetu sisi kuufahamu. Historia hii yahusishwa moja kwa moja na kiini msingi cha somo letu – yaani aya sita za mwisho za Danieli 11.

> "Hatuna muda wa kupoteza. Nyakati za dhiki ziko mbele yetu. Ulimwengu unakabiliwa na roho ya vita. Karibuni matukio ya ajabu yaliyonenwa katika unabii yatatimia. **Unabii katika sura ya kumi na moja ya Danieli** umekaribia utimilifu wake kamili. **Mengi ya historia hii ambayo yametendeka kwa utimilifu wa unabii huu yatajirudia.** Katika sura ya thelathini mamlaka yameongelewa ambayo 'yatavunjika moyo'
>
> 'Kwa maana merikebu za Kitimu zitakuja kinyume naye, naye atavunjika moyo, na atarejea, na kutoa wazi hasira yake dhidi ya agano takatifu, ndivyo atakavyofanya; Atarudi na kuonyesha fadhili kwa wale waliachao agano takatifu. Majeshi yatasimama upande wake, na kuinajisi ngome ya hekalu na kuondolea mbali sadaka ya kuteketezwa ya kila siku, na ndipo watakapolisimamisha chukizo la yharibifu lifanyalo ukiwa. Na wale wanaofanya uovu dhidi ya hekalu takatifu atawanajisi kwa udangayifu wake, lakini watu wanaomjua Mungu wao watasimama imara, na kutenda makuu. Wale wenye hekima watawaagiza wengi, ingawa kwa kitambo watauawa kwa upanga au kuchomwa moto, au kukamatwa na kufanywa mateka. Watakapoanguka, watapokea msaada kidogo, nao wengi ambao si waaminifu wataungana nao kw udanganyifu. Baadhi ya wenye hekima watajikwaa, ili kwamba waweze kujaribiwa, kusafishwa, kutakaswa na kufanywa wasio na waa mpaka wakati wa mwisho, kwa maana bado ni hadi wakati ulioamriwa. Mfalme atafanya apendavyo. Atajikweza na kujitukuza mwenyewe kujihesabu mwenye nguvu zaidi juu ya kila mungu naye atasema vitu ambavyo havijasikiwa dhidi ya Mungu wa miungu. Atafanikiwa hadi wakati wa ghadhabu utimie…'
>
> **"Matukio sawa na yale yaliyoelezewa ndani ya maneno haya yatatendeka**. Twauona ushahidi kwamba Shetani anazidi kuyadhibiti mawazo ya wanadamu kwa kasi, yaani wale wasiomcha Mungu. **Hebu wote wasome na kuuelewa unabii wa kitabu hiki,** kwa kuwa tunaingia sasa katika wakati wa taabu ulionenwa; 'Wakati huo Mikaeli atasimama, jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako; na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo; na wakati huo watu wako wataokolewa; kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile. Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele. Na walio na hekima watang'aa kama mwangaza wa anga; na hao waongozao wengi kutenda haki watang'aa kama nyota milele na milele. Lakini wewe, Ee Danieli, yafunge maneno haya, ukakitie muhuri kitabu, hata wakati wa mwisho; wengi wataenda mbio huko na huko, na maarifa yataongezeka.' Daniel 12:1–4." *Manuscript Releases*, volume 13, 394.

Dada White anatambulisha utimilifu wa kihistoria wa Danieli kumi na moja kama jambo ambalo tunapaswa kulitarajia kuliona likijirudia wakati "utimilifu kamili" wa Danieli kumi na moja ukijifunuwa. Yeye hasa huiangazia Danieli 11:30-36.

Wale waanzilishi pamoja na Dada White walielewa kuwa Danieli kumi na moja ilitimia kuanzia aya ya kwanza hadi kirai cha kwanza cha aya ya arobaini, inayotufikisha 1798 – "wakati wa mwisho." Kwa hivyo, Dada White anapouzungumzia utimilifu kamili wa Danieli kumi na moja, anazungumza kuhusu aya ya 40-45. Huku akituelekeza kwenye "matukio" na "historia" itakayojirudia, yeye huitenga historia ya aya hizi hata zaidi kwa kudondoa Danieli 12:1-4. Dada White kwa wazi alitambua kusimama kwa Mikaeli katika Danieli 12:1, kuwa ni kufungwa kwa rehema. Utimilifu kamili wa aya za 40-45 watupeleka kutoka 1798 hadi kwenye vita vya Harmagedoni. Wakati wa matukio yaliyoelezewa katika aya za 40-45, Mikaeli anasimama, na kufunga kazi yake ya upatanisho na rehema ya wanadamu. Tazama Danieli 12:1.

> "Waskati huo Mikaeli atasimama… Wakati huu wa dhiki ukija, kila kesi imeamuliwa; hakuna rehema tena, wala huruma kwa wale wasiotubu. Muhuri wa Mungu aliye hai uko juu ya watu Wake." *Testimonies*, volume 5, 212–213.

Katika muda huo toka 1798 hadi kufungwa kwa rehema, twafaa kutarajia kuona "matukio sawia" na zile historia za Danieli kumi na moja, hasa ile historia inayohusishwa na Danieli 11:30-36. Hebu na tuupitie kwa kifupi utimilifu huo wa kihistoria wa Danieli 11:30-36.

Ile njozi ya Danieli kumi na moja huanza na Alexander Mkuu akiushinda ufalme wa Umedi na Uajemi. Katika aya ya nne, twauona ufalme wa Alexander ukigawanywa sehemu nne kuambatana na wale majemedari wake wanne. Kuanzia aya ya tano na kuendelea, majemedari wanaotajwa ni wawili pekee. Falme hizo mbili zilikuwa ni Seleucus na Ptolemy. Mwingiliano wao huanzisha hadithi inayoendelea ya kung'ang'ania utawala wa dunia hadi kwenye mwisho wa Danieli kumi na moja. Mashindano haya ya utawala yaashiriwa kwenye unabii kama pambano kati ya mfalme wa kaskazini na kusini. Kusini na kaskazini hutegemea ule ufalme aliousimamisha Alexander Mkuu.

Jambo moja muhimu kuhusu hadithi hii ni jinsi maandiko yanavyotambulisha ni nani wafalme hao wa kaskazini na kusini. Kwa kuilinganisha historia iliyonakiliwa na huo ushuhuda wa Danieli kumi na moja, wanahistoria na waanzilishi waligundua kuwa **mfalme wa kaskazini** ulikuwa ni ule ufalme **ulioimiliki sehemu ya kijiografia ya Babeli.** Vilevile waligundua kuwa **mfalme wa kusini** alikuwa ndio ule ufalme ulioimiliki **sehemu ya kijiografia ya Misri.** Kanuni hii katika Danieli kumi na moja huleta pamoja ushuhuda wa Maandiko na kumbukumbu ya historia. **funguo huu wa kijiografia** ndiyo kanuni ambayo tutaitumia katika Danieli 11:40-45 tunapoanza kutambulisha ni akina nani hao wafalme wa kaskazini na kusini. Ukweli huu wa kihistoria bila shaka, ni mojawapo ya vidokezo, ambavyo Roho wa Unabii alinuia kutuelekeza wakati ulipowadia wa kuuleta unabii huu kwenye "utimilifu wake kamili."

Kwenye aya za kwanza kumi na tatu, twauona mtiririko wa historia ukielezewa, wkati falme tofauti zilianguka na kuinuka. Katika aya ya kumi na nne twaona maudhui ya kimsingi ya Danieli kumi na moja yakitambulishwa kwa mara ya kwanza kwenye njozi kwa maneno haya, "wahuni wa watu wako." Aya hii yataja kuwa "wahuni" hawa "watayathibitisha maono" hayo. Uriah Smith alizungumzia fungu hili katika aya ya 14 kwa maoni yafuatayo:

> "'**Kuyathibitisha maono hayo**.' **Warumi**, zaidi ya watu wengine, ni **wahusika hasa wa unabii wa Danieli**. Mwanzo wa kuingilia kwao katika shughuli za mataifa haya, kumetajwa hapa kuwa ni kuthibitisha, au kuonyesha, ukweli wa njozi iliyotabiri kuwepo kwa utawala kama huo." *Daniel and the Revelation*, 244.

Toka hapa kuendelea, njozi hii yaifafanua historia ya Roma ya kishenzi au ya kipapa. Katika aya ya ishirini, twaipata Roma ya kishenzi ikimwamuru Yusufu alipe ushuru huko Bethlehemu. Katika aya ya ishirini na mbili, Roma ya kishenzi yamvunja "jemadari wa agano," kwa kumsulubisha Kristo.

Katika aya ya ishirini na nne, twauona muda wa utawala wa Roma ya kishenzi ukiwa umejumuishwa ndani ya muda wa unabii wa kibiblia. Fungu la mwisho la aya hii laitaja miaka 360 kama wakati ambao Roma ya kishenzi ingeutawala ulimwengu kwa maneno haya, "hata kwa muda." Uriah Smith anakubaliana na wale waanzilishi wengine na pia wanahistoria kuhusu mwanzo na kikomo cha unabii huu wa wakati:

> "Vita hivyo vilipiganwa mnamo Septemba 2, 31 B.C., ufuoni mwa guba la Ambracia, karibu na mji wa Actium. Ulimwengu ulikuwa hatarini……
>
> "Vita hivi bila shaka **vyauthihirisha mwanzo wa ule 'wakati'** uliotajwa katika aya ya 24. Kwa vile katika 'wakati' huu hila zake zilitarajiwa kutungwa juu ya **ngome, au Roma**, twaweza kuhitimisha kuwa **mwishoni mwa kipindi hicho,** utawala wa magharibi ungekoma, au badiliko lingetendeka kwenye milki kiasi kwamba mji huo haungechukuliwa kama maskani ya serikali. **Kuanzia 31 B.C., 'wakati' wa kiunabii, ama miaka 360, ungetuleta hadi A.D. 330.** Hivyo basi ni ukweli hakika kuwa **makao makuu ya milki yalihamishwa toka Roma hadi Constantinople** naye Constantino Mkuu **mwaka huo huo**." Ibid, 262-264; soma pia Encyclopedia Britannica, 11th Edition, Vol. VII, p. 3, art., "Constantinople."

Ile miaka 360 ya Roma ya kishenzi kuutawala ulimwengu ilikuwa mkabala na ule muda wa kiunabii wa miaka 1260 ya utawala wa Roma ya kipapa. Hata hivyo cha muhimu katika somo letu hili, ni kuwa utawala huo wa Roma ya kikafiri hufikia kikomo pale zile aya hasa alizoziangazia Dada White huanzia. Aya za 30-36 huizungumzia historia inayouelezea mpito toka Roma ya kishenzi hadi ile ya kipapa. Tutapata kuwa matukio na matendo ndani ya kipindi hicho cha mpito, huenda sambamba na ule mtiririko wa matukio kwenye aya za 40-45. Tunapoanza kuzitazama aya za 30-36, twamrejelea tena Uriah Smith pale anapozungumzia Danieli 11:29:

> "Wakati huo ulioteuliwa huenda ni ule wakati wa aya ya 24, ambao ulitajwa hapo awali. Ulifikia kikomo, kama ilivyoonyeshwa, mwaka wa A.D. 330…. **Kuondolewa kwa makao makuu ya milki hadi Constantinople ilikuwa ni ishara ya kuanguka kwa milki hiyo.** Ndipo Roma ikaupoteza umaarufu wake….
>
> "[Tukiendelea, lakini sasa kuangazia aya ya thelathini.] **Je, meli hizo za Kitimu ni nini**, ambazo zilikuja kinyume na utawala huu, na je, harakati hii ilifanywa lini?… Carthage.
>
> "Je, vita vya majini dhidi ya Carthage kama kituo cha utenda kazi vimewahi kufanywa dhidi ya Milki ya Roma? Twafikiria kuhusu ule uvamizi wa kutisha wa **Vandals** dhidi ya Roma chini yule **Genseric** mkatili, kisha twatoa jibu la kukubaliana kwa urahisi." Ibid, 266-267.

Tukitumia Danieli 11:30-36 kama muhtasari wa historia iliyotambulishwa na Roho wa Unabii, twaona kuwa historia hii ya kale ilikuwa ni **wakati wa mpito** kwa Roma. Roma ya kishenzi ilikuwa karibu kuondoka kwenye onyesho la historia kama mtawala wa dunia, huku Roma ya kipapa ikijiandaa kulijaza pengo hilo. Danieli saba huzumngumzia mpito huo.

Katika Danieli 7:23–24 twapata kuwa **baada** ya "ufalme wa nne" kuinuka, "**mwingine utainuka**." Haya ni maelezo ya kule kuanguka kwa Roma ya kishenzi na kuinuka kwa Roma ya kipapa. Katika unabii wa Danieli saba twaona kuwa mfalme

huyu wa tano "**atawashusha wafalme watatu**," huku akipaa na kuyatwaa mamlaka. Genseric, mfalme wa hao Vandals, alikuwa ni mmoja wa wafalme hao watatu.

Wakati Roma ya kipapa ikiinuka na kuyatwaa mamlaka, ililazimu **pembe tatu**, ama falme tatu, kung'olewa ili kuitayarisha njia. Historia hii yenyewe ni marudio ya historia nyingine ya hapo awali ipatikanayo katika Danieli kumi na moja, kwani wakati Roma ya kishenzi ilipoutwaa utawala wa ulimwengu, ililazimika kwanza **kuzishinda eneo tatu**. Katika Danieli 8:9 twaiona ile "pembe ndogo," inayoashiria Roma ya kishenzi, ikisonga "kuelekea **kusini**, kuelekea **mashariki,** na kuelekea **ile *nchi* ya uzuri**," hivyo kueleleza pande za ushindi ilizozifuata Roma pale ilipouleta ulimwengu chini ya utawala wake. Twainakili hasa historia hii, kwani yule mfalme wa kaskazini katika Danieli 11:40-45, vilevile angevishusha **vitu vitatu**, kabla ya kuyatwaa mamlaka ya ulimwengu.

Katika Danieli 11:30–36 twaona kuwa utawala wa Roma ya kishenzi wazidi kudhoofika kimamlaka. Hapo awali, ilipotishwa na zile falme zingine, Roma ilizishinda. Lakini sivyo kwa wakati huu. Pale Roma ilipoondoka kupigana vita, "ilighadhabika" - **kwa sababu ya uwezo wake wa kushinda**. Katika kipindi hiki zile "pembe tatu" zilizokuwa zikizua vita dhidi Roma ya kishenzi, zilikuwa pia zikizua vita vya kithiolojia dhidi ya Ukatoliki.

Pembe hizo tatu, zilizoashiria mataifa ya Heruli, Goth na Vandals ziliifuata imani ya Kiariani. Katika kipindi hiki Justinian alimtangaza askofu wa Roma kuwa ndiye **kichwa cha kanisa**, vilevile **mrekebishaji wa uasi**, katika jaribio la kuizuilia imani ya Kiariani isije ikayatawala mafundisho ya Kikatoliki. Juhudi hizo za Justinian za kuyashikilia mafunzo ya Kikatoliki dhidi ya uvamizi wa Kiariani zilifungua mlango kwa Kanisa la Katoliki kupiga marufuku baadhi ya vitabu ambavyo viliyatishia mafundisho hayo yao ya kibinadamu. Marufuku hayo yaliijumlisha Biblia, kwani walianza kufundisha ya kuwa ni wazee wa kanisa pekee ambao wana uwezo wa kuisoma pasipo hatari yoyote. Shambulizi hili dhidi ya Biblia lilikuwa ndiyo "gadhabu dhidi ya lile agano takatifu," nao uteuzi huo wa askofu wa Roma kuwa kichwa cha kanisa, yalikuwa ni yale "kuwasikiliza walioacha hilo agano takatifu," katika aya ya thelathini.

Aya ya thelathini na moja yanakili kuwa, "na wenye silaha watasimama upande wake" Huku historia na unabii zikisonga mbele ili kuweka Roma ya kipapa juu ya kiti cha enzi cha ulimwengu, twampata Clovis, mfalme wa Ufaransa, akiusalimisha upanga wake na nchi, kwa Upapa. Ufaransa ilikuwa taifa la kwanza la Kikatoliki, pia wa kwanza miongoni mwa falme za Ulaya kuikana imani yao ya kishenzi na kuukumbatia Ukatoliki, hivyo kuyakabidhi mamlaka yao kwa Upapa. Muungano huu ulikuwa ni njia na mbinu za kuzishinda zile pembe tatu za Kiariani. Unabii ulifundisha ya kuwa pembe hizi tatu zingeng'olewa kabla ya Upapa kuchukua mamlaka juu ya ulimwengu.

Clovis na zile pembe zingine za Ulaya hawakuzitumia tu fedha zao na **silaha** kuzishusha pembe hizo tatu, bali pia waliusitisha (**wakauondoa**) upinzani wao wa kishenzi dhidi ya Ukatoliki. Ukweli huu umeelelezwa kama "waliondoa ya daima."

Akiizungumzia hiyo "ya daima," Dada White asema:

> "Kisha nikaona kuhusiana na 'ya daima' (Danieli 8:12) kwamba neno 'dhabihu' lilitumiwa tu kwa hekima ya wanadamu, wala halihusiani kabisa na sentensi, na kwamba Bwana alitoa usahihi wake kwa wale waliotangaza ujumbe wa saa ya hukumu. Umoja ulipokuwepo, kabla ya 1844, karibu wote waliungana na mtazamo sahihi wa neno 'udaima,' lakini katika machafuko tangia mwaka 1844 mitazamo mingine imekuwa ikishikiliwa, na giza na machafuko vikafuata." *Early Writings*, 74–75.
>
> Waanzilishi waliangazia hiyo "ya daima," kama iliyoashiria ukafiri. Uriah Smith auelezea ufahamu wao:
>
> "[Neno hilo *kafara*] lapaswa kuwa 'ukiwa.' Dhihirisho hilo lina maana ya **utawala uletao ukiwa**, ambao lile chukizo la uharibifu **ni mfanano tu**, na ambalo **lauandama** wakati wake ufikapo. Basi yaonekana wazi kuwa **ukiwa huo 'ya kudumu' ulikuwa ni ukafiri**, nalo lile **'chukizo la uharibifu' ni upapa**… Katika sura ya tisa, Danieli azungumzia ukiwa na machukizo katika **hali ya wingi**. Hivyo basi, machukizo zaidi ya moja, hulisaga kanisa; yaani, tunapolizungumzia kanisa, **ukafiri na upapa, vyote viwili ni machukizo**.
>
> Lakini jinsi vilivyotofautishwa, kunao ufinyu wa lugha. Mmoja ni ule ukiwa 'ya udaima,' huku mwingine hasa ni uhalifu au 'chukizo' la uharibifu.
>
> Ni jinsi gani hiyo 'ya daima', au ushenzi, uliweza kuondolewa? ... **Kubadili dini kwa Clovis** [A.D. 496] ilisemekana kuwa sherehe ya kumtawaza mfalme huyo wa Ufaransa kwa majina ya 'Jalali Mkristo Zaidi' na 'Kifungua Mimba wa Kanisa.' Kati ya wakati huo na A.D. 508, [pembe zinginezo za Ulaya] zililetwa katika utiifu.
>
> "Kutoka … A.D. 508, Upapa ulipata ushindi juu ya ushenzi… Wakati falme mashuhuri za Ulaya ziliuacha uhusiano wao na ushenzi, ilikuwa tu ni kuyaendeleza machukizo yake katika hali nyingine; kwa kuwa Ukristo jinsi unavyodhihirishwa na **Kanisa Katoliki la Roma ulikuwa, na bado ni, ushenzi tu uliobatizwa**." *Daniel and the Revelation*, 270–272.

Historia ya Danieli 11:31 ni maelezo ya falme za kishenzi za Ulaya zikija kuusaidia Upapa ili wauketishe juu ya kiti cha enzi cha ulimwengu. Kuondolewa kwa hiyo "ya kudumu," ni maelezo ya jinsi walivyouacha ushenzi. Maneno hayo "kuondoa" yanabeba maana mara-mbili kwani hayafundishi tu kuhusu ondoleo, bali pia maana ya pili huleta wazo la – **kuinua juu**. Wakati ushenzi ulipotupiliwa mbali na falme za Ulaya, pale walipojisalimisha kwa Ukatoliki, ushenzi hakika uliinuliwa juu, kwani Ukatoliki ndilo dhihirisho kubwa zaidi la ushenzi katika historia – japo kavikwa vazi la Ukristo.

Mnamo A.D. 508 falme za Ulaya zilianza kuzua vita dhidi ya zile nchi zinazoashiriwa na "pembe tatu," na kufikia 538 pembe ya mwisho miongoni mwa hizo tatu ilishindwa, ndipo Upapa ukaketi juu ya kiti cha enzi cha ulimwengu. Kisha lile "chukizo lifanyalo ukiwa," linaloashiria Upapa, likasimamishwa.

Katika aya za 32-35, twaona kielelezo cha yale mateso ya Enzi za Giza, huku sehemu ya mwisho ya aya ya thelathini na tano ikionyesha mwisho wa ile miaka 1260 kwa maneno haya, "*hata* wakati wa mwisho; kwa maana ni kwa wakati ulioamriwa." Kirai hiki chatupeleka hadi aya ya arobaini. Lakini kabla ya Danieli kufika aya ya arobaini, aya za 36-39, huyaleta maelezo ya mada kuu ya Danieli – yaani Upapa:

> Naye mfalme atafanya kama apendavyo; naye atajitukuza na kujiadhimisha juu ya kila mungu, naye atanena manenoi ya ajabu juu ya Mungu wa miungu, naye atafanikiwa mpaka ghadhabu itakapotimia; maana yaliyokusudiwa yatafanyika. Danieli 11:36.

Bila shaka huu ni Upapa, naye Paulo alifafanua fungu hili katika tamko lake lenye nguvu sana kuhusu Upapa:

> Mtu awaye yote asiwadanganye kwa njia yo yote; maana haiji, usipokuja kwanza ule ukengeufu; akafunuliwa yule mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu; yule mpingamizi, ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu. 2 Wathesalonike 2: 2-4.

Dada White amuunganisha huyo mfalme wa Danieli ambaye hutenda "apendavyo," na yule "mtu wa kuasi" wa Paulo, kuuelezea Upapa:

> "Mapatano haya kati ya ukafiri na Ukristo yalisababisha kutokea kwa '**mtu wa kuasi**' aliyetabiriwa katika unabii kama **mpingaji na ajiinuaye mwenyewe** juu ya Mungu.ufunuo huo mkubwa kabisa wa dini ya uongo ndio kazi bora kabisa ya mamlaka ya shetani – kazi ya mfano bora ya jitihada zake za yeye mwenyewe kuketi juu ya kiti cha enzi ili kuitawala dunia **kulingana na mapenzi yake.**" *The Great Controversy*, 50.

Tunapozidi kujifunza Danieli 11:40-45 tutauona mfululizo wa kihistoria ndani ya aya hizi ambao waenda sambamba na historia tuliyoichambua. Tutatoa ushahidi kuonyesha kuwa Danieli 11:40 ni maelezo ya vita vya kiroho kati ya Upapa na ukanaji Mungu ulioanza mnamo 1798. Tutaonyesha kuwa Ufaransa uliivaa taji ya mfalme wa kusini mnamo 1798, lakini mwaka wa 1917 taji hiyo ilipitishwa kwa mrithi wake – Urusi, iliyojulikana baadaye kama Muungano wa Sovieti. Tutaonyesha kuwa mfalme wa Kaskazini mnamo 1798 alikuwa ni Upapa, na kuwa Upapa ungali bado umeivaa taji hiyo ya kinabii.

Aya ya arobaini yafundisha kuwa mwanzoni, kwenye vita baina ya mfalme wa kusini na mfalme wa kaskazini, mfalme wa kaskazini **alighadhabishwa** kwa uwezo wake wa kuushinda ufalme wa kusini. Ama kwa kweli, vita hivyo huanza wakati mfalme huyo wa kaskazini anapolipokea jeraha la kufisha, huku akipokonywa ufalme wake wa kisiasa.

Akiandika kuhusu Danieli 11:30, Dada White alizungumzia wakati fulani ambapo Roma ilikuwa haiwezi kumshinda adui wake. Ufunuo kumi na tatu yauelezea Upapa kama kile kichwa kilichopokea jeraha la kufisha. Vita hivyo na ile huzuni ya Upapa vyafafanuliwa pale mfalme wa kusini "atashindana" na mfalme wa kaskazini katika Danieli 11:40.

Lakini aya ya arobaini yafundisha kuwa badiliko lingetokea. Baadaye, mfalme wa kaskazini angerejea, na huku akiungana na nguvu za kijeshi na za kiuchumi, amfagilie mbali huyo mfalme wa kusini. Tutaona kuwa nguvu za kiuchumi na za kijeshi zilikabidhiwa mfalme huyo wa kaskazini katika vita hivi, jinsi Clovis alivyokuja kuusaidia Upapa hapo awali.

Tutaona kuwa katika utimilifu wa aya hii Muungano wa Kisovieti, 'mfalme wa kusini' wa kisasa, ulifagiliwa mbali na Upapa – yaani mfalme wa kaskazini. Kufagiliwa huku kulitimizwa kwa muungano na Marekani. Matukio haya ya hivi majuzi hayaendi tu sambamba na historia inayoangaziwa na Dada White katika Danieli 11:30-31, bali pia yaunga mkono ushuhuda wa Ufunuo kumi na tatu, ambao waitambulisha Marekani kama yule mnyama ajaye kuusaidia Upapa mwisho wa ulimwengu.

Tumezingatia sehemu zile tatu za kijiografia ambazo Roma ya kikafiri ilizishinda pale ilipoketi juu ya kiti cha enzi cha ulimwengu. Tumelinganisha na kung'olewa kwa zile pembe tatu kabla ya kuketi kwa Upapa juu ya kiti cha enzi cha ulimwengu, ambao ulikuwa ndio mwanzo wa Enzi za Giza. Tutaona katika sura inayofuata ya kuwa aya ya arobaini ni moja ya hatua tatu anazozichukuwa Babeli ya kisasa ili kurejea kwenye kiti cha enzi cha ulimwengu siku hii yetu. Hatua ya kwanza ilikuwa ni kutekeleza kuanguka kwa yule mfalme wa kusini, yaani Muungano wa kitambo wa Sovieti, nayo hatua hii sasa ni historia iliyopita.

Hatua ya pili ni aya ya arobaini na moja, pale mfalme wa kaskazini anapouchukuwa utawala wa kiroho juu ya ile nchi ya uzuri. Nchi hiyo tukufu katika aya hii sio nyingine bali ni Marekani, (mnyama wa pili wa Ufunuo kumi na tatu). Kwa kuingia kwenye muungano mchafu na Vatikani ili kumwangusha adui wao mmoja, Marekani ilianza safari ya kujisalimisha kwake mikononi mwa upapa kwani iliukana urithi wake kama shujaa wa Uprotestanti. Kwa ufafanuzi, Uprotestanti unamaanisha: kuipinga Roma. Haiwezekani kuipinga Roma huku ungali rafiki yake.

Kama vile Clovis alivyousaidia Upapa kwa kuufadhili kijeshi na kiuchumi, kupitia kuukubali Ukatoliki badala ya ukafiri, vivyo hivyo Marekani haikutoa tu usaidizi wa kijeshi na wa kiuchumi ili kuuangusha Muungano wa Sovieti, bali pia ilianza sehemu yake ya kinabii kama Uprotestanti ulioasi, au "nabii wa uwongo" wa Ufunuo kumi na sita. Kutimia kwa aya ya arobaini hugeuza ukweli wa Ufunuo kumi na sita kuwa "ukweli wa sasa" – wakati wanadamu sasa waongozwa kuelekea Harmagedoni.

Hatua ya tatu ni aya ya arobaini na mbili ambapo ulimwengu, ambao huashiriwa kiunabii na Misri, utakamatwa na mkono wa chuma wa Roma. Kisha katika aya ya arobaini na tatu, uchumi wa ulimwengu utakuja chini ya nguvu za mfalme wa kaskazini. Wakati uchumi wa ulimwengu unakuja chini ya udhibiti wa mfalme huyo wa kaskazini, basi Upapa umerejea nafasi yake ya mamlaka kama mtawala wa kisiasa. Ama katika ishara ya unabii, upapa kwa mara nyingine tena umekuwa "mnyama" wa unabii wa Biblia. Upapa uliacha kuwa "mnyama" wa unabii wa Biblia mnamo 1798, japo uliendelea kuwa "mwanamke" wa unabii wa Bibila. Lile "jeraha la kufisha" latambulisha wakati upapa uliacha kuutawala ulimwengu kama mamlaka ya kisiasa, (mnyama). Wakati utakaporejea kwenye nafasi hii, jeraha lake litakuwa limepona kabisa.

Aya ya arobaini na nne yaizungumzia mvua ya masika na mateso dhidi ya watu wa Mungu, huku aya ya arobaini na tano ikielezea mgawanyiko wa ulimwengu katika makundi mawili tunapoikaribia Harmagedoni. Tutavipata vipengele vingi vya kuvutia tunapozidi kujifunza aya hizi. Tunapoendelea na somo hili, hatutaitetea tu misingi iliyowekwa hapa kwa undani, bali pia tutazidi kuulinganisha mfululizo huu na yale maonyesho na historia ambayo Dada White alituelekeza.

Danieli 11:30-36 sio tu mfululizo wa historia uliowekwa kama ruwaza ya kutumika ili kuelewa Danieli 11:40-45, bali ni historia kamili ya kuinuka kwa mara ya kwanza kwa Upapa kwa utawala mwanzoni mwa Enzi za Giza. Roho Mtakatifu, kupitia Dada White, atuelekeza hadi mara ya kwanza kabisa ya Upapa kukikalia kiti cha enzi cha ulimwengu kama ruwaza ya historia ya kulinganishwa mara ya mwisho ya Upapa kuketi juu ya kiti cha enzi ulimwengu.

Kile kilicho mbele ya kanisa na ulimwengu ni kupona kwa jeraha la kufisha la Upapa? Jeraha hilo lilikuwa ni pale Upapa ulipoupoteza uwezo wa kutawala kama serikali – wala sio kukoma kama kanisa.

"Ushawishi wa Roma juu ya zile nchi zilizoutambua utawala wake ungali bado haujakwisha. Nao unabii unatabiri **kurejea kwa mamlaka yake**. 'Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti, na pigo lake la mauti likapona: na dunia yote ikamstaajabia mnyama yule.' Aya ya 3. Kupata jeraha hilo la kufisha maana yake ni **lile anguko la Upapa mnamo 1798** … Paulo ataja wazi kuwa **yule 'mtu wa kuasi' ataendelea hadi kule kuja mara ya pili.** 2 Wathesalonike 2:3-8. Hadi mwisho wa nyakati ataiendeleza kazi hiyo yake ya udanganyifu …

"Na hebu ikumbukwe kwamba, Rumi inajivuna kuwa kamwe haibadiliki. Kanuni za Gregory VII na Innocent III bado ni kanuni za kanisa la Romani Katoliki. Na **lingekuwa lina mamlaka** kama lilivyokuwa nayo zamani, lingeyatumia kwa nguvu kubwa sasa kama lilivyotumia katika karne zilizopita. Waprotestanti wanaelewa kidogo sana kile wanachokifanya wakati wanaposhauri na kupendekeza kukubali msaada wa Rumi, katika kazi ya kutukuza Jumapili. Wakati wao wanapokuwa wakidhamiria kutimiza lengo lao, **Rumi yenyewe inadhamiria kujiimarisha upya katika mamlaka yake, kupata tena, utawala wake iliyoupoteza. Ngoja kanuni ziwekwe katika nchi ya Marekani ili kanisa liweze kutumia au kuongoza mamlaka ya serikali;** hapo ndipo ushikaji wa dini utakapolazimishwa na sheria za serikali; kwa ufupi, ni kwamba mamlaka ya kanisa na serikali zitatawala dhamiri (zitakuwa na amri juu ya dhamiri za watu, namna ya kuabudu na siku ya kushika), na **ushindi wa Rumi katika nchi hii (Marekani) ni wa hakika.**"

"Neno la Mungu limetoa onyo kwa **hatari inayokaribia**; ngoja onyo hili lipuuzwe, na hapo, ndipo **ulimwengu wa Kiprotestanti utakuja kugundua** makusudi ya Rumi, **wakati ukiwa umechelewa sana kuuepuka mtego.** Kanisa la Romani Katoliki linakuwa kimyakimya kuelekea kwenye utawala. Mafundisho yake yanatumiwa katika kumbi za kutunga sheria (mabunge). Katika makanisa, na katika mioyo ya wanadamu. Linalundika maghorofa yake ya kifahari na majengo makubwa katika maficho ya siri nahali ambapo **mateso yake ya awali yatakapofanyikia wakati yatakapojirudia.** Linaimarisha Majeshi yake kwa siri na pasipo kutiliwa wasiwasi ili lije kuendelea na kutimiza malengo yake lenyewe **wakati muda utakapokuwa umewadia wa lenyewe kupambana.** Linachohitaji zaidi ni eneo linalofaa, na hali tayari limeshatolewa kwake. Hivi karibuni tutaona na kugundua kusudi la msingi la Romani. Yeyote atakayeamini na kutii neno la Mungu atakabiliana na mashutumu na mateso." *The Great Controversy*, 579–581.

"Lipo hitaji kubwa la kukichunguza kitabu cha Danieli na kitabu cha Ufunuo, na kujifunza mafungu hayo kikamilifu, ili tuyajue yaliyoandikwa." *Evangelism*, 363.

Wafalme wa Kusini na Kaskazini

Sasa tutawatambulisha wafalme wale wawili wa Danieli 11:40-45. Katika sura ya mwisho tulipitia kwa kifupi njozi nzima ya Danieli kumi na moja na tukapata ya kuwa kiunabii, wafalme wa kaskazini na kusini walitambulishwa katika kumbukumbu ya historia, kwa kuutambua utawala wa dunia ambao ulimiliki eneo la Misri au Babeli. Utawala ulioimiliki Misri ulitambuliwa kwenye unabii wa Danieli kumi na moja kama mfalme wa kusini, huku utawala ulioimiliki Babeli ulieleweka kama mfalme wa kaskazini. Kanuni hii itaturuhusu kuwatambua wafalme hao kote katika Danieli kumi na moja.

Ili kuitumia kanuni hii katika Danieli 11:40-45, tutazitumia kanuni mbili za unabii ambazo huathiri kutambulishwa kwa wafalme hao tangu 1798 kuendelea.

Louis F. Were alikuwa ni mwandishi Mwadventista ambaye kiini cha maandishi yake mengi kilikuwa ni ufahamu wa unabii. Japo sasa ameiaga dunia, vitabu vyake vingali bado vipo. Tutazitazama kanuni hizi mbili kama zilivyowasilishwa katika mojawapo ya vitabu vyake. Kanuni ya kwanza yaitwa **"Ulimwengu Mzima Kuashiriwa na Mahali Maalum."**

> "Manabii wote waliitumia kanuni ya **Ulimwengu Mzima Kuashiriwa na Mahali Maalum.**" Baadhi ya mifano ya matumizi haya ni kama ifuatayo: "'Unabii wake [Zefania] kuhusu hukumu iliyokaribia juu ya Yuda watumika kwa uzito huo huo kuelezea zile hukumu zitakazoshuka juu ya *walimwengu* wasiotubu wakati wa kurudi kwa Kristo mara ya pili.' *Prophets and Kings*, 389. 'Kristo aliona ndani ya Yerusalemu ishara ya *ulimwengu* … ulioharakisha kukutana na hukumu za Mungu.' 'Unabii wa Mwokozi kuhusu kumwagwa kwa hukumu za Mungu juu ya Yerusalemu utatimia tena … maangamizi ya ulimwengu.'" *The Great Controversy*, 22, 36.
>
> "Mifano *chungu nzima* yaweza kudondolewa kuhusu matumizi ya mahali maalum kuashiria matukio ya ulimwengu mzima mnamo mwisho wa nyakati – **kanuni hii hutumika kote ndani ya Biblia**. Kama alivyotaja Dr. Angus: 'Kutoka kwa tabia iliyofanana ya mgawo wa kale huibuka upekee mwingine wa unabii. Haizungumzi tu *lugha yao*, bali mara nyingi huwa na matumizi *mara dufu* …' *Bible Handbook*, 285." *Bible Principles of Interpretation*, 25. [Herufi mlazo ni za asili; mkazo wa herufi nzito umeongezwa.]

Kanuni ya pili muhimu ya kinabii na yenye uhusiano wa karibu na hiyo tuitumiayo katika kuwatambulisha wafalme wa Danieli kumi na moja yaitwa, **"Vitu vya Israeli Sasa ni vya Kanisa."** Kanuni hii huuchora msitari wa kugawanya ili kuamua iwapo tutayafahamu majina au sehemu za unabii kama tafsiri yake ni ya kihalisi au ni ya kuashiria.

> "Kanuni hii **ni ya kimsingi** katika kuufahamu u**nabii wa Danieli na Ufunuo** – ni **kanuni ya kimsingi kwa ujumbe wa mwisho wa Mungu.** Bwana alimpa Paulo kazi ya kipekee ya kuonyesha jinsi kanisa ilivyokuwa 'Israeli ya Mungu,' kuwa ahadi kwa Israeli halisi zingetimizwa kupitia ujuzi wa kanisa:
>
> "'Si watoto wa mwili walio watoto wa Mungu, bali watoto wa ile ahadi wanahesabiwa kuwa wazao.' Warumi 9:8. '*Na kama ninyi ni wa Kristo*, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi.' Wagalatia 3:29 ….
>
> "'Twahesabiwa pamoja na Israeli …. Ahadi *zote* za mibaraka kupitia utiifu, ni *zetu*.' *The Ministry of Healing*, 405. 'Nilionyeshwa kuwa wale wanaojaribu kumtii Mungu … ndio watu wateule wa Mungu, yaani *Israeli yake ya kisasa*.' *Testimonies*, vol. 2, 109.… Kanuni ya kuwa **historia ya Israeli ni kifanani au unabii kuhusu ujuzi wa kanisa,** huendelea kutumika ndani ya Roho ya Unabii." Ibid., 11-12.

Sasa tutaitumia kanuni iliyotajwa hapo awali katika kuwatambulisha wafalme wa Danieli kumi na moja. Mfalme wa kaskazini ni utawala uliomiliki Babeli. Mfalme wa kusini alitambulishwa na utawala uliomiliki Misri. Kwa vile 1798 ilikuwa ni baada ya msalaba, yatupasa kujaribu kuitambua Misri ya kiroho na Babeli ya kiroho. Vilevile sharti tuzitambue falme zilizowamiliki.

Tutaanza na mfalme wa kusini. Katika Biblia, neno kusini hutoka kwenye neno la Kiebrania linalohusishwa na Misri. Neno hilo humaanisha "kusini."

> "**kusini** – 5045: kutoka mzizi usiotumika unaomaanisha *kuchomwa na jua*; ***kusini*** (kutokana na ukame wake); hasa Negeb au **wilaya ya kusini** ya Yuda, mara kwa mara, **Misri** (kama kusini mwa Palestina): **kusini** (nchini)." *Strong's Exhaustive Concordance of the Bible*.

Ufunuo 11:8 kitamathali huitambulisha Ufaransa kama "mji ule mkuu," na kuuita "kiroho," "Sodoma na **Misri**."

Nasi tuna lile neno la unabii lililo imara zaidi, ambalo, mkiliangalia, kama taa ing'aayo mahali penye giza, mwafanya vyema, mpaka kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu.

2 Peter 1:19.

"'**Mji mkuu**' huo, ambao kwenye mitaa yake waliuliwa wale mashahidi wawili, na ambamo maiti zao zimelala, **ndio Misri 'kiroho'**. Miongoni mwa mataifa yote yaliyowakilishwa kwenye historia ya Biblia, Misri ndiyo iliyodhihirisha ujasiri zaidi katika kukana kuwepo kwa Mungu aliye hai na kuzipinga amri zake. Hakuna mfalme aliyejitokeza kuuasi utawala wa Mbingu hadharani na kwa ukatili zaidi ya mfalme wa Misri. Wakati alipoletewa ujumbe na Musa, kwa jina la Bwana, Filauni alijibu kwa kiburi: "Huyo Yehova BWANA ni nani, hata nimtii na kuruhusu Israeli waende? Simjui huyo Yehova, wala sitawaruhusu Israeli waende.'' Kutoka 5:2. Huu ndio ukanaji Mungu; nalo taifa linalowakilishwa na Misri lingetoa matamshi sawia na hayo ya kuyakana madai ya Mungu aliye hai, na lingedhihirisha roho sawa na huyo wa kutoamini na ujeuri.

'Mji huo mkuu' pia walinganishwa, 'kiroho,' na Sodoma. Upotovu wa Sodoma kwa kuzivunja sheria za Mungu ulidhihirika hasa katika uasherati. Na dhambi hii vilevile ilikuwa ni sifa iliyopita zingine, ya taifa ambalo lingetimiza ainisho la andiko hili.

"Kulingana na maneno ya nabii, basi, **muda mfupi kabla ya mwaka wa 1798**, utawala fulani wenye asili na tabia ya kishetani ungeinuka ili ufanye vita dhidi ya Biblia. Na katika nchi ambapo ushuhuda wa mashahidi hao wawili ungenyamazishwa, ungedhihirishwa **ule ukanaji Mungu wa Filauni** na uasherati wa Sodoma.

"Unabii huu umepata utimilifu kamili zaidi katika historia ya Ufaransa. Wakati wa yale mapinduzi ya 1793, 'ulimwengu kwa mara ya kwanza ulilisikia kongamano la watu, waliozaliwa na kuelimishwa katika ustaarabu, na waliojitwalia haki ya kulitawala mojawapo ya mataifa mazuri zaidi ya Ulaya, wakiziinua sauti zao kwa pamoja na kuukana ukweli ulio wa dhati zaidi kuwahi kupokelewa na moyo wa mwanadamu, **na kuikanusha kwa pamoja ile hali ya kumwamini na kumwabudu Mungu**.' —Sir Walter Scott, *Life of Napoleon*, vol. 1, ch. 17. '**Ufaransa ndilo taifa pekee ulimwenguni ambalo kumbukumbu sahihi bado ingali ipo, ambalo kama taifa liliinua mkono wake na kuasi waziwazi dhidi ya Muumbaji wa mifumo ya sayari**.' *Blackwoods Magazine*, November, 1870." *The Great Controversy*, 269–270.

Kitambulisho cha **"mfalme wa kusini"** katika unabii wa Danieli kumi na moja huamuliwa kwa kujua ni utawala gani unaoidhibiti **Misri**. Mnamo 1798 taifa linalotambulishwa na Biblia kama lililokuwa na sifa za kiroho sawa na zile za Misri, ni Ufaransa. **Ufaransa ilikuwa ndiye mfalme wa kusini mnamo 1798**.

Danieli 11:40 hutaja kuwa wakati wa mwisho, mfalme wa kusini **angemsukuma** mfalme wa kaskazini. Neno kushindana likitafsiriwa humaanisha kufanya vita dhidi ya.

"**sukuma** – 5055: *kumba* kwa pembe; kitamathali *kufanya vita* dhidi ya: dunga, sukuma (chini)." *Strong's*.

Danieli vilevile hutumia **sukuma** kuelezea ushindi wa kijeshi wa Wamedi-Waajemi.

> Nikamwona huyo kondoo mume akisukuma upande wa magharibi, na upande wa kaskazini, na upande wa kusini; wala hakuna mnyama yeyote awezaye kusimama mbele yake, wala hakuna myana yeyote awezaye kupokonya mkononi mwake; lakini alitenda kama alivyopenda mwenywe, akajitukuza nafsi yake. Danieli 8:4.

Katika Danieli 11:40, neno sukuma huashiria vita fulani vitakavyoanza wakati wa mwisho – 1798. Vita hivi vingeelekezwa dhidi ya mfalme wa kaskazini, na vingeanzishwa na mfalme wa kusini – Ufaransa. Je, ni utawala gani ambao uliidhibiti milki ya Babeli mnamo 1798? Kama vile **kusini** yahusishwa na Misri katika Biblia, **kaskazini** ni eneo linalohusishwa na Babeli.

> "angalieni, nitapeleka watu na kuzitwaa **jamaa zote za upande wa kaskazini,** asema Bwana, nami nitatuma ujumbe kwa Nebukadreza, mfalme wa **Babeli,** mtumishi wangu, nami nitawaleta juu ya nchi hii, na juu yao wakaao ndani yake, na juu ya mataifa haya yote yaliyopo pande zote; nami nitawaangamiza kabisa, na kuwafanya kitu cha kushangaza, na kitu cha kuzomewa, na ukiwa wa daima." Yeremia 25:9.

> "Maana Bwana MUNGU asema hivi; Tazama, nitamleta Nebukadreza, **mfalme wa Babeli,** mfalme wa wafalme, juu ya Tiro **toka kaskazini**, pamoja na farasi, na magari ya vita, na wapanda farasi, na jeshi, na watu wengi." Ezekieli 26:7.

Dada White autambulisha utawala unaolihodhi eneo la Babeli ya kiroho:

> "Yule mwanamke (Babeli) wa Ufunuo 17 ameelezewa kama 'aliyevikwa nguo ya rangi ya zambarau, na nyekundu, amepambwa kwa dhahabu, na kito cha thamani, na lulu, naye alikuwa na kikombe cha dhahabu mkononi mwake, kilichojawa na machukizo, na machafu … na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa, la siri, *BABELI MKUU, MAMA WA MAKAHABA*.' Asema nabii 'Nikamwona yule mwanamke amelewa kwa damu ya watakatifu, na kwa damu ya mashahidi wa Yesu.' Babeli pia imetangazwa kuwa 'mji ule mkuu, unaowatawala wafalme wa dunia.' Ufunuo 17:4-6, 18. Ule utawala ambao kwa karne nyingi ulidumisha himaya ya udhalimu juu ya wafalme wa mataifa ya Kikristo, **ndio Roma.**" *The Great Controversy*, 382.

Kahaba huyo wa Roma ni ule utawala unaodhibiti Babeli ya kisasa ama ya kiroho. Kwa hivyo, Upapa ndio "mfalme wa Kaskazini". Anapofafanua kuhusu Ufaransa katika Ufunuo 11:8, Yohana atambulisha Ufaransa kama, **"mji ule mkuu."** Babeli vilevile hutajwa kama **"mji huo mkuu,"** katika Ufunuo 17:18. Katika unabii, mji huwakilisha ufalme.

"Harusi hiyo yawakilisha yale mapokezi ya **Ufalme** na Kristo. **Mji ule Mtakatifu, yaani Yerusalemu Mpya, ambao ndio mji mkuu na mwakilishi wa ufalme huo**, waitwa 'bi harusi, yaani mke wa Mwana kondoo.' Malaika akamwambia Yohana: Njoo huku, nami nitakuonyesha yule Bibi-arusi, mke wa Mwana-Kondoo… Akanichukua katika Roho,' asema nabii, 'akanionyesha **ule mji mkuu, Yerusalemu mtakatifu**, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mwenyezi Mungu.' Ufunuo 21:9-10 … Yeye ataupokea Yerusalemu Mpya, mji mkuu wa ufalme wake, 'ukiwa umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe.' Ufunuo 21:2. Tazama Danieli 7:14. Baada ya kuupokea **ufalme**, Yeye atakuja kwa utukufu Wake, kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana." *The Great Controversy*, 426–427.

Mnamo 1798, Ufaransa, ambayo huelezewa katika Danieli 11:40 kama "mfalme wa kusini", ilianza kufanya vita dhidi ya Upapa, unaosimuliwa kama "mfalme wa kaskazini". Upapa ulipokea jeraha la kufisha mnamo 1798 pale Napoleon, mfalme mkuu wa Ufaransa, alipomshika papa mateka. Upapa uliacha kuwa ufalme kwa wakati huo, kwani ulivuliwa nguvu zake za kiserikali na za kisiasa. Hata hivyo, Upapa haukuacha kuwa kanisa wakati huo. Alizipoteza tu nguvu na mamlaka yake kama ufalme. Jeraha alilolipata mwaka wa 1798 hatimaye litapona pale atakapoirejelea ile cheo yake kama ufalme tawala wa kisiasa.

Katika kitabu, *The Keys of This Blood*, Malachi Martin aipendekeza imani yake ya kuwa yapo mashindano mara tatu ya kuutawala ulimwengu, yaani baina ya Upapa, Muungano wa Sovieti, na Marekani. Yeye aamini kuwa Upapa utarejea kwenye kiti cha enzi cha ulimwengu mwishoni mwa karne hii. Asema kuwa shindano hili ni pambano kati ya nguvu hizo tatu ili kuamua ni nani atakayeudhibiti muundo "siasa za nchi kijiografia" itakayoutawala ulimwengu. Vilevile anafasili kile ambacho Upapa ulikipoteza mnamo 1798:

"Istilahi hii "siasa za nchi kijiografia" ni ubunifu wa hivi majuzi. Ni muundo wa maneno mawili ya Kigiriki, yanayomaanisha 'dunia' na 'mfumo wa kisiasa,' ambayo wagiriki wa kale hawakuwahi kuyaunganisha …

"Mwishoni mwa miaka elfu mbili tangu Paulo alipouonyesha mtazamo wa dini sahihi, mrithi wa 263 wa yule Mvuvi Mkuu asiyejulikana, aongoza na kutawala huko Roma kama kichwa cha dini hiyo ya kijiografia inayoishi ndani ya muundo huo wa kisiasa. Kwani **Yohana Paulo wa Pili sio tu kichwa cha kiroho** cha mwili wa waumini kote ulimwenguni, bali **pia ni mkurugenzi mkuu wa nchi huru** ambayo hutambuliwa kama mojawapo ya jamii ya serikali katika mwisho wa karne hii ya ishirini. Je, inayo malengo na muundo wa kisiasa? Ndio, inayo malengo na muundo wa kisiasa. **Kwani, hatimaye, Yohana Paulo wa Pili kama anayedai kuwa Mwakilishi wa Kristo, hudai kuwa yeye ndiye koti la mwisho la hukumu kwa jamii ya serikali zote kama jamii**." *The Keys of This Blood*, 371, 374–375.

Jeraha hilo la kufisha litapona wakati ulimwengu utakubaliana na mtazamo wa Malachi Martin. Unabii unasema yatatendeka, nao Upapa unazidi kusubiri.

"Na hebu ikumbukwe kwamba, **Rumi inajivuna kuwa kamwe haibadiliki**. Kanuni za Gregory VII na Innocent III bado ni kanuni za kanisa la Romani Katoliki. Na lingekuwa lina mamlaka kama lilivyokuwa nayo zamani, lingeyatumia kwa nguvu kubwa sasa kama lilivyotumia katika karne zilizopita. Waprotestanti wanaelewa kidogo sana kile wanachokifanya wakati wanaposhauri na kupendekeza kukubali msaada wa Rumi, katika kazi ya kutukuza Jumapili. Wakati wao wanapokuwa wakidhamiria kutimiza lengo lao, **Rumi yenyewe inadhamiria kujiimarisha upya katika mamlaka yake,** kupata tena, utawala wake iliyoupoteza. Ngoja kanuni ziwekwe katika nchi ya Marekani ili kanisa liweze kutumia au kuongoza mamlaka ya serikali; hapo ndipo ushikaji wa dini utakapolazimishwa na sheria za serikali; **kwa ufupi, ni kwamba mamlaka ya kanisa na serikali zitatawala dhamiri, na ushindi wa Rumi katika nchi hii (Marekani) ni wa hakika."** *The Great Controversy*, 581.

Sababu nyingine ya kumtambua "mfalme wa kaskazini" kama Upapa ni ile **kanuni ya Biblia ya kuwa unabii wa hivi majuzi huzidisha, hupanua na kuthibitisha unabii wa hapo awali.** Kanuni hii yaitwa, **"Rudia na Upanue."** Louis F. Were aizungumzia kanuni hii:

"Mungu alilichagua taifa la Waebrania kuutangaza ukweli Wake, nao walijielezea kwa *kurudiarudia* – kurudia huko kukiwa ni *upanuzi* wa yale yaliyotangulia …

"Naye Rev. W. F. Wilkinson, M.A., katika kitabu chake 'Personal Names in the Bible,' ukurasa 17, asema: – kulingana na ustadi wa ushairi wa Kiebrania, ikiwa maneno au virai vya maana moja vitajitokeza kwenye vishazi viwili sambamba au kinyume, basi tofauti ya hiyo ya pili kutoka kwa ya kwanza yaonyesha kuwa hayo ni *maelezo*, au *ufafanuzi*, au ongezeko la wazo lililoko kwenye lile la kwanza'…

"Biblia imejaa sio tu marudio ya upanuzi katika aya binafsi, bali pia marudio elezi katika mifano, mahubiri, nabii, historia, n.k.

"Maudhui za Biblia zimeandikwa juu ya mpango wa kupanda. Vitabu vya mapema huweka msingi kwa maendeleo ya baadaye. Utondoti hujikusanya hadi, kama vile mchoraji huitumbukiza burashi yake ndani ya marangi mbalimbali, picha kamili hutokea." *The Certainty of The Angel's Message*, 110–111.

Kwa sababu ya kanuni hii, njozi ya Danieli kumi na moja yafaa kuyarudia na kuyapanua maono ya Danieli ya hapo awali. Katika kitabu cha Danieli kunazo nabii nne. Ndani ya nabii hizi nne twapata ushahidi wa nguvu ya kuwa "mfalme wa kaskazini" ni Upapa. Ushahidi huu msingi wake hasa ni kanuni hiyo ya kurudia na kupanua.

Unabii wa kwanza wa Danieli mbili, waelezea kuhusu mfululizo wa falme tano za dunia zinazofuatwa na ufalme wa mbinguni: Babeli, Umedi-Uajemi, Uyunani, Roma katika awamu mbili (zikiashiriwa na miguu miwili), kisha ufalme

wa mwisho, yaani jiwe lililochongwa kutoka mlimani "pasipo mikono," ambalo huzivunja falme zingine zote na kuijaza dunia nzima. Ufalme huo wa mwisho ni ufalme wa Mungu, ambao utaanzishwa mwisho wa ulimwengu.

Katika unabii ufuatao wa Danieli, upatikanao kwenye sura ya saba, mfululizo wa falme hizo za dunia watambulishwa. Unabii wa sura ya saba hurudia na kuupanua ujumbe wa hapo awali, na kuzikuza zaidi awamu hizo mbili za Roma kwa kuitanguliza "pembe" iliyochukuwa nafasi ya zile "pembe tatu" ambazo "ziling'olewa". Kisha katika Danieli nane, unabii wa tatu huielezea historia hiyo hiyo, huku tena ikiirudia na kuipanua, (japo haijumuishi Babeli kwenye orodha, kwani ilikuwa imepita muda wa utawala na mamlaka yake, ikawa ikisubiri kuondoshwa tu).

Katika njozi ya Danieli kumi na moja, Babeli kama ilivyo katika sura ya nane, haitajwi, kwani wakati wa njozi hiyo, ilikuwa tayari imekwisha ondoka kwenye onyesho la historia. Unabii huo huanza na Wamedi na Waajemi, wakifuatwa na Uyunani. Je, wapo wengine wawezao kusema eti ufalme unaofuata hauashiriwi na Roma katika awamu zake mbili? Nabii zote tatu zilizopita za Danieli zaitia Roma katika mwisho wa ulimwengu ambapo itaipokea adhabu yake. Mbili kati ya hizo zaitaja hukumu yake kuwa ni isiyo ya kawaida – "pasipo mikono" na "kuvunjwa pasipo mikono." Vivyo hivyo, utawala wa mwisho wa dunia katika Danieli kumi na moja "atafikia mwisho wake, na hakuna atakaye msaidia."

Tungekuwa watu wasio na msimamo iwapo tutazisoma jumbe hizi nne kisha tukose kuziona zikikamilishana, zikijengana, na kusikilizana zenyewe kwa zenyewe.

Babeli ndicho kichwa cha dhahabu – yaani simba.

Umedi-Uajemi ni mabega ya fedha, yaani dubu, na pia kondoo dume.

Ugiriki ni mapaja ya shaba, pia ni chui, yule beberu, na yule mfalme hodari.

Roma ni miguu ya chuma, yule mnyama mwenye pembe kumi, na ule upembe mdogo. Na katika kupatana na nabii za hapo awali, Roma vilevile ndiye "mfalme wa kaskazini" wa Danieli 11:40-45.

Tukitumia kanuni ya rudia na upanue, twaiona Roma ya kipapa ikiwa ndiyo mada ya unabii wa mwisho wa Daneli. Ipo njia nyingine ya kumtambulisha mfalme huyo wa kaskazini kama Upapa. Dada White atuelekeza kwenye Upapa kufungamana na "sura ya mwisho ionekanayo waziwazi katika historia ya dunia hii."

> "Yale matukio yanayohusiana na utenda kazi wa yule mtu wa kuasi ndiyo sura za mwisho zinazoonekana wazi katika historia ya dunia hii." *Selected Messages*, book 2, 102.

Mfululizo wa matukio katika Danieli 11:40-45 waanza mnamo 1798. Lakini mfululizo wa matukio yanayotajwa na aya hizi hauishi na aya ya arobaini na tano. Matukio yanayoelezewa huendelea hadi Danieli 12:4, ambapo Danieli anaambiwa "ayafungie maneno hayo, na kukitia muhuri kitabu hicho."

Danieli 12:1 yaendeleza aya za hapo awali, kwani kirai chake cha kufungua chahitaji kujumuishwa na mfululizo wa hapo awali: "Ndipo **wakati huo** Mikaeli atasimama." Wakati gani? Wakati uliomalizia kuelezewa katika aya zilizotangulia. "Katika wakati huo," waelekeza nyuma kwenye matukio ya hapo awali. "Wakati huo" wawadia katika aya zinazotangulia, nao ndio mwisho wa rehema kwa wanadamu.

> "'**Wakati huo** Mikaeli, mtawala mkuu ambaye huwalinda watu wako, atasimama. Kutakuwako wakati wa taabu ambao haujatokea tangu mwanzo wa mataifa hadi wakati huo. Lakini wakati huo, watu wako, kila mmoja ambaye jina lake litakutwa limeandikwa kwenye kitabu, ataokolewa.' Danieli 12:1. Pale wakati huu wa taabu ukija, kila kesi itakuwa tayari imeamriwa; hakuna muda wa neema tena, hakuna tena huruma kwa wasiotubu. Muhuri wa Mungu aliye hai uko juu ya watu wake." *Testimonies*, volume 5, 212–213.

"Mfalme wa kaskazini" "atafikia mwisho wake" mwishoni mwa muda wa rehema, kwani "wakati huo" Mikaeli atasimama, na kuacha upatanishi wake Pahali Patakatifu Mno.

"Mfalme wa kaskazini" ndiye "mtu wa kuasi", yaani papa wa Roma, kiongozi wa ufalme wa mwisho wa kidunia ambao umeelezewa ndani ya nabii zote za Danieli. Upapa ndio utawala unaoidhibiti Babeli ya kiroho, ambayo Ufaransa, ikiwakilishwa na "mfalme wa kusini", iliisukuma mnamo 1798. Vita vilivyozuka mwakani 1798 kati ya wafalme hawa viliendelea hadi kuanguka kwa Muungano wa Sovieti hivi majuzi. Sehemu iliyosalia katika aya ya arobaini yazungumzia vita hivi, nacho kitakuwa ndicho kiini cha somo letu katika sura ifuatayo. Hata hivyo, kabla ya kuianza sehemu hiyo ya somo hilo, tutarejelea swala tulilolianza katika somo lililopita.

Katika sura iliyopita kiini chetu kilikuwa ni fungu moja ambapo Dada White alifundisha kuwa maonyesho na historia ambayo ni sawa na ile historia iliyotukia katika njozi ya Danieli kumi na moja, hasa aya za 30-36, "yangerudiwa". Pia tuliiona historia ya kuinuka kwa Roma ya ukafiri na ya kipapa katika utawala. Wote wawili iliwapasa kuzishinda falme tatu kwanza ili kuweza kuutawala ulimwengu. Ile pembe ndogo ya Roma ya kikafiri ililazimika kushinda kusini, mashariki, na ile nchi ipendezayo. Soma Danieli 8:9. Roma ya kipapa ililazimika kuzing'oa zile pembe tatu – Vandals, Goths na Heruli. Kabla ya lile jeraha linalouzuia Upapa kutawala kama serikali juu ya ulimwengu kupona, sharti pia uvitiishe vitu vitatu. Vitu hivi vitatu ni kuta tatu.

Tunaposonga katika somo letu tutaona kuwa wakati Muungano wa Sovieti uliporomoka ili kuutimiza unabii wa Danieli 11:40, ule ukuta unaoashiriwa na **Pazia la Chuma** uliondolewa. Hatua kubwa katika kuporomoka kwake ilikuwa ni kule kuharibiwa kwa Ukuta wa Berlin. Katika Danieli 11:41, eneo linalofuata la kushindwa latambulishwa kama "nchi ya uzuri". Hiyo "nchi ya uzuri" ni Marekani ambayo huuinamia utawala wa Roma pale wabunge wake wanapoitengeneza sanamu ya mnyama, kwa kuipitisha sheria ya kitaifa ya Jumapili. Wakati jambo hili litafanyika, kama ishara, **ule ukuta unaotenganisha kanisa na serikali** utakuwa umekwisha ondolewa.

Ufunuo 13:11-12, yafundisha kuwa mara tu baada ya Marekani kuongea kama joka (jambo ambalo Roho wa Unabii hutambulisha kama kupitisha kwa sheria ya kitaifa Jumapili), ndipo Marekani itaulazimisha ulimwengu mzima kufanya hivyo

pia. Ulimwengu utafuata Marekani katika kuisimamisha sanamu ya mnyama. Ufafanuzi wa sanamu ya mnyama wahusisha hali ya kulazimishwa kwa sheria za kidini na serikali. Ili ulimwengu uweze kuitengeneza sanamu ya mnyama, sharti wawe na serikali moja ulimwenguni ambayo yaweza kuunda na kulazimisha sheria. Bila ya uwezo huu, ufafanuzi wa sanamu ya mnyama hauwezi kutimizwa.

Baada ya "mfalme wa kaskazini" kuingia kwenye "nchi ya uzuri" katika aya ya arobaini na moja, anaanza kuitawala "Misri", ambayo yawakilisha ulimwengu mzima. Kabla ya ulimwengu wote kutawaliwa na serikali ya ulimwengu mzima, ambayo itazilazimisha sheria za kidini, serikali za ulimwengu zitalazimika kuzisalimisha haki zao kama mataifa binafsi. Mambo haya yatakapofanyika, basi kama ishara, ule **ukuta wa madaraka ya kitaifa** utakuwa umekwisha ondolewa. Sheria aina hii tayari zinaendelezwa ndani ya Umoja wa Mataifa.

Kama vile Roma ya kikafiri ilizishinda falme tatu pale ilipouteka nyara ulimwengu, vivyo hivyo Roma ya kipapa ilizishinda falme tatu. Roma ya kikafiri ilitumia jeshi lake kutimiza jambo hilo, huku nayo Roma ya kipapa ikilitegemea jeshi la utawala mwingine lifanye kazi ya kuipandisha kwenye kiti cha enzi cha dunia. Mapambano ya kijeshi ya wote wawili, yaani Roma ya kikafiri na ya kipapa, ya kupanda juu ya kiti cha enzi cha dunia, yalihusisha vita halisi vikipiganwa na majeshi halisi.

"Mfalme wa kaskazini" pia atazishinda tawala tatu anapokirudia cheo cha mamlaka alichokipoteza mnamo 1798. Vikwazo vitatu ambavyo Upapa wa kisasa utaviondoa vitatekelezwa kwenye uwanja wa vita vya kiroho, kinyume na vita halisi. Pambano hilo litazuka kwenye uwanja wa itikadi na mafundisho ya dini. Ukuta wa kwanza katika pambano hili sasa ni historia iliyopita, kwani pambano la itikadi baina ya ukanaji Mungu na Ukatoliki, ambalo lilianza na yale Mapinduzi ya Ufaransa, tayari limekamilika.

Kuta mbili zifuatazo za ushindi vilevile ni mapambano ya kiroho yanayohusika na mafundisho ya ukweli na ya uwongo. Kama vile Upapa kwa ishara wanyosha mkono wake hadi kwenye "nchi ya uzuri" na kisha hadi "Misri", kwanza Marekani, kisha ulimwengu, watakuwa mawindo katika vita hivi vya mwisho vya kung'ang'ania kiti cha enzi cha ulimwengu. Wakati kuta hizi za mwisho zitakapoondolewa, kupona kwa lile jeraha kutakamilika, jinsi aya ya arobaini na tatu inavyomwelezea "mfalme wa kaskazini" akilileta jengo la uchumi wa ulimwengu chini ya utawala wake. Jambo hili lawakilisha kurudi kwake kabisa kwenye cheo alichokipoteza mnamo 1798 – yaani cheo chake kama ufalme unaotawala vyote kisiasa.

Tunapozidi kusoma kuhusu matukio haya ya mwisho, twafaa kukumbuka ya kuwa kuta hizi zote tatu za kiishara zijapo anguka, kunao "ukuta" mwingine wa kiishara ambapo twaweza kupata usalama na kimbilio:

> "Niliona kuwa kama Mungu angekuwa ameibadilisha Sabato kutoka siku ya saba hadi siku ya kwanza, basi angeyabadilisha maandiko ya amri hiyo ya Sabato, iliyoandikwa juu ya vipengele vya mawe, ambavyo sasa viko ndani ya sanduku lililoko Mahali Patakatifu Mno pa hekalu ya mbinguni; nayo ingesomeka hivi: Siku ya kwanza ndiyo Sabato ya Bwana Mungu wako. Lakini niliona ya kuwa inasomeka sawa na jinsi ilivyoandikwa juu ya vipengele vya mawe kwa kutumia kidole cha Mungu, na kuletwa kwa Musa huko Sinai. 'Bali siku ya saba ni Sabato ya BWANA Mungu wako.' Kutoka 20:10. Niliona kuwa **Sabato takatifu ni, na itakuwa, ukuta wa kuwatenganisha Israeli wa kweli wa Mungu na wale wasioamini**; na ya kuwa Sabato ndilo swala kuu la kuiunganisha mioyo ya watakatifu wapendwa wa Mungu wanaomsubiri." *Early Writings*, 33.

"Uadilifu kamili wafaa kuhifadhiwa na kila mwanafunzi. Kila wazo lafaa kuligeukia neno la Mungu lililofunuliwa, kwa usikivu wa unyenyekevu. Nuru na neema watapewa wale wanaomtii Mungu jinsi hiyo. Watayaona maajabu kutoka kwenye sheria yake. Mambo makuu ya kweli ambayo yamekaa bila kusikizwa wala kuonekana tangu siku ya Pentekoste, yatang'aa kutoka kwenye neno la Mungu yakiwa na ule usafi wake wa asili. Kwa wale wampendao Mungu kwa kweli, Roho mtakatifu atawafunulia ukweli uliochujuka kutoka akilini, na pia ataufunua ukweli ambao ni mpya kabisa. Wale walao nyama na kuinywa damu ya Mwana wa Mungu watatoa kutoka kwenye vitabu vya Danieli na Ufunuo ukweli uletwao na Roho Mtakatifu. Wataanzisha vitendo vya nguvu ambavyo haviwezi kuzimwa. Vinywa vya watoto vitafunguliwa ili kuzitangaza siri zilizokuwa zimefichwa kutoka akilini mwa wanadamu. Bwana amevichagua vyombo vipumbavu vya ulimwengu huu ili ziwafadhaishe wenye hekima, na vyombo vidhaifu vya ulimwengu ili viwafadhaishe watu hodari." *The Fundamentals of Christian Education*, 474.

Wakati wa Mwisho

Na wakati wa mwisho mfalme wa kusini atashindana naye; na mfalme wa kaskazini atamshambulia kama upepo wa kisulisuli, pamoja na magari ya vita, na wapanda farasi, na merikebu nyingi; naye ataingia katika nchi hizo, na kufurika na kupita katikati. Danieli 11:40.

Hapo awali, tuliutambua wakati wa mwisho kama 1798. Tuliona kuwa kote katika Danieli kumi na moja, utawala ulioidhibiti Misri ulikuwa ni "mfalme wa kusini", nao utawala ulioitawala Babeli ulikuwa ni "mfalme wa kaskazini".

Mnamo 1798, utawala uliokuwa ukiidhibiti Misri ya kiroho – kulingana na Ufunuo 11:7-11 na *The Great Controversy*, 269-270, ulikuwa ni Ufaransa. Na wakati huo huo katika historia, utawala ulioidhibiti Babeli ya kiroho ulikuwa ni Upapa, kulingana na Ufunuo 17:1-6 na *The Great Controversy*, 382.

Tulipata kuwa neno "shindana" katika sehemu ya kwanza ya Danieli 11:40 humaanisha kufanya "vita dhidi ya." Wakati Napoleon alipomshika mateka papa wa Roma mnamo 1798, kipande cha kwanza cha aya ya arobaini kilitimia: "Na wakati wa mwisho mfalme wa kusini atashindana naye." Sasa tutaichukuwa sehemu iliyosalia ya aya hii.

Sehemu inayofuata ya aya hii yatabiri kuwa "mfalme wa kaskazini" "atakuja dhidi ya" yule "mfalme wa kusini" "kama kisulisuli," kudokeza shambulio la kulipiza kisasi wakati fulani siku za usoni. Hata hivyo, siyo tu kulipiza kisasi, bali mageuzi makuu ya vita hivi yanawakilishwa, kwani katika maneno ya mwisho ya aya hiyo "mfalme wa kaskazini" "atafurika na kupita juu."

Tutaona hapo chini ya kuwa neno "kisulisuli" humaanisha kuondoa kwa njia ya kutisha kama dhoruba. Neno hili limewekwa pamoja na neno "shambulia," kuonyesha sio tu kufagiliwa kwa nguvu nyingi, bali pia **kuinuka**.

Kipande cha mwisho cha aya hiyo chawakilisha kuwa "mfalme wa kaskazini" atampitiliza na kumwondoa mfalme wa kusini, kwani "kufurika" ni kushinda, kutimua, au kuosha, na "kupita katikati" ni kuvuka au kupitiliza.

Hebu na tuzichunguze fasili kwenye kamusi ya Kihebrania ya Strong kuhusu maneno kadhaa muhimu katika Danieli 11:40:

> "kisulisuli – 8175: mzizi wa kimsingi; kufanya ***dhoruba***; kwa kudokeza *kutetemeka*, i.e. *hofu*:– kuogopa sana, hofu, tupa dhoruba, kuwa na tufani, **kuja kama (kuondoa kama vile kwa) kimbunga.**
>
> "dhidi ya – 5921: sawa na 5920 hutumika kama kihusishi (katika hali ya umoja au wingi, mara nyingi pamoja na kiambishi au kama kiunganishi pamoja na kishirikishi kufuatia) juu, juu ya, kupinga …
>
> "5920: kutoka 5927 ….
>
> "5927: mzizi wa kimsingi: kupaa, kitensi kisichoelekezi (kuwa juu) au (kupanda); hutumika kwa njia nyingi mbalimbali, la msingi na la ya pili, kihalisi na kitamathali ….
>
> "kufurika – 7857: mzizi wa kimsingi; *kufoka*; kwa kudokeza kugharikisha, kusafisha, kwa analojia *kuenda shoti*, kushinda …
>
> "pita – 5674: mzizi wa kimsingi; *kuvuka*; hutumika kwa upana kuhusu *mpito* wowote (kawaida au kitamathali; elekezi, kisichoelekezi, shadidi, au cha kufanyiza); hasa *kufunika* …." *Strong's Exhaustive Concordance.* [Mkazo wote kuongezwa.]

Aya ya arobaini yafundisha kuwa wakati fulani baada ya 1798 yule mfalme wa kaskazini angemfagilia mbali mfalme wa kusini kwa namna ya nguvu, huku pia akiinuka kwa njia fulani.

Katika sura iliyopita tumependekeza kuwa Danieli 11:40-45 ni unabii uliokusudiwa na Mungu kutumika kama kichocheo cha kuwaamsha watu Wake mwishoni mwa ulimwengu. Tulipendekeza kuwa kama jambo sawia na harakati ya Miller twafaa kutarajia kuona yakirudiwa baadhi ya matukio yaliyotukia chini ya harakati ya wale waanzilishi. Tuliutazama hasa ule unabii wa Josiah Litch kuhusu kuanguka kwa Milki ya Uturuki kama mfano wa jinsi utimilifu wa unabii unavyowaathiri watu wa Mungu na walimwengu.

Kuambatana na tukio hilo la kihistoria na utabiri ya kuwa baadhi ya uzoefu wa waanzilishi utarudiwa, tulipendekeza kuwa kule kuporomoka hivi majuzi kwa Muungano wa Sovieti kwalingana na kule kuanguka kwa Milki ya Uturuki, ijapo kuwa unabii huu ulikosa kuutaja muda kamili wa kiunabii. Pendekezo hili laibua swali moja, Ni jinsi gani huyo "mfalme wa kusini" alianza kama Ufaransa na kisha akawa Muungano wa Sovieti?

Kote kwenye mtiririko wa historia, kama inavyodhihirika katika Danieli kumi na moja, wafalme wa kaskazini na kusini waliinuka na kuanguka huku tawala mpya zikitokezea na kuzipindua falme zilizotangulia. Baada ya 1798, taji ya kusini pia ilibadili mikono.

Ufaransa ilivaa taji ya mfalme wa kusini mnamo 1798. Hata hivyo baada ya yale Mapinduzi ya Ufaransa, falsafa ya ukanaji Mungu ilizidi kukua, huku serikali ya Ufaransa ikiacha kumkana Mungu kama kanuni ya kimsingi ya serikali yake.

Ukianzia kwenye kitalu cha Ufaransa, kumkana Mungu mwishowe ulienea kote Ulaya na ulimwenguni. Japo ulizidi kukua katika ushawishi wa kiakili, kumkana Mungu kuliacha kuwa na sauti, kwani kuwa na sauti kiunabii huhitaji kuwa na serikali fulani.

> "'Unenaji' wa taifa ni tendo la mamlaka zake za bunge na mahakama." *The Great Controversy,* 442.

Baada ya muda fulani, taifa lingine laitwaa ile taji ya "mfalme wa kusini" kwa kuinua na kuushirikisha ukanaji Mungu katika serikali yao.

Ni jambo la kuvutia kuona ya kuwa sifa moja ya kumkana Mungu katika historia ya mataifa ni kwamba kila wakati huandamana na mapinduzi. Tukianzia na yale Mapinduzi ya Ufaransa, ukanaji Mungu uliileta kasri ya "mfalme wa kusini" huko Ufaransa; hata hivyo, kufikia 1917, ukanaji Mungu uliihamisha kasri ya mfalme wa kusini hadi Urusi wakati wa Mapinduzi ya Bolsheviki. Baada ya Vita vya Pili vya Ulimwengu Urusi ilipanuka na kuwa Muungano wa Sovieti. Dada White adokeza kuwa kanuni hizi za ukanaji Mungu zingeendelea na kufikia kiwango cha juu cha umuhimu kuliko Mapinduzi ya Ufaransa tu:

> "Kuwekwa kwa mali na utawala sehemu moja; ushirikiano mwingi wa kuwatajirisha wachache kwa kuwadharau walio wengi, ushirikiano mwingi wa tabaka za maskini ili wazitetee haki zao; roho wa vurugu, misukosuko na umwagaji wa damu; kuenezwa ulimwenguni kote kwa mafundisho yale yale yaliyopelekea Mapinduzi ya Ufaransa – yote haya yanauhusisha ulimwengu mzima kwenye harakati sawa na zile zilizoisukasuka Ufaransa." *Education*, 228.

Kuinakili historia ya ushindi wa Muungano wa Sovieti kwa miaka iliyofuata ni jambo la kuelimisha kwa njia nyingi. Kwanza kabisa ni ukweli kwamba huku nchi baada ya nchi ilipokuja chini ya utawala wa ufalme huu, namna ya kimsingi ya kutekeleza tendo gumu kama hilo ilikuwa ni mapinduzi. Kusudi la Ukomunisti (Ujamaa) lilikuwa ni kupenya, kutia kasumba ya fikra maalum, na kuyaleta mapinduzi.

Jambo jingine la kukua huku ni kwamba karibu nchi zote ambazo mwishowe zililetwa chini ya mwavuli wa Muungano wa Sovieti zilikuwa hapo awali ni mataifa yaliyotawaliwa na Ukatoliki. Moja kwa moja, Ukatoliki ulikuwa ukiupoteza msingi wake wa uwezo.

Huku mapinduzi ya kikomunisti yakienea kote ulimwenguni, Upapa nao ulipata chombo cha kuutambulisha Muungano wa Sovieti kama adui wake mmoja na Marekani. Hila hii ya *adui mmoja* ilitayarisha njia ya ushirikiano unaoelezewa katika aya ya arobaini, ambao pia ndio ushirikiano unaozungumziwa kwa upana katika Ufunuo kumi na tatu.

Aya ya arobaini yafundisha kuwa "mfalme wa kaskazini" hatimaye angemfagilia mbali "mfalme wa kusini" – kwa magari ya vita, wapanda farasi, na merikebu. Kuzitambulisha ishara hizi za kiunabii kunalenga wajibu wa Marekani katika vita hivi.

Twafahamu kuwa "magari ya vita" na "wapanda farasi" huashiria nguvu za kijeshi katika unabii wa Biblia:

> Ndipo Adonia mwana wa Hagithi akatabakari, akasema, Mimi nitakuwa mfalme. Akajiwekea tayari **magari na wapanda farasi**, na watu hamsini wapige mbio mbele yake 1 Wafalme 1:5. Basi, Ben-hadadi mfalme wa Shamu akakusanya **jeshi lake lote**; nao walikuwapo wafalme thelatini na wawili pamoja naye, na **farasi**, na **magari**: akakwea akauhusuru Samaria, akaupiga vita 1 Wafalme 20:1.
>
> "Meli" huashiria nguvu za kiuchumi katika unabii wa Biblia:
>
> Washukao baharini katika **merikebu**, Wafanyao **biashara** zao katika maji mengi Zaburi 107:23. Kwa kuwa katika saa moja **utajiri mwingi** namna hii umekuwa ukiwa. Na kila nahodha na kila aendaye mahali popote kwa matanga, na mabaharia, **nao wote watendao kazi baharini**, wakasimama mbali; wakalia sana, walipouona moshi wa kuungua kwake, wakisema, Ni mji upi ulio mfano wa mji huu mkubwa! Wakatupa mavumbi juu ya vichwa vyao, wakalia, wakitokwa na machozi na kuomboleza, wakisema, Ole, ole, mji ule ulio mkuu! Ambao ndani yake **wote wenye merikebu baharini walipata mali kwa utajiri wake**; kwa kuwa katika saa moja umekuwa ukiwa. Ufunuo 18:17-19.

Katika Danieli 11:30, watawala wa Milki ya Roma walikuwa wamehuzunika kwa kuwa walikosa uwezo wa kukuwa na ufalme wao kama walivyofanya hapo awali. Baada ya muda, Ufaransa ilikuwa taifa la kwanza la kikatoliki pale mfalme wake, Clovis, alilitoa wakfu taifa lake kwa upapa na kuanza kuzing'oa zile pembe tatu. Kumbukumbu ya historia ya hivi majuzi inayoelezea kuanguka kwa Muungano wa Sovieti yasisitiza historia ya Clovis kwani inalitambulisha shinikizo la kijeshi na la kiuchumi lililowekwa na Marekani, pale ilipousaidia Upapa kumfagilia mbali mfalme wa kusini, huku ikiuanzisha wajibu wa kiunabii uliotajwa kuhusu Marekani na Ufunuo kumi na tatu. Ule uliokuwa ni ukweli kwa Uadventista kwa miaka 150 ukawa ni "ukweli wa sasa."

Danieli 11:40 yasema kuwa wakati "mfalme wa kaskazini" atakapoufagilia mbali ufalme wa kusini, "ataingia katika nchi hizo." Fungu hili laonyesha kuwa ufalme wa kusini ungekuwa ni shirikisho la **mataifa**. Bila shaka huo ulikuwa ndio ukweli kuhusu ule uliokuwa Muungano wa Sovieti na nchi zake nyingi za pambizoni.

UNABII KUTIMIA

Dada White ameitoa taarifa itakayoturuhusu kuujaribu mpangilio wa matukio tuliyoyapendekeza tukilinganisha na ushuhuda wa kumbukumbu ya historia.

> "**Matukio ya kihistoria, yanayoonyesha utimilifu wa unabii moja kwa moja**, yaliletwa mbele ya watu, nao unabii huo ukaonekana kuwa ni kuwekwa kwa mstari matukio yanayotuongoza hadi mwisho wa historia ya dunia hii kiishara. Matukio yanayohusika na utenda kazi wa yule mtu wa kuasi ndiyo maonyesho yaliyofunuliwa wazi katika historia ya dunia hii. *Selected Messages*, book 2, 102.

Huku "matukio ya kihistoria" yanayohusishwa na kuporomoka kwa Muungano wa Sovieti yalipokuwa yakiendelea kunakiliwa na vyombo vya habari vya kiulimwengu, twayapata maelezo ya historia ya vita vinavyoendelea baina ya ukanaji Mungu na Ukatoliki. Ushirikiano kati ya Marekani na Upapa wazungumziwa, ukiwemo wajibu wa Marekani kijeshi na kiuchumi. La ajabu ni kuwa twawapata waandishi wa makala haya ya kiulimwengu mara kwa mara walielekezwa kuyachagua maneno katika kuzisimulia hadithi zao ambayo ni maneno yale yale yanayopatikana katika maelezo ya Biblia aya ya arobaini. Mungu anakusudia watu wake waone kuwa "matukio haya ya historia" ni "utimilifu wa moja kwa moja wa unabii." Mungu atuhitaji tuutambue mfululizo huu wa matukio kama mwito wa kuiamsha Laodikia.

THIBITISHO KWENYE MAGAZETI YA KILIMWENGU

"Gorby Ainamia Vikosi vya Askari wa Kirumi"—Kichwa katika gazeti la *U.S. News & World Report*.

"Wakati yule Mfalme wa Roma Takatifu Henry IV alipoamua **kuomba** msamaha kwa Papa Gregory VII mnamo 1077, alisimama pekupeku kwa siku tatu kwenye theluji nje ya makao ya papa ya Canossa, Italia. Mkataba wa Gorbachev na kanisa haukuwa na upungufu wa umuhimu kwa njia yake." *Time*, December 11, 1989.

"Kikao cha rais wa Sovieti pamoja na Papa Yohana II mnamo Ijumaa ndio usitawi wa hivi karibuni wa mapinduzi katika ulimwengu wa Kikomunisti ambayo papa alisaidia kumemetusha naye Gorbachev akaruhusu kutendeka." *U.S.A. Today*, hadithi ya kichwa, 1989.

"Hadi kufikia hivi majuzi, vikosi vya Marxism vilionekana kuwashinda askari wa Msalaba. Wakati wa Mapinduzi ya Bolsheviki ya 1917, Lenin alikuwa ameahidi stahimili lakini akaleta hofu. 'Urusi iligeuka kuwa nyekundu kwa damu ya wafia dini,' asema Father Gleb Yakunin, mpiganiaji hodari zaidi wa uhuru wa dini ndani ya Russian Orthodox. Katika miaka ya kwanza mitano ya utawala wa Bolshevik, maaskofu 28 na makasisi 1,200 walichinjwa kwa mundu nyekundu. Starlin aliuzidisha pakubwa ukatili huo, na kufikia mwisho wa utawala wa Krushchev, uangamizaj wa wahudumu wa kanisa ulifikia takriban 50,000. Baada ya Vita vya Pili vya Dunia, mateso mengine makali japo yenye umwagaji wa damu uliopungua yalienea hadi Ukraine na jumuia mpya ya Sovieti, ambapo waliathirika mamilioni ya Wakatoliki wa Roma na Waprotestanti pamoja na Orthodoxi. *Time*, December 4, 1989.

"Katika vikao vya siri na viongozi wa serikali, mashauriano ya faragha pamoja na makundi ya waasi na kueneza propaganda ya harakati zake dhidi ya udhalimu, yeye [Yohana Paulo II] amesaidia kuyaleta mabadiliko makuu zaidi ya sera tangu Mapiduzi ya Urusi." *Life*, December 1989.

"Ziara yake [Papa Yohana Paulo II] ya ushindi huko Poland mwaka wa 1979, asema askofu wa Poland, ilibadili 'fikra za hofu, hofu ya polisi na vifaru, ya kupoteza ajira, ya kukosa kupandishwa cheo, ya kufukuzwa shule, ya kukosa kupata pasipoti. Watu walijifunza kuwa iwapo wataacha kuiogopa serikali, basi serikali itakuwa bila uwezo.' Hapo ndipo Solidarity ilizaliwa, huku ikiungwa mkono na kanisa na kuongozwa na marafiki wa papa kama vile Lech Walesa na Tadeusz Mazowieke, ambaye hatimaye alikuwa Waziri Mkuu wa kwanza Mkristo katika jumuia ya Sovieti." *Time*, December 4, 1989.

"Mnamo 1935 Josef Starlin, mtawala wa kidikteta wa Muungano wa Sovieti, alipewa mawaidha asiyoyaomba. Fanya ishara ya kuridhisha kwa Vatikani, akaambiwa. Kama wange**sukumwa** mbali sana, Wakatoliki wa nchi yake wangekuwa wenye kuyapinga mapinduzi. Masharubu makubwa ya Starlin yalizidisha dhihaka yake. 'Papa. Anavyo vikosi vingapi?' Jibu kwa wakati huo lilikuwa ni kwamba hana. Jibu leo ni kwamba *hahitaji* chochote. Majengo ya Ukomunisti yanaporomoka kwa kuguswa tu." *Life*, December 1989.

"Mkurupuko wa uhuru huko Ulaya Mashariki ni ushindi mtamu kwa Yohana Paulo II." *Life*, December 1989.

Neno "kurupuka" ni kitenzi kinachotumika kuelezea kuenea kwa uhuru huu. Yeye "atafurika [kurupuka] na kupita katikati." Neno hili "sukumwa" lilichaguliwa na mwandishi huyu kuelezea ile vita ambayo Ukomunisti ulikuwa ukizua dhidi ya Ukatoliki.

"Kati ya matukio yote yaliyoitikisa jumuiya ya Sovieti mnamo 1989, hakuna lililojaa vitisho vya historia – au la shaka – kama kabiliano taratibu linalokusudiwa kufanyika wiki hii Mjini Vatikana. Huko, ndani ya maabara pana ya kisherehe kwenye Kasri ya Mitume ya karne ya 16, yule Zari wa ulimwengu wa ukanaji Mungu, yaani Mikhail Gorbachev, atamtembelea Wakili wa Kristo, Papa Yohana Paulo II.

"Utakuwa ni wakati wa kuchangamsha, sio tu kwa sababu Yohana Paulo alisaidia kuwasha moto wa ari ya uhuru nyumbani kwao Poland, ambao **ulifagia kama moto wa kichaka** kote Ulaya ya Mashariki. Zaidi ya hayo, mkutano wa watu hao wawili unaashiria mwisho wa vita vya kiroho vya kuvutia zaidi karne ya 20, pambano ambalo ndani yake nguvu za Ukomunisti zilizoonekana kama zisizozuilika, zilipondaponda Ukristo usiotikisika." *Time* December 4, 1989.

"Ijapokuwa ile sera ya Gorbachev ya kuacha ilikuwa ndicho chanzo mara moja cha mlipizano wa madaraka ambayo yamefagia kote Ulaya ya Mashariki miezi michache iliyopita, Yohana Paulo astahili kutambuliwa zaidi japo kwa mbali." *Time*, December 4, 1989.

Hapa neno hili "kufagia" limetumika, na kufagilia mbali ina maana ya "kushambulia kama kisulisuli." Tukio hili laelezewa kuwa vita vya kiroho vyenye kuvutia sana katika karne ya ishirini, huku Gorbachev akitambuliwa kama Zari wa ukanaji Mungu ulimwenguni, kisawe cha kuwa Zari wa ulimwengu wa Ukomunisti. Waandishi wa kilimwengu huutambulisha Ukomunisti kama – ukanaji Mungu.

"Ushindi wa Yohana Paulo II – **wimbi** la uhuru **inayoiosha Ulaya ya Mashariki** yajibu ombi lake la ari." *Life*, December, 1989.

Neno "kufurika" humaanisha "kuosha," kama kwa maji. Ni nani aliyekuwa akiwachagulia maneno wanahabari hawa wa kilimwengu?

"**Siku za Kisulisuli**" ni Kichwa katika Newsweek, December 25, 1989, cha makala ambayo ni kronolojia ya kuporomoka kwa Ukomunisti. Mwandishi alifikiria kuwa kichwa mwafaka cha makala hayo lingekuwa ni neno sawa na lile alilolitumia Danieli mara mbili – kulielezea tukio hilo hilo kinabii.

MAGARI YA VITA NA WAPANDA FARASI

"Mnamo 1981, jumuiya ya ukomunisti ilipata mshtuko mwingine. Rais mpya wa Marekani, Ronald Reagan, alianza kuitimiza ahadi yake ya kubishana na Wasovieti, wala sio kuwatuliza. Miaka michache iliyofuata, alizidisha ongezeko la nguvu za **kijeshi** na kutangaza Mkakati wa Uwezo wa Kijeshi (SDI), mfumo wa angani wa kujihami dhidi ya shambulizi la makombora. Aliwaunga mkono waasi waliopinga Ukomunisti huko Nicaragua, Angola, Cambodia, na Afghanistan. Na akitumia majeshi ya Marekani, alikiweka huru kisiwa cha Grenada kutokana na wahuni wa Kikomunisti.

"Imani ya Wasovieti ilitikisika ….

"Ulaya ya Magharibi pia iliwashinikiza Wasovieti. NATO iliendelea kuimarisha uanajeshi wa kisasa. Wapigaji kura wa Kijerumani walizisukumia mbali "lele za amani" za Usovieti na kuichagua serikali iliyochagua kuyatuma makombora mapya ya masafa ya wastani….

"Shinikizo la kijeshi kutoka Marekani na washirika wake wa Magharibi lilikuwa limesababisha mshtuko kwa Wasovieti." *Reader's Digest*, Marchi 1990.

PAMOJA NA MERIKEBU NYINGI

"Gorbachev pia amefahamu kwamba kupona kisiasa na kiuchumi kwaitegemea heri njema ya watu Wasovieti, ambao idadi ya Wakristo walioko miongoni mwao kila mara imezidi ile ya Wakomunisti. Zaidi ya hayo, Gorbachev ahitaji ushirikiano wa Magharibi, asema Father Mark, kasisi mmoja wa Orthodox mwenye fikra za marekebisho huko Moscow, ambaye huuona mkakati wa Gorbachev ndani ya U.S.S.R. kama 'matokeo ya hitaji la sera ya kigeni,'" *Time*, December 4, 1989.

"Katika miaka ya 1980, uchumi wa kikomunisti, ambao daima huwa ni finyu, ulianguka tumbo juu. Kabla ya hayo, ulikuwa umekosa bidhaa za walaji na za starehe. Sasa upungufu wa kudumu wa bidhaa kuu ulizidi pia. Wakati wachimba migodi wa Kisovieti walipofanya mgomo mnamo 1989, baadhi ya madai yao yalikuwa ni sabuni, karatasi za chooni na sukari." *Reader's Digest*, Machi 1990.

"Kulingana na Gorbachev, ule uchachuchachu ulioko katika eneo la Baltics unatikisa sio tu pembe ndogo ya milki iliyojengwa na Lenin na Starlin, bali misingi ya milki yenyewe. Swala la uraia ni utoneshaji wenye nguvu wa ishara zingine nyingi, kutoka uchumi unaoporomoka hadi mapambano ya kimbari, hivyo uangukaji huo wa kustaajabisha wa milki ya Kisovieti katika Ulaya ya Mashariki huenda usisimamie mpakani mwa Usovieti. Huku uchumi unapozidi kuzorota na upungufu kuongezeka, hali ya raia kuishiwa na imani juu ya Ukomunisti na Gorbachev mwenyewe inaongezeka, nazo jamhuri zenye uhasama, na mataifa na makundi ya kisiasa wanaushindania kwa ukali zaidi uwezo wa kisiasa na mgawo wa uchumi huo unaofifia. Ufisadi na uhalifu umeenea; walio wachache na wafanyi kazi wa reli wanatishia kukatiza ugavi wa mafuta majira haya ya baridi kali. Wakazi wa Azerbaijani wakata reli inayoelekea Armenia ambayo ni nchi iliyo ndani yake; wakulima waweka akiba ya chakula, na kuziacha rafu za miji zikiwa tupu." *U.S. News and World Report*, January 15, 1990.

KISULISULI CHAANZA

"Nchini Poland uhuru wa kutembeatembea ulizaliwa karibu miongo mitatu iliyopita pale askofu wa Krakow alipoomba idhini ya kujenga kanisa mpya. Wakati mamlaka ya Ukomunisti ilipolikataa ombi hilo lake, askofu huyo alisimamisha msalaba mkubwa na kuisherehekea misa nje hadharani. Wakomunisti waliuangusha chini. Washirika wa kanisa wakaurejesha tena na tena hadi mwishowe Wakomunisti wakasalimu amri." *Jubilee*, April 1990.

Askofu huyo wa Krakow alikuwa ndiye nani hasa? Sio mwingine ila Papa Yohana Paulo II.

"Huku ikiungwa mkono na Papa, Solidality (Muungano wa Wafanyakazi wa Poland) ulibuniwa, naye Yohana Paulo II akatuma ujumbe huko Moscow eti kwamba kama majeshi ya Usovieti yangethubutu kuigandamiza Solidarity, yeye mwenyewe angeenda hadi Poland na kusimama na watu wake." *Reader's Digest*, Machi 1990.

"Wakati Tadeusz Mazowiecki alipochukuwa usukani mnamo Agosti 1989 kama waziri mkuu wa kwanza wa Poland asiyekuwa Mkomunisti kwa muda wa miaka arobaini na tano, aliulizwa iwapo yeye alikuwa Msosiolisti. 'Mimi ni Mkatoliki,' akajibu kwa kifupi." *U.S. News and World Report*, May 21, 1990.

"Maaskofu watatu wapya Wakatoliki wameteuliwa hivi majuzi huko Czechoslovakia. Na mwezi huu Gorbachev atakutana na Yohana Paulo II katika ziara yake ya Italia – makabiliano ya kwanza ya ana kwa ana kati ya viongozi wa Kremlin na Vatikana. Vikao hivyo vyaweza kupelekea kuhalalishwa kwa Kanisa Katoliki ya Kiukraini iliyopigwa marufuku kitambo ndani ya U.S.S.R." *Life*, December, 1989.

"Mwaka jana, maaskofu wawili mashuhuri wa Lithuania walirudishwa kuziongoza Diocese baada ya jumla ya miaka 53 kama wakimbizi wa ndani, nalo kanisa kuu la Vilniusi, lililokuwa likitumika kama jumba la makumbusho la Sanaa, likarejeshwa kuwa la ibada. Mwaka huu, jamuhuri ya Belarusi ilipata askofu wake wa kwanza baada ya miaka 63. Jambo hili lilimwandalia njia Askofu mkuu Angelo Sodano, ambaye hushughulika na maswala ya uhusiano wa kigeni wa Vatikana, kufanya maandalizi ya ziara ya kihistoria ya Gorbachev kwenye Jimbo Takatifu.

"Makubaliano haya na Ukatoliki ni sehemu tu ya ukarimu wa Gorbachev kidini." *Time*, December 4, 1989.

"Kuamshwa kwa uhuru wa kidini kwatarajiwa kujumuisha kuondolewa kwa marufuku rasmi ya Kanisa Katoliki la Ukraini, ambalo limedumu mafichoni tangu 1946 pale Starlin alipoliamrisha lijiunge na Kanisa la Orthodoxi la Urusi. Kushinda huko kwa uhalali wa Kanisa la Ukraini limekuwa ni kusudio la kimsingi la papa. Maafisa katika Muungano wa Sovieti wasema kuwa watatengeneza njia ya kuhalalishwa na kuruhusiwa kwa Wakatoliki wa Ukraini kujisajili, jinsi makundi mengine yanavyohitajika sasa kufanya chini ya sheria ya Kisovieti." *U.S. News and World Report*, December 11, 1989.

Habari za ulimwengu zasema kuwa Ukatoliki ulijishirikisha na Marekani, kwa kutumia shinikizo la kiuchumi, kijamii, kidini, kisiasa na kijeshi kusababisha kuporomoka kwa Ukomunisti. Licha ya hadithi za ajabu kuhusu shangwe ya ushindi wa uinjilisti Mashariki mwa Ulaya, tunalo hakikisho ya kuwa Kanisa Katoliki laharakisha kudai tena ushawishi wake wa awali juu ya nchi hizi huku likizidi – "kufurika na kupenya."

Gazeti la *Time*, Februari 24, 1992, lilichagua kichwa, "**Ushirikiano Mtakatifu**," katika kujadili kuja pamoja huku kwa Marekani na Vatikana wanapojaribu kuuangusha Ukomunisti.

Gazeti hilo lafafanua kuhusu siri ya ushirikiano huu, na ukaribu uliopo kati ya Vatikana na uongozi wa Marekani. Linauleta ufungamano kati ya Vatikana na miungano ya wafanyakazi, huku ikitambulisha Solidarity kama mmoja wa wahusika wakuu katika njama hii. Vilevile linayatambulisha matumizi ya jeshi letu, CIA, vyama vya wafanyakazi na pesa, kama vifaa muhimu vya ushirikiano huu.

"Ni Rais Ronald Reagan na Papa Yohana Paulo II pekee waliokuwepo ndani ya Maabara ya Vatikana mnamo Jumatatu, Juni 7, 1982. Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa hao wawili kukutana, nao walizungumza kwa dakika hamsini ….

"Katika mkutano huo, Reagan na papa walisikizana kufanya kampeni ya siri ya kuharakisha mvurugiko wa milki ya Kikomunisti. Asema Richard Allen, Mshauri wa kwanza wa Reagan katika mambo yanayohusu Usalama wa Kitaifa: '**Huu uliokuwa ni mojawapo wa miungano ya siri zaidi kuwahi kufanyika.**'

"'Reagan aliingia akiwa na mitazamo rahisi sana aliyoishikilia kwa nguvu,' asema Admiral Bobby Inman, naibu mkurugenzi wa zamani wa CIA. 'Ni mtazamo halali ya kuwa aliona kuporomoka (kwa ukomunisti) kukija, naye **akasukuma – kwa nguvu.** Katika nusu ya kwanza ya 1982, mkakati wenye sehemu tano ulitokea ambao ulikusudiwa kusababisha kuporomoka kwa itikadi ya Kisovieti ….

"[1.] Ongezeko la zana za kujihami za Marekani ambalo tayari laendelea, likikusudiwa kulifanya jambo la gharama kubwa mno kwa Wasovieti kushindana na Marekani **kijeshi.** Ule Uwezo wa Mkakati wa Kujihami wa Reagan – yaani Vita vya Sayari – ukawa ndicho kitovu cha mkakati huo.

"[2.] Operesheni za siri zilizokusudiwa kutia moyo wa kufanyika marekebisho huko Hungary, Czechoslovakia na Poland.

"[3.] Msaada wa **kifedha** kwa mataifa ya Mkataba wa Warsaw ukikadiriwa na radhi yao ya kuzilinda haki za binadamu kufanya marekebisho ya kisiasa na ya soko-huru.

"[4.] Kutengwa **kiuchumi** kwa Muungano wa Sovieti na kuondolewa kwa teknolojia ya Magharibi na Japani kutoka Moscow. Utawala huo ulilenga kuinyima U.S.S.R. kile ulichotumai kingekuwa ndio asili kuu ya pesa zao katika karne ya ishirini na moja: faida kutoka kwa mfereji wa bara kwa bara unaopeleka petroli hadi Ulaya ya Magharibi.

"[5.] Kuongezeka kwa matumizi ya Uhuru wa Redio, Sauti ya Marekani na Redio ya Ulaya Huru kupeperusha jumbe za Utawala huo kwa watu wa Ulaya ya Mashariki.

"'Kama viongozi wote wakuu na waliobahatika, Papa na Rais walizitumia nguvu za historia kwa manufaa yao wenyewe.'" *Time*, February 4, 1992, 29–30.

Jambo la kustaajabisha katika historia hii ni kwamba Mungu, kupitia Danieli, aliyaelezea matukio haya kwa muhtasari ndani ya aya moja tu, yenye maneno hamsini pekee.

Katika kitabu chake, *Keys of This Blood*, Malachi Martin, aliyehudumu ndani ya Vaticana, ajitahidi kuonyesha kuwa yale majaribio ya kumuua papa yalitazamwa na Yohana Paulo II kama ushahidi wa kiungu ya kuwa ndiye papa ambaye angepaa kwenye kiti cha enzi cha ulimwengu. Papa huyo aliliona jaribio hilo la mauaji yake kama ishara kutoka kwa Maria, hivyo kuuthibitisha ule ujumbe uliotumwa kwa Kanisa Katoliki na kwa ulimwengu – kupitia kwa ufunuo wa kimwujiza eti kutoka kwa "bikira" wa Fatima, nchini Ureno. Mwujiza huu, na ujumbe ulioambatana nao, ndio nguvu zinazouongoza Ukatoliki huku wakijiandaa kwa miaka elfu ijayo ya amani. Mwujiza huo wa Fatima unazo habari maalum kuhusu Ukomunisti, Urusi na kuongoka kwa ulimwengu. La ajabu ni kwamba mwujiza huu ulifanyika mwaka wa 1917 – mwaka ule ule yalipofanyika Mapinduzi ya Bolsheviki.

Kupona kwa lile jeraha la kufisha kwatambulisha kurejeshewa Upapa kwa uwezo wa kutawala kisiasa. Vatikana ilikipoteza kiti chake cha enzi mwaka wa 1798, pale "mfalme wa kusini" alipoanzisha vita dhidi ya "mfalme wa kaskazini." Yafaa pia kuangaliwa kuwa lile jaribio la 1981 la kumwua Papa – mfalme wa kaskazini – liliamrishwa na mfalme wa kusini – Muungano wa Sovieti.

Katika maelezo mafupi ya picha mbili zilizokuwa zikionyesha majaribio ya mauaji ya papa na Ronald Reagan, taarifa ifuatayo ilifanywa:

> "Kuguswa Kidogo na Kifo – Katika mkutano wa kwanza, Reagan na Yohana Paulo II walijadiliana kuhusu jambo lingine ambalo wanashirikiana: wote wawili wamewahi kunusurika majaribio ya kuwaua yaliyoachana kwa miezi sita tu mnamo 1981, na wote wawili **waliamini kuwa Mungu aliwaokoa** ili wautekeleze wajibu fulani maalum. Na wote wawili waliutaja kuwa ni 'muujiza' ukweli kuwa 'walinusurika.'
>
> "Mnamo Mei 1981, mbele ya umati katika uwanja mraba wa St. Peter, Papa Yohana Paulo alipigwa risasi na kujeruhiwa vibaya sana na Mehmet Ali Agea. Mara moja kulikuwa na kisio kuwa mwuaji huyo Mturuki alikuwa ametumwa na walaji njama wa jumuiya ya Mashariki kutoka Bulgaria, huku wakifadhiliwa na polisi wa ujasusi wa Usovieti. Kusudi lao: kumnyamazisha mtu mmoja mwenye uwezo wa kuitikisa misingi ya Ukomunisti wa kimataifa." *Life*, December 1989.

> "Huku ikiungwa mkono na Papa, Solidality (Muungano wa Wafanyakazi wa Poland) ilibuniwa, naye Yohana Paulo II akatuma ujumbe huko Moscow eti kwamba kama majeshi ya Usovieti yangethubutu kuigandamiza Solidarity, yeye mwenyewe angeenda hadi Poland na kusimama na watu wake. Wasovieti waliogopa mno hadi wakapanga njama ya kumwua … Papa aliwatahadharisha viongozi wa Solidarity, hasa rafiki yake Lech Walesa, kusonga polepole. Walifanya hivyo. Mnamo 1988, Jemedari Wojciech Jaruzelski, kiongozi wa kikomunisti wa Poland, aliwaendea na kutaka maafikiano. Solidarity ilisisitiza kuwe na uchaguzi, ambao ulifanyika huku wakijinyakulia asilimia 80 ya kura. Wakati serikali ya kikomunisti ilipoanguka, athari zake juu ya Ulaya Mashariki ilikuwa ni ya kusisimua." *Reader's Digest*, March 1990.

Vitendo vya mwisho katika kupona kwa jeraha hilo la kufisha la Upapa vimeanza, na la kinaya ni kuwa, papa anayetawala mwenyewe alipokea jeraha la kufisha katika wakati huu. Kutimia kwa Danieli 11:40 ni hatua ya kwanza ya hatua tatu zinazohitajika kukamilisha uponyaji wa jeraha hilo la Papa ambalo ni la kufisha. Hatua ya kwanza sasa ni historia iliyopita. Kumbukumbu ya historia ya vita kati ya falme hizi mbili yathibitisha kuwa viliendelea hadi mwisho kabisa. Eneo lingine la Vatikana kulishinda ni "nchi ya uzuri" – yaani Marekani.

Huenda jambo muhimu sana kuhusu aya ya arobaini ni kwamba Marekani tayari imebuni muungano na adui ambaye anajiandaa kuiweka chini ya utawala wake. Huu ni msisitizo wa jinsi Upapa ulivyofikia kuutawala ulimwengu pale mwanzo, kwani mara tu Clovis alipoisalimisha imani yake ya kikafiri pale alipokuja kuusaidia Upapa, vivyo hivyo Marekani nayo iliisalimisha imani yake ya Kiprotestanti pale ilipokuja kuusaidia Upapa. Huu ni ukweli kwa sababu ili kuifikia maana ya Protestanti, sharti mtu aupinge upapa, na kushikilia hali thabiti ya kukana aina yoyote ya ushirikiano na Ukatoliki.

> "Ndugu zangu, Bwana ataka ushirikiano kazini mwake. Hitaji lake ni kwamba sisi tuunganishe mivuto yetu na kazi yake, kama alivyofanya Danieli. Twafaa kupata manufaa makuu kwa kusoma kitabu cha Danieli kikihusiana na Ufunuo. Danieli aliusoma nabii. Alijitahidi kufahamu maana zake. Yeye aliomba na kufunga ili apate nuru kutoka mbinguni. Nao utukufu wa Mungu ulifunuliwa kwake hata zaidi ya kile ambacho angevumilia. Sisi pia tunalo hitaji la kuangaziwa na Mungu sawa na hilo. Mungu ametuita tupeane ujumbe wa mwisho wa onyo kwa ulimwengu. Zitasikika sauti katika kila upande ili kuwavuta kwingine watu wa Mungu kwa nadharia mpya. Yatupasa kuipa tarumbeta sauti fulani. Hatutambui hata nusu yale yaliyo mbele yetu. Kama vitabu vya Danieli na Ufunuo vingesomwa pamoja na maombi yenye ari, tungekuwa na ufahamu bora zaidi kuhusu hatari za siku za mwisho, na kujiandaa vyema kwa kazi iliyoko mbele yetu – yatupasa kujiandaa kuungana na Kristo na kufanya kazi katika njia zake." *Review and Herald*, February 9, 1897.

Nchi ya Uzuri ya Kisasa

Tena ataingia katika hiyo Nchi ya uzuri, na Nchi nyingi zitapinduliwa, lakini nchi hizi zitaokolewa na mkono wake Edomu, Moabu na wakuu wa watu wa Amoni. Danieli 11:41.

Danieli 11:41 yatambulisha eneo linalofuata la ushindi kwa "mfalme wa kaskazini" kama "nchi ya uzuri." Neno linalotafsiriwa kama "uzuri" laelezewa ndani ya *Strong's Concordance* kama, "katika maana ya umaarufu; mng'ao (kama waziwazi), zuri, njema."

Kwa kukubaliana na maana hiyo neno hili wakati mwingine hutafsiriwa kama "nzuri." Wakati mwingine hutumika kuielezea Palestina ya kale, yaani Nchi ya Ahadi ya kale ya Israeli ambayo "ilitiririka maziwa na asali." Hii ilikuwa ndiyo nchi ambayo Musa kwa ari alitamani kuingia – japo alikatazwa.

> Nami nakuomba nivuke, nikaone hiyo nchi nzuri iliyoko ng'ambo ya Jordani, mlima ule mzuri, na Lebanoni. Kumbukumbu la Torati 3:25.

> "Yule Mtawala Mkuu wa mataifa alikuwa ametangaza kuwa Musa hangeliongoza kusanyiko hilo la Israeli kuingia ndani ya nchi hiyo njema, na japo mtumishi huyo wa Mungu alimsihi kwa ari, hangeubadili uamuzi huo. Yeye alijua kuwa sharti angekufa. Hata hivyo hakusita hata kwa muda katika kuwachunga Israeli. Kwa uaminifu alikuwa amejitahidi kuliandaa kusanyiko hilo kuingia kwenye **urithi walioahidiwa**." *Patriarchs and Prophets,* 469.

> Nchi hiyo njema ilikuwa ni "urithi ulioahidiwa," ambao ulikusudiwa kulitimiza lengo fulani kwa Waisraeli wa kale.
>
> "Huko Misri ustaarabu wao ulikuwa umepotoka. **Mungu alikusudia** kuirejesha hamu yao ya chakula kuwa katika hali ya usafi na afya, ili wayafurahie yale matunda ya asili waliopewa Adamu na Hawa huko Edeni. Alielekea kuwaweka ndani ya Edeni ya pili, **nchi njema**, ambapo wangeyafurahia matunda na nafaka alizonuia kuwapa. Yeye alikusudia kuviondoa vyakula duni walivyokuwa wamevizoea huko Misri; kwani aliwatakia wawe watu wenye afya bora na timamu wakati wa kuingia kwenye **nchi hiyo njema** ambapo alikuwa akiwaongoza, **ili mataifa ya washenzi yaliyowazingira walazimike kumtukuza Mungu wa Israeli**, yaani Mungu aliyewatendea watu wake maajabu kama hayo. Isipokuwa kama wale watu waliomtambua kama Mungu wa Mbinguni wangekuwa wenye afya timamu, **jina lake halingetukuzwa**." *The Seventh-day Adventist Bible Commentary*, volume 1, 1102.

> "Sheria ya Mungu sharti iinuliwe, na mamlaka Yake kudumishwa; nayo nyumba ya Israeli ilipewa jukumu hili kuu na adilifu. Mungu aliwatenga kutoka ulimwenguni, ili awakabidhi amana takatifu. **Yeye aliwafanya mabohari wa sheria yake, naye alikusudia ya kuwa kupitia kwao, angeuhifadhi ujuzi wake miongoni mwa wanadamu**. Hivyo nuru ya Mbinguni ingeng'aa juu ya ulimwengu uliofunikwa na giza, na sauti ingesikika ikiwasihi watu wote wageuke kutoka kwa ibada ya sanamu wamtumikie Mungu aliye hai.
>
> "'Kwa uweza mkuu, na mkono wenye nguvu,' Mungu aliwatoa watu Wake wateule kutoka nchi ya Misri. Kutoka 32:11. 'Akamtuma Musa mtumishi wake, pamoja na Aroni, ambaye alikuwa amemchagua. Walifanya ishara zake za ajabu miongoni mwao, miujiza yake katika nchi ya Hamu.' 'Alikemea bahari ya Shamu, nayo ikakauka, akawaongoza katika vilindi vyake kama vile jangwani.' Zaburi 105:26-27; 106:9. Yeye aliwaokoa kutokana na hali yao ya utumwa ili awalete kwenye nchi nzuri, nchi ambao **kwa majaliwa yake alikuwa amewaandalia** kama hifadhi kutoka kwa maadui wao. Angewaleta kwake mwenyewe na kuwakumbatia na mikono yake ya milele; nao kama shukrani kwa wema na rehema Zake walitakiwa kuliinua jina lake na kulifanya tukufu duniani.
>
> "'Kwa kuwa fungu la BWANA ni watu wake, Yakobo kura yake ya urithi. Katika nchi ya jangwa alimkuta, katika nyika tupu ivumayo upepo. Alimhifadhi na kumtunza, akamlinda kama mboni ya jicho lake. Kama tai avurugaye kiota chake na kurukaruka juu ya makinda yake, ambaye hutanda mabawa yake na kuwadaka na kuwachukua kwenye mbawa zake. BWANA peke yake alimwongoza, hakuwepo mungu mgeni pamoja naye.' Kumbukumbu la Torati 32:9-12. Hivyo aliwaleta Waisraeli Kwake, ili waweze **kudumu chini ya kivuli cha Aliye Juu Zaidi**. Baada ya kuhifadhiwa kimwujiza kutokana na hatari za kutangatanga jangwani, hatimaye waliimarishwa katika **nchi ya Ahadi kama taifa lililopendelewa**." *Prophets and Kings,* 16.

Palestina "ilibuniwa" na Bwana kama nchi yenye rutuba na ya kusitawi, iwezayo kuwatosheleza Waisraeli wa kale kwa mahitaji yao yote ya kimaisha. Katika ubunifu wake wa uwekevu, Bwana aliiweka Palestina katika makutano ya barabara za ulimwengu wa kale. Eneo hili la kati liliwawezesha Wasraeli kuingiliana na wanadamu kwa urahisi huku wakijitahidi "kuuhifadhi ujuzi Wake miongoni mwa wanadamu." Mungu "alikusudia" kulea "taifa lililopendelewa," ambalo lingekuwa "bohari ya sheria Yake." Kama wangeyashikilia masharti ya hiyo "amana takatifu," wangeliinua "jina Lake" na kulifanya "tukufu duniani." Ili kulitekeleza kusudio hilo takatifu Yeye aliibuni nchi maalum ya usitawi, iliyowekwa na Mungu katikati mwa jukwaa la maonyesho ya ulimwengu. Ufafanuzi wa neno "uzuri" huelezea vizuri Palestina na kusudi lake, hasa tukiangazia umaarufu na uzuri wake.

DANIELI NA ILE NCHI YA UZURI

Danieli aongea kuhusu "nchi ya uzuri" mara mbili katika sura ya kumi na moja. Ameitaja nchi hii mara ya kwanza katika Danieli 11:16:

> Maana ajaye kupigana naye atatenda kadiri apendavyo, wala hapana mtu atakayesimama mbele yake; naye atasimama katika nchi ya uzuri, na uharibifu utakuwa mkononi mwake.

Uriah Smith, akizungumzia aya hii asema:

> "Baada ya kuvikomesha vita hivyo, Pompey alizibomoa kuta za Yerusalemu, akaihamisha miji kadhaa kutoka kwenye mamlaka ya Judea hadi ile ya Syria, na kuwatoza Wayahudi ushuru. Kwa mara ya kwanza Yerusalemu, kwa njia ya kushindwa, iliwekwa mikononi mwa **Roma, na utawala huo ulikuwa uishike 'nchi ya uzuri' kwa mikono yake ya chuma** hadi iiharibu kabisa." *Daniel and the Revelation,* 247.

Uriah Smith, pamoja na waanzilishi wengineo Waadventista, aliitazama Danieli 11:16 vilivyo, kwamba ilielezea ushindi wa Roma ya kikafiri juu ya hiyo "nchi ya uzuri," yaani Palestina ya kale. Uvamizi wa Roma ya kikafiri na ushindi wake waonyeshwa kiunabii na matumizi ya kiishara ya neno "mkono."

"Mkono" hutumika kiunabii kutambulisha kutiishwa kwa nguvu. Ishara hii ya kutiishwa yaweza kuelezea kutiishwa kwa kawaida au kwa kiroho, kulingana na muktadha. Kuifahamu maana ya kiishara ya "mkono" kama nguvu, hutambulisha jinsi alama ya mnyama itakavyotumika. Katika Danieli 11:41, twaiona Roma ya kipapa ikiishinda kiroho nchi ya Marekani kuhusiana na maelezo ya wale wanaoponyoka "mkono" wake. Tutatazama kwa karibu zaidi matumizi ya kiroho ya neno "mkono" katika sura ifuatayo.

Danieli 11:16 yaionyesha Palestina ya kale ikivamiwa waziwazi jinsi Israeli ya kale ilivyoshindwa waziwazi na Roma ya kikafiri, lakini hiyo "nchi ya uzuri" ya Israeli ya kisasa itashindwa kiroho na Roma ya kipapa. Dada White ashauri kuwa "uzoefu wote" wa Israeli ya kale unayo mafundisho muhimu ambayo Israeli ya kisasa yafaa "kuyatafakari kwa uangalifu."

YA KALE NA YA KISASA

> "Ujuzi wote wa Israeli unalo fundisho kwetu sisi, tunaoishi katika masaa ya mwisho ya nyakati. Twafaa kutafakari kwa uangalifu njia ya matendo yao na jinsi walivyopelekana na Mungu, kisha tuyaige matendo yao mema, huku tukiepukana na yale matendo yaliyowaletea ghadhabu yake. Mungu huyu mwenyezi wa Israeli ndiye Mungu wetu. Ndani yake twaweza kutumainia, na iwapo tutayatii matakwa yake, Yeye atatutendea kazi kwa namna ya ajabu kama alivyowatendea watu wake wa kale. Lingekuwa ni somo la dhati na juhudi zisizo na kikomo kwa Israeli ya kisasa kujileta kwenye uhusiano wa ndani na wa karibu na Mungu." *The Signs of the Times*, November 11, 1880.

> "**Nilielekezwa nyuma kwa Israeli ya kale**. Ni watu wazima wawili pekee walioingia nchi ya Kanani miongoni mwa jeshi hilo kubwa lililotoka Misri. Maiti zao zilitapakaa jangwani kwa sababu ya dhambi zao. **Israeli ya kisasa wako kwenye hatari kuu** kwa kumsahau Mungu na kuongozwa kwenye ibada ya sanamu **kuliko watu Wake wa kale**." *Testimonies*, volume 1, 609.

> "Ushahidi dhahiri umepeanwa ya kuwa Mungu ni Mungu mwenye wivu, na kuwa **Yeye atahitaji kutoka kwa Israeli ya kisasa kama alivyohitaji kutoka kwa Israeli ya kale**, kwamba waitii sheria yake. **Historia hii takatifu imenakiliwa na kalamu ya unabii kwa wote waishio duniani.**" *The Signs of the Times*, May 27, 1880.

Wakati Dada White anasema, "Uzoefu wa Israeli unalo fundisho kwetu sisi," na kuwa, "historia hii takatifu," "imenakiliwa" kwa "wote waishio duniani," anaitambua nchi ya ahadi kama sehemu muhimu ya usambamba kati ya Israeli ya kale na ya kisasa.

Tafakari vyema dondoo ifuatayo. Japo kimsingi inazungumzia Marekani, Dada White kwanza anadondoa kutoka Yeremia 3:18-19. Aya hii hasa inaizungumzia Palestina ya kale kama "nchi" ambayo Israeli walikuwa "wamepewa kuwa urithi." Kisha Dada White anatambulisha nchi fulani iliyopendelewa ambayo ilikuwa imepeanwa na Mungu – Israeli ya kisasa. Pia fahamu kuwa wote wawili, yaani Yeremia na Dada White, wanatofautisha vyema kati ya watu wa Mungu na nchi waliopewa watu wa Mungu:

> "Siku zile nyumba ya Yuda watakwenda pamoja na nyumba ya Israeli, nao watakuja pamoja, **kutoka nchi ya kaskazini, mpaka nchi ile niliyowapa baba zenu iwe urithi wao**. Lakini mimi nalisema, nitawezaje kukuweka pamoja na Watoto, na kukupa **nchi ipendezayo, urithi ulio mwema** wa mataifa? Nami nikasema, Mtaniita, Baba yangu, wala hamtageuka na kuacha kunifuata." Yeremia 3:18-19.

> "Wakati **nchi** ambayo **Bwana alipeana kama hifadhi kwa watu wake,** ili waweze kumwabudu kulingana na dhamiri zao, **nchi** ambayo kwa miaka mingi **ngao ya Mwenyezi** ilinyoshwa juu yake, **nchi iliyopendelewa na Mungu** kwa kuifanya **bohari ya dini safi ya Kristo** – wakati **nchi hiyo**, kupitia wabunge wake, itazikana kanuni za Uprotestanti, na kuukubali uasi wa Roma katika kuivuruga sheria ya Mungu – ni wakati huo ambapo kazi ya mwisho ya yule mtu wa kuasi itafichuliwa." *Signs of the Times*, June 12, 1893.

Tulifahamu hapo awali ya kuwa ahadi ya Mungu kwa Israeli ya kale ilikuwa kwamba "wangeishi chini ya kivuli cha Aliye Juu Zaidi" huku Yeye "akiwakumbatia kwa mikono yake ya milele." Kuhusu Israeli ya kisasa, Marekani ndiyo "nchi" iliyotolewa kama "kimbilio kwa watu Wake." Ndiyo "ile nchi" ambayo "yapendelewa" na "ngao ya Mwenyezi." Dada White aitaja "ile nchi" mara nne katika fungu hili, huku akisisitiza eneo la kijiografia la Marekani. Marekani "ilikusudiwa" na Mungu ilitimize kusudi la Israeli ya kisasa sawa na ilivyofanya Palestina kwa Israeli ya kale.

> "Bwana ameitendea mengi **Marekani** zaidi ya **nchi** nyingine yoyote imulikwayo na jua. **Hapa** Yeye alitoa kimbilio kwa watu Wake, ambapo wangeweza kumwabudu kulingana na dhamiri zao. **Hapa** Ukristo umeendelea katika usafi wake. Fundisho lipeanao uhai kuhusu Mpatanishi mmoja kati ya Mungu na mwanadamu limefundishwa bila kuzuiwa. Mungu **alikusudia** kwamba **nchi hii** daima iwe huru ili watu wote wamwabudu kulingana na dhamiri zao. Yeye **alikusudia** kwamba asasi zake za kiserikali, katika uzalishaji wao mpana, usimamie uhuru wa haki za injili." *Maranatha*, 193.
>
> "**Marekani ni nchi ambayo imekuwa chini ya ngao maalum ya Mwenyezi**. Mungu ameitendea **nchi hii** mambo makuu. Lakini katika kuivunja sheria Yake, watu wamekuwa wakifanya kazi itokayo kwa yule mtu wa kuasi. Shetani anafanya ubunifu wake ili aihusishe jamii ya wanadamu katika kutotii," *The Seventh-day Adventist Bible Commentary*, volume 7, 975.

Marekani ilikusudiwa kuwa nchi ya kisasa ya maziwa na asali, ili watu wa Mungu waweze kuutangaza ujumbe wa onyo la mwisho kwa ulimwengu. Usitawi wake, kanuni za serikali, na cheo chake kama chungu cha kuyeyushia watu wa mataifa yote ya ulimwengu "zilikusudiwa" kutoa manufaa ya unjilisti kama yale yaliyotolewa na Israeli ya kale kupitia ile nchi tukufu ya Palestina ya kale. Kufikia sasa, tumeshindwa kuyatumia kikamilifu manufaaa haya, kama vile Israeli ya kale ilishindwa. Muda unakwisha upesi!

> "**Je, ni jambo la bure tu** ambapo kuutangaza kwa ukweli wa milele **kumekabidhiwa taifa hili** ili upelekewe mataifa yote ya ulimwengu? Mungu amewachagua watu fulani na kuwafanya chemchemi ya ukweli mzito wenye matokeo ya milele. Wao wamekabidhiwa nuru ambayo sharti iangazie ulimwengu. Je, Mungu amekosea? Je, sisi kweli ni vyombo vyake alivyovichagua? Je, sisi ndio waume na wanawake ambao wataupelekea ulimwengu ujumbe wa Ufunuo kumi na nne, kuutangaza ujumbe wa wokovu kwa wale wanaosimama ukingoni mwa uharibifu? Je, twatenda kama kweli ndio sisi?" *Selected Messages*, book 1, 92.

Vita baina ya wafalme wa kusini na kaskazini katika Danieli 11:40 vyaashiria 1798 kama mwanzo wa pambano kati ya Ukatoliki na ukanaji dini. Vita vinavyoonyeshwa katika aya hiyo havisuluhishwi hadi pale "magari ya vita, na merikebu," ambazo zaashiria uwezo wa Marekani wa kiuchumi na kijeshi, zinapoletwa kwenye ushirikiano na Ukatoliki. Marekani na Upapa walibuni ushirikiano wenye msingi wa kuitambulisha USSR, "mfalme wa kusini" wa kisasa, kama adui wa pamoja.

Ushirikiano huu waenda sambamba na vitendo vya Clovis, mfalme wa Ufaransa, ambaye aligeuka kutoka kwenye dini ya taifa lake ili aje ausaidie ukatoliki katika vita vyake dhidi ya Uariani. Ushirikiano huo kati ya Clovis na Ukatoliki ulianzisha mashambulizi dhidi ya Ostrogoths, Vandals na Heruli, ambavyo vilikuwa ni vita sio tu dhidi ya mataifa hayo **matatu**, bali pia vita dhidi ya falsafa ya kidini ya Uariani ambayo ilikuwa ikishikiliwa na mataifa hayo matatu. Ushirikiano huo ukishabuniwa, Clovis na mataifa mengine ya Ulaya ambayo hapo awali yalikuwa ya kikafiri, walianza mashambulizi ya kijeshi ambayo yaliuketisha Upapa juu ya kiti cha enzi cha ulimwengu. Kutoka A.D. 508, kazi ya kuzing'oa pembe zile tatu za Danieli saba, iliendelezwa hadi ya mwisho kati ya hizo pembe tatu ilishindwa mnamo AD 538. Wakati huo utawala wa Upapa ambao ndio chukizo liletao ukiwa, ulisimamishwa.

Ushirikiano baina ya Clovis na Vatikana ulipelekea utawala wa Upapa wa miaka 1260, ambao ulimalizia na kupatiwa lile "jeraha la kufisha" mnamo 1798. Ufaransa ya Clovis iliuwezesha Upapa kuianzisha miaka hiyo 1260, nayo Ufaransa ya Napoleon ikatumia uwezo wake kuitamatisha miaka hiyo 1260 kirasmi. Kile kilichoanza kwa ushirikiano kiliisha kwa vita na kuchukuliwa mateka. Aya ya arobaini yaanza na mwisho wa kipindi cha kwanza cha utawala wa upapa mnamo 1798, lakini kisha hutambulisha kulipiza kisasi siku za usoni dhidi ya "mfalme wa kusini," na hivyo kuanzisha kipindi cha mwisho cha utawala wa upapa. Katika aya hii, huku ikielezea matokeo ya mwisho ya ushirikiano huo wa Clovis, twaiona Marekani ikiashiriwa na kama "merikebu, na magari ya vita" inapoanza kuirudia kumbukumbu ya historia hiyo ya kufedhehesha ya ushirikiano wa Clovis.

Katika mandhari ya kihistoria ya 1798, Dada White pia azungumza kuhusu Marekani:

> "Ni taifa gani la Ulimwengu Mpya lilikuwa likiinuka katika uwezo mnamo 1798, huku likionyesha ahadi ya nguvu na ukuu, **na kuivuta nadhari ya ulimwengu**? Kutumika kwa ishara hii hakuruhusu swali lolote. Taifa moja, moja pekee, lafaa ainisho la unabii huu; laelekeza bila shaka kwenye Marekani. Mara kwa mara wazo hili, karibu maneno kamili, ya mwandishi huyo mtakatifu yamekuwa yakitumiwa, bila ya kufikiria, na mnenaji na mwana historia katika kuelezea kuinuka na kukua kwa taifa hili. Mnyama alionekana 'akipaa juu kutoka ardhini;' na, kulingana na watafsiri, neno hilo linalotajwa 'kupaa juu' kawaida humaanisha 'kukua au kuchipuka kama mmea ….'

"'Naye ana pembe mbili mfano wa Mwanakondoo.' Pembe mfano wa mwanakondoo huashiria ujana, uungwana, upole, vikionyesha hali halisi kabisa ya tabia ya Marekani. Wakati ule lilipoonyeshwa kwa nabii kama Linalopanda juu katika mwaka 1798. Miongoni mwa wakimbizi wakristo wa kwanza kukimbilia Marekani na kutafuta mahali pa amani na usalama kutoka kwenye mateso ya utawala na ukatili wa makasisi, walikuwepo wengiwalionuia kuanzisah serikali katika msingi mpana wa raia na uhuru wa dini. Mitazamo yao ilipata nafasi katika tangazo la uhuru, ambalo linaweka ukweli mkuu kwamba, watu wote wameumbwa sawa, na kupewa haki isiyoondolewa ya uhai, uhuru, na kutafuta Furaha. Na katiuka kuwapa watu hakikisho la haki za kujitawala wenywe, ikiweka wazi kwamba wawakilishi wakisha chaguliwa kwa kura ya umma watatunga na kusimamia sheria. Uhuru wa imani ya dini pia uliruhusiwa, kila mtu akiwa ameruhusiwa kumwabudu Mungu kulingana na msukumo wa dhamiri yake. Sera ya serikali ya jamhuri na imani ya Uprotestanti zikawa kanuni za msingi za taifa. Kanuni hizi ndizo siri ya nguvu na ustawi wake. Walioteswa na kunyanyaswa katika wote wa Ukristo walienda katika nchi hii wakiwa na ari na matumaini. Mamilioni wametafuta ufukwe wake, na **Marekani imetokea kuwa miongoni mwa mataifa yenye nguvu kubwa sana duniani.**" *The Great Controversy*, 441.

Yafaa kufahamika hapa kuwa Dada White amevipendekeza vitabu vya Danieli na Ufunuo kama vitabu vinavyoongezeana. Tunapoitambua Marekani kinabii katika Danieli 11:40-41, tutaulinganisha unabii huu na ule wa Ufunuo kumi na tatu, kama vile "mkono ndani ya glavu." Twajua kuwa aya ya arobaini yatutia kihistoria katika wakati wa lile "jeraha la kufisha." Ufunuo kumi na tatu ni ushahidi kuhusu yule mnyama mwenye jeraha la kufisha na yule mnyama autumiao uwezo wake kumponya mnyama huyo aliyeuliwa. Aya hizi katika Danieli zajichomoza kikamilifu kwenye Ufunuo kumi na tatu, na pia zinalingana vilivyo na ushuhuda wa Roho ya Unabii kuhusu kipindi hiki katika historia.

Mnamo 1798, ukanaji Mungu uliyaweka makao yake makuu ndani ya milki ya Ufaransa, baadaye kuhamia Urusi na hatimaye kukua na kuwa milki ya USSR. Mnamo 1798, Ukatoliki huwa mnyama aliyeuliwa, aliyetolewa kwenye cheo chake cha kisiasa kama mfalme wa dunia, ijapokuwa alikusudiwa hatimaye kukirejelea cheo hicho hicho alichokipoteza. Ukanaji Mungu na Ukatoliki zote zaonyeshwa zikiwa katika hali ya mabadiliko. Ni hivyo pia kuhusu Marekani, kwani mnamo 1798, Marekani ingali bado mnyama mwana kondoo mchanga wa Ufunuo kumi na tatu. Katika ujana wake, Marekani inahimiliwa na usafi wa mafundisho yake ya Kiprotestanti, lakini baada ya muda fulani, itaacha kuwa mwana kondoo na kuanza kunena kama joka. Vitu hivi vitatu vimefungwa pamoja katika Danieli 11:40, na kufikia aya ya arobaini na moja, Marekani, kwa kule kuipitisha sheria ya Jumapili, yakamilisha lile badiliko la Ufunuo 13:11.

Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa Mwana-Kondoo, akanena kama joka.

Sawa na kutambulisha pahali pa kuanzia kihistoria, maandiko yaonyesha nguvu tatu maalum katika Danieli 11:40. Nguvu hizo tatu zimewekwa ndani ya mandhari ambapo uhusiano wao waonekana kama tawala tatu za kisiasa zinazong'ang'ania utawala wa ulimwengu, lakini chini ya hiyo njaa ya utawala wa kilimwengu twaona pia mgongano wa mitazamo mitatu ya kiroho na ya kifalsafa.

Tunapokumbuka ya kuwa ule ujeuri wa Filauni dhidi ya Mungu uliashiria ukanaji Mungu, japo kwa hakika, huku akijidai kutomjua Mungu, Filauni na wananchi wake waliabudu miungu mingi bandia likiwemo jua, mwezi na nyota. Dini ya kimsingi ya falsafa ya ukanaji Mungu sio nyingine bali ni ukafiri safi, ambao leo hii watambuliwa ndani ya falsafa ya kuabudu miungu ya mwendo wa kizazi kipya. Dini ya "mfalme wa kusini" sio nyingine ila ni uchawi wa kisasa – ukiashiriwa na joka katika Ufunuo 16:13.

Nikaona roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura, zikitoka katika kinywa cha yule joka, na katika kinywa cha yule mnyama, na katika kinywa cha yule nabii wa uongo.

Kuyafahamu haya, kwazileta tawala zile tatu za Danieli 11:40 katika mandhari wazi zaidi, kwani yule mnyama na nabii wa uwongo wa Ufunuo 16:13 ni Ukatoliki na Uprotestanti ulioasi. Nguvu hizo tatu zinazouvuta ulimwengu kuelekea Harmagedoni, huanza harakati za kufanya hivyo katika Daneli 11:40!

Kuanzia lile shambulizi la kulibiza dhidi ya utawala wa ukanaji Mingu wa "mfalme wa kusini," mfululizo wa matukio yanayojitokeza kupitia aya zifuatazo yaelezea kukua kwa nguvu za kiroho za Ukatoliki ambao hushinda kupitia kuungwa mkono na jeshi la Waprotestanti walioasi. Ushindi wa kiroho unaowakilishwa unacho kifanani huku jiografia ya ulimwengu, hatua kwa hatua, ikiletwa chini ya umiliki na utawala wa Upapa, ikihimiliwa na kuungwa mkono na Marekani.

Ile "nchi ya uzuri" ya Marekani ndiyo shabaha inayofuata ya ushindi wa kiroho na huyo "mfalme wa kaskazini" wa kipapa.

"Taifa lililo kuu na **lenye kupendelewa zaidi** duniani **ni Marekani**. Majaliwa ya neema yameikinga **nchi hii**, na kuimwagilia mibaraka maalum ya mbinguni. **Hapa**, walioteswa na waliodhulumiwa wamepata hifadhi. Hapa, imani ya Kikristo imefundishwa katika usafi wake. Watu hawa wamekuwa wakipokea nuru kuu na rehema zisizo na kifani. Lakini vipaji hivi vimelipwa kwa kukosa shukrani na kumsahau Mungu. Mungu hufanya hesabu ya mataifa, na hatia yao imepimwa sawasawa na nuru waliyoikataa. Kumbukumbu ya kuogofya sasa iko kwenye nakala ya mbinguni dhidi ya **nchi yetu**; lakini uhalifu utakaojaza kipimo cha dhambi yake ni ule wa kuidharau sheria ya Mungu.

"Kati ya sheria za wanadamu na torati ya Yehova litakuja pambano kuu la mwisho la ubishani baina ya ukweli na uwongo. Sasa twaingia kwenye pambano hili – pambano ambalo sio baina ya makanisa yanayong'ang'ania mamlaka, bali ni kati ya dini ya Biblia na dini ya hekaya na utamaduni. **Mawakala wanaoungana dhidi ya ukweli na haki katika bishano hili sasa wafanya kazi kwa bidii.**" *The Signs of the Times*, July 4, 1899.

"**Marekani** …. pahali ambapo nuru kuu zaidi kutoka mbinguni imekuwa ikiwaangazia watu, yaweza kuwa pahali pa hatari kubwa zaidi na giza kwa sababu watu hawaendelei tena kuutenda ukweli na kutembea katika nuru." *Selected Messages*, book 3, 387.

"Watu wa **Marekani wamekuwa ni watu waliopendelewa**; lakini wanapouzuilia uhuru wa dini, kusalimisha Uprotestanti, na kuukaribisha upapa, kipimo cha hatia yao kitakuwa kimejaa, na 'uasi wa kitaifa' utasajiliwa vitabuni mwa mbinguni. Matokeo ya uasi huu yatakuwa ni uharibifu wa kitaifa." *Review and Herald*, May 2, 1893.

"**Nchi yetu** imo hatarini. Wakati unakaribia ambapo wabunge wake watazikana kanuni za Uprotestanti hata kuukubali uasi wa Roma. Watu ambao Mungu amewatendea maajabu, aliowatia nguvu ili waitupilie mbali nira ya upapa, watabuni sheria ya kitaifa ili kuipa nguvu imani potovu ya Roma, na hivyo kuuamsha uonevu ambao wasubiri kuguswa tu ili kuanza tena ukatili na udhalimu. Twakaribia kipindi hiki kwa hatua za kasi." *The Spirit of Prophecy*, volume 4, 410.

Mafungu yaliyopita kutoka kwa Roho ya Unabii, ambayo yalionyesha kusudio la Marekani, yanao umaizi mwingine muhimu ambao tuliupita – hadi sasa. Katika mafungu hayo tisa yaliyopita, tulijaribu kuitambulisha "nchi ya uzuri" ya kisasa kama Marekani. Hebu yapitie haya tena na utapata kuwa mafungu haya yote yanazungumzia sio tu Marekani, bali pia yanaizungumzia ile sheria ya kitaifa ya Jumapili.

Marejeo hayo mawili kwa "nchi ya uzuri" katika Danieli kumi na moja, hutambulisha kuingia kwa Roma kwenye nchi ya Israeli. Katika kukubaliana na Danieli, Dada White pia aweka habari yake kwenye "nchi ya uzuri" ya kisasa kuhusiana na "mfalme wa kaskazini" wa kipapa pale aingiapo ndani yake kwa kuipitisha sheria ya kitaifa ya Jumapili.

Historia ya Israeli ya kale yaleta usambamba muhimu ambao Israeli ya kisasa yafaa kuutafakari kwa maombi. Funzo moja, la umuhimu zaidi katika mfululizo huu, ni kutambua kuwa, kama vile Mungu alivyoitoa "nchi ya uzuri" ya Palestina kwa Israeli ya kale, vilevile ameitoa "nchi ya uzuri" ya Marekani kwa Waadventista Wasabato – yaani Israeli yake ya kisasa. Tumekabidhiwa jukumu la kuutangaza ujumbe wa onyo la mwisho kwa ulimwengu ambao unaogofya kwa kutojua kwake kuhusu masuala yanayojiri na majanga yanayohusishwa na nyakati za mwisho za neema. Israeli ya kale ilipewa jukumu sawa na hilo na wakashindwa. Ishara za nyakati, kuhusiana na kuongezeka kwa nuru ya unabii, zatudai sisi kama watu kuanza kuviondoa vikwazo vyovyote kutoka kwenye ujuzi wetu binafsi ambavyo vyaweza kutuzuilia tusiwe miongoni mwa wale wanaoutangaza ujumbe huu wa mwisho kwa sauti kuu.

"Kitabu cha Ufunuo sharti kifunuliwe kwa watu. Wengi wamefundishwa kuwa ni kitabu kilichofungwa, lakini kimefungwa tu kwa wale wanaoukataa ukweli na nuru. Ukweli ulio ndani yake sharti utangazwe, ili watu wapate nafasi ya kujiandaa kwa mujibu wa matukio yatakayotukia hivi karibuni. Ujumbe wa Malaika wa Tatu sharti upeanwe kama tumaini pekee la wokovu kwa ulimwengu unaopotea.

"Hatari za siku za mwisho ziko juu yetu, na katika kazi yetu twahitajika kuwaonya watu kuhusu hatari inayowakabili. Hebu na yale maonyesho ya dhati ambayo unabii umefunua ya kwamba yatatendeka hivi karibuni yasije yakaachwa bila kutajwa. Sisi tu wajumbe wa Mungu, na hatuna muda wa kupoteza. Wale watakaokuwa wafanya kazi pamoja na Bwana wetu Yesu Kristo wataonyesha haja kubwa ya ukweli upatikanao ndani ya kitabu hiki. Kwa kalamu na sauti watajitahidi kuyafafanua maajabu ambayo Kristo alikuja kutoka mbinguni ili kuyafunua." *Signs of the Times*, July 4, 1906.

Epuko Kuu

Tena ataingia katika hiyo nchi ya uzuri, na nchi mingi zitapinduliwa; lakini nchi hizi zitaokolewa na mkono wake, Edomu, na moabu, na wakuu wa watu wa Amoni. Danieli 11:41.

Katika Danieli 11:40-41, ndani ya kila aya limeashiriwa eneo maalum la uvamizi wa Upapa. Tumefahamu kuwa katika aya ya arobaini, Muungano wa Sovieti umeashiriwa kama "mfalme wa kusini," na katika aya ya arobaini na moja, Marekani yaashiriwa kama ile "nchi ya uzuri." Katika aya ya arobaini na mbili, ulimwengu mzima unaashiriwa kama "Misri," jambo ambalo tutalijadili katika sura ijayo. Neno **nchi** lapatikana katika kila moja ya aya hizi, lakini katika arobaini na moja, limechapishwa kwa herufi mlazo, hivyo kutambulisha neno lililoongezwa na watafsiri.

Katika aya ya arobaini, Upapa wazifagilia mbali nchi nyingi zilizoubuni ule Muungano wa Sovieti, na katika aya ya arobaini na mbili, Upapa wazileta nchi zote za ulimwengu chini ya utawala wake. Lakini katika aya ya arobaini na moja, wakati Upapa unaingia kwenye "nchi ya uzuri" ya Marekani, wengi (yaani watu) wanaangamizwa – wala **sio** nchi nyingi. Bila kuwa waangalifu, wale watafsiri wa King James Version waliidunisha tofauti muhimu ndani ya aya hizi kwa kule kuliongeza neno nchi katika aya ya arobaini na moja. Kwanza, Upapa waingia ndani ya nchi za ule uliyokuwa Muungano wa Sovieti; kisha, huingia Marekani; kisha, kila nchi duniani yaletwa chini ya utawala wake.

KUSONGA MBELE

Katika Danieli 11:40-45, twauona Upapa ukitembea huku ukipaa juu ya kiti cha enzi cha ulimwengu, na hatimaye kwenye maangamizi yake ya mwisho. Aya hizi zamwonyesha "mfalme wa kaskazini" akiupitia mfululizo wa matukio. Kwanza, **amvamia** mfalme wa kusini; kisha **aingia** ndani ya mataifa; na kisha **apita katikati**. Katika aya ya arobaini na moja, yeye **aingia** kwenye "nchi ya uzuri"; kisha, katika aya ya arobaini na mbili aenda hadi "Misri", na kufikia aya ya arobaini na tatu, nchi zote **zatembea** pamoja naye. Katika aya ya arobaini na nne yeye **aondoka** kwenda kuharibu, na hatimaye **aitia** hema yake katika aya ya arobaini na tano, ambapo atambulishwa kama **aufikia** kwa mwisho wake. Matukio haya yanayofunuliwa hutoa mandhari ambayo yaitambulisha habari inayoashiriwa ndani ya aya hii kama uendeleaji.

UTENGANO WA NAMNA MBILI

Huku Upapa ukiingia kiroho kwenye "nchi ya uzuri" pale sheria ya Jumapili itakapopitishwa, wale ambao "wataokolewa toka mkononi mwake," wanatofautishwa na wale "watakao angamizwa." Utengano kati ya wale watakaoangamizwa na wale watakaoponyoka hufanyika kwanza miongoni mwa watu wa Mungu, na kisha kuendelea ulimwenguni. Jaribio la sheria ya Jumapili litaimaliza shughuli ya kuwatenga watu wa Mungu, na mwanzo wa kuwatenganisha watu wa ulimwengu.

Utengano huu wa kwanza hufanyika ndani ya kanisa la Mungu, nao hutofautisha kati ya wale watakaoipokea mvua ya masika na wale watakaozisikiliza roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani:

> "**Suala kuu** lililo karibu sana [jaribio la Sabato] **litawang'oa** wale ambao Mungu hajawateua na Yeye atakuwa na wahudumu safi, wa kweli na waliotakaswa ambao wamejiandaa kwa mvua ya masika."*Selected Messages*, book 3, 385.
>
> "Niliona kwamba hakuna atakaelipata lile "Burudisho" isipokuwa amepata ushindi juu ya kila dhambi imzingayo, juu ya kiburi, ubinafsi, kuupenda ulimwengu, na juuu ya kila neno na tendo baya. Kwa hiyo, tunapaswa kumsogelea bwana, zaidi na zaidi na katika siku ya Bwana. Hebu sote na tuangalie kuwa Mungu ni mtakatifu na hakuna awezaye kuishi mbele zake isipokuwa tu wale walio watakatifu." *Early Writings*, 71.
>
> "**Wakati sheria ya Mungu itadharauliwa** kanisa litapepetwa kwa majaribu makali, na sehemu kubwa ya watu kuliko ile tunayoidhania, watazisikiliza roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani. *Selected Messages*, book 2, 368.

Utengano wa pili huanza pale bi harusi wa Mungu aliyesafishwa anapoanza kuwaita "kondoo wengine" Wake watoke Babeli.

> "Wakati wale 'wasioamini ukweli, bali waliufurahia uovu' (2 Wathesaloniki 2:12) wataachwa ili waupokee udanganyifu mkali hata kuamini uwongo, ndipo nuru ya kweli itang'aa juu ya wote ambao mioyo yao imefunguka ili kuupokea, na watoto wote wa Bwana waliosalia Babeli wataukubali mwito: 'Tokeni kwake, watu wangu.' Ufunuo 18:4." *Maranatha* 173.

Yale mateso yatakayoandamana na jaribio la sheria ya Jumapili yatawagawanya watu wa Mungu kati ya wale "wanaoupokea udanganyifu mkali" na wale "waliojiandaa kwa mvua ya masika."

> "Wakati mateso hayajakuwepo wameingia watu miongoni mwetu ambao huonekana kuwa timamu na Ukristo wao bila lawama, lakini ambao wangetuacha iwapo mateso yangezuka." *Evangelism*, 360.
>
> "**Kwa kadiri tufani ikaribiavyo,** kundi kubwa la watu ambao **wamejidai kuuamini** ujumbe wa malaika wa tatu, lakini hawakuwa wametakaswa kwa njia ya utii wa kweli, watauacha msimamo wao na kujiunga na askari wa upinzani." *The Great Controversy*, 608.

BADILIKO KWA MATATIZO ZAIDI

Kwa vile Marekani itabuni ushirikiano na Ukatoliki katika Danieli 11:40, itaacha kuishikilia misingi na kanuni za Uprotestanti. Badiliko hili litaendelea kukua na hatimaye kupelekea sheria ya Jumapili, inayoashiriwa na kuunganishwa kwa mikono. Baada ya sheria ya jumapili, ushirikiano huu utazidi kukua hadi pale Marekani itaulazimisha ulimwengu mzima kuitengeneza sanamu ya mnyama, na hatimaye ihusike katika kuyachapisha makataa ya kifo ulimwenguni.

> "Hatuoni ni jinsi gani Kanisa la Roma laweza kujitetea kutokana na shitaka la uabudu sanamu…. Na hii ndiyo dini ambayo Waprotestanti wanaanza kuitazama kwa fadhila nyingi, na ambayo **hatimaye itaungana** na Uprotestanti. Hata hivyo, muungano huu hautaletwa na badiliko la Ukatoliki; kwani Roma kamwe haibadiliki. Yeye hudai kuwa kamwe hakosei. Uprotestanti ndio utakaobadilika. Kuzikubali fikra za mabadiliko kutauleta hadi pahali ambapo waweza kuukumbatia mkono wa Ukatoliki." *Review and Herald*, June 1, 1886.

Kabla ya sheria ya Jumapili "kutekelezwa kikamilifu," huku Marekani ikisonga zaidi karibu na Ukatoliki na mbali zaidi na urithi wake wa Kiprotestanti, ile kinga ya Mungu, ambayo kanuni za Uprotestanti zililipatia taifa hili, itakuwa imeondolewa. Kuondolewa kwa fadhila za Mungu kutaleta majanga na taabu kulingana na upungufu wa umbali kati ya Marekani na Ukatoliki. Taabu hizi zitachangia mateso mwanzoni, ambayo kwa upande wake, yatachangia kugawanyika kwa watu wa Mungu.

> "Itatangazwa kuwa watu wanamuudhi Mungu kwa kuikiuka sabato-Jumapili; ya kuwa dhambi hii imeleta **shida ambazo hazitaisha hadi** utunzaji wa Jumapili **ulazimishwe kikamilifu**; na kuwa wale wanaohubiri kuhusu madai ya amri ya nne, hivyo kuiharibu heshima ya Jumapili, wanawasumbua watu, na kuwazuilia **wasirejeshewe fadhila za Mungu na usitawi wa kimaisha**. Hivyo lile shitaka lililosukumwa hapo kale dhidi ya mtumishi wa Mungu litarudiwa kwa kuzitumia sababu sawa na hizo ambazo zilikuwa zimeimarishwa vilivyo." *The Great Controversy*, 590.

Watu wa nchi hii watatamani "kurejeshwa kwa fadhila za Mungu na usitawi wa kimaisha." Hamu yao ya kuurejelea "usitawi" yadhihirisha kuwa majonzi ya kiuchumi yatakuwepo kabla ya sheria ya Jumapili.

> "Pesa hizo hizo zinazowekezwa kwa unyimifu katika kazi ya Mungu, na ambazo zinashikiliwa kwa ubinafsi, baada ya muda usio mrefu, zitatupiwa fuko na popo, pamoja na miungu mingine yote. Hivi karibuni thamani ya pesa itapunguka ghafla pale ukweli wa matukio ya milele utafunguka kwenye hisia za mwanadamu." *Welfare Ministry*, 266.

Kuongezeka kwa kuyumbayumba kwa uchumi pamoja na ongezeko la majanga kutachangia madai ya utunzaji wa Jumapili, huku pia wakiyazidisha mateso ya watu wa Mungu, hivyo kuwagawanya hata zaidi watu wa Mungu. Ndipo kazi yetu ya kuwaonya watu itazuiliwa na mateso, masaibu ya kiuchumi, ongezeko la majanga na uasi kutoka kusanyiko letu:

> "Kazi ambayo kanisa limekosa kuitenda wakati wa amani na usitawi litalazimika kuifanya wakati wa hatari ya kutisha katika hali ya kufisha moyo. Maonyo yalionyamazishwa kwa sababu ya kufanana na ulimwengu, au kushikiliwa, sharti yapeanwe chini ya upinzani mkali kutoka kwa maadui wa imani. Na wakati huo wale watu wa juu juu, kundi la wasiopenda mabadiliko, ambao ushawishi wao umeikwamisha kazi, wataikana imani na kusimama pamoja na maadui wazi wa imani, ambao wamekuwa wakiwaunga mkono kwa muda mrefu." *Testimonies*, volume 5, 463.

MCHUJO

Shughuli hii ya kutenganisha yaitwa "mchujo." Mchujo huu utaimaliza kazi ya Mungu wakati itakapo pitishwa sheria ya kitaifa ya Jumapili nchini Marekani, kisha kusambaa kwa wakazi wa ulimwengu. Sheria ya Jumapili ni mstari wa kikomo kwa wale wanaokiri kuwa Waadventista wa Siku ya Saba, lakini pia ni mstari wa kuanzia kwa mchujo kuhama kutoka kwa Uadventista hadi ulimwenguni. Suala la Sabato dhidi ya utakatifu wa Jumapili litaubuni mstari wa utengano kati ya wale watiifu na wasiotii hapa ulimwenguni.

> "Sabato itakuwa jaribu la uaminifu, kwa maana ndicho kipengele cha ukweli hasa kinachopiganiwa. Wakati jaribu la mwisho litakapoletwa kuhusiana na wanadamu, ndipo **mstari wa kutofautisha utakapochorwa** kati ya wale wanaomtumikia Mungu na wale wasiomtumika. Wakati utunjzaji wa sabato ya uongo katika kuridhia sheria ya serikali, ni kinyume na amri ya nne, itakuwa ni kukubali utii kwa mamalaka inayopingana na na Mungu, utunzaji wa Sabato ya kweli, katika kutii sheria ya Mungu, ni Ushahidi wa uaminifu kwa Muumbaji. Wakati kundi moja, kwa kukubali ishara ya utii kwa mamlaka za dunia, linapokea chapa ya mnyama, kundi linguine linachagua ishara ya utii kwa mamlaka ya mbinguni, linapokea Muhuri wa Mungu." *The Great Controversy*, 605.

KUONYESHA UWEZO UNAOHITAJIKA

Huku mateso yakizidi, wale ambao wameukiri ukweli tu, bila ya kuwa na ujuzi wake, wataendelea kulitoroka kusanyiko la Uadventista. Wakati huo wale ambao wameukiri na pia kuwa na ujuzi wa kweli watakuwa na ari zaidi kadiri ya uasi ulioko ulimwenguni na kanisani:

"**Wakati** sheria ya Mungu inabatilishwa, wakati jina Lake linapuuzwa, **wakati** utunzaji wa Sabato unachukuliwa kama uvunjaji wa sheria za nchi, **wakati** mbwa mwitu waliovalia ngozi za kondoo, kwa upofu wa akili zao na ugumu wa mioyo yao, wanajitahidi kuilazimisha dhamiri, je, sisi nasi tutauacha utiifu wetu kwa Mungu? La, la hasha. Mtu mwovu amejawa na chuki dhidi ya wale wanaozitii amri za Mungu, lakini thamani ya sheria za Mungu kama kanuni ya kuzielekeza tabia sharti idhihirishwe. **Ari ya wale wanaomtii Bwana itazidishwa kadri ulimwengu na kanisa wanaposhirikiana ili kuibatilisha sheria.** Wao watasema pamoja na Mtunga Zaburi, 'Mimi nazipenda amri zako zaidi ya dhahabu; naam, zaidi ya dhahabu safi.' Zaburi 119:127. Hili ni jambo ambalo lina hakika kutendeka pale sheria ya Mungu itakapopuuzwa kwa amri ya kitaifa. **Wakati** Jumapili itainuliwa na kudumishwa kwa sheria, **ndipo ile kanuni inayowaongoza watu wa Mungu itadhihirika**, jinsi kanuni ya wale Waebrania watatu ilivyodhihirika pale Nebuchadnezzar alipowaamuru kuiabudu ile sanamu ya dhahabu katika uwanda wa Dura. Tutaona jukumu ni lipi wakati kweli itatiishwa na uwongo." *Manuscript Releases*, vol. 13, 71.

WAKATI WA HUKUMU ZA UHARIBIFU

Mgawanyiko wa watu wa Mungu ambao "humnpoyoka" yule "mfalme wa kaskazini" na wale ambao "huangamizwa" naye, hufikia kilele chake pale sheria ya Mungu inapobatilishwa "kwa namna maalum." Kitendo hiki cha uasi wa kitaifa hufuatiwa na uangamiaji wa kitaifa huku hukumu za uharibifu za Mungu zikimwagwa:

"**Wakati** unakuja ambapo sheria ya Mungu **kwa namna maalum** itabatilishwa nchini mwetu. Watawala wa nchi yetu watailazimisha sheria ya Jumapili kwa miswada ya bunge, na hivyo watu wa Mungu watajipata kwenye hatari kuu. **Wakati** taifa letu, katika vikao vyake vya bunge, litazipitisha sheria za kuzifunga dhamiri za watu kuhusu haki zao za kidini, kwa kulazimisha utunzaji wa Jumapili, na kuwadhulumu wale waitunzayo Sabato ya siku ya saba, sheria ya Mungu, kwa makusudi yote, itabatilishwa nchini mwetu; nao **uasi wa kitaifa utafuatiwa na maangamizo ya kitaifa.**" *Review and Herald*, December 18, 1888.

"Waprotestanti watawashawishi watawala wa nchi wabuni sheria za kuyarejesha mamlaka ya yule mtu wa dhambi, anayeketi hekaluni mwa Mungu, akijifanya kuwa yeye ndiye Mungu. Kanuni za Ukatoliki wa Roma zitalindwa na serikali. Uasi huu wa kitaifa utafuatiwa upesi na uangamizaji wa kitaifa. Upinzani kutoka kwa ukweli wa Biblia hautavumiliwa tena na wale ambao hawajafanya sheria ya Mungu desturi ya maisha yao." *Review and Herald*, June 15, Juni 15, 1597.

MLANGO ULIOFUNGWA

Wakati sheria ya Jumapili itakapotekelezwa, "maangamizo ya kitaifa" yatafuata "upesi" nyuma yake. Wakati huu wa "hukumu za uharibifu" utafuata kufungwa kwa rehema kwa Waadventista Wasabato nchini Marekani.

"Wengi wanaojua ukweli wameipotosha njia yao mbele za Mungu na kuondoka kwenye imani. Mapengo waliyoyaacha yatajazwa na wale wanaowakilishwa na Kristo kama waliokuja saa kumi na moja. Kunao wengi ambao Roho wa Mungu anawasihi. Wakati wa hukumu za uharibifu za Mungu ni wakati wa rehema kwa wale wasio na nafasi ya kujua ukweli. Bwana atawatazama kwa upendo. Moyo wake wa huruma umeguswa; mkono wake ungali bado umenyoshwa ili aokoe, huku mlango ukifungwa kwa wale waliokataa kuingia. Watu wengi watakubaliwa kuingia ambao wanausikia ukweli kwa mara ya kwanza siku hizi za mwisho." *This Day With God*, 163.

Wale walioko Babeli "ambao Roho wa Mungu anajitahidi kuwashawishi," wataitikia ujumbe wa kilio kikuu na kuzichukuwa nafasi za wale Waadventista ambao "wameipotosha njia yao mbele za Mungu". Kwa wale walioipotosha njia yao, wakati wa "maangamizo ya kitaifa" utakuwa ni "wakati wa hukumu za uharibifu za Mungu," huku kwa wale wasiokuwa na nafasi ya kuujua ukweli," utakuwa ni wakati wa rehema." Wakati wa rehema na wakati wa hukumu utaamuriwa na iwapo sisi binafsi tutaikubali nuru iliyoletwa kwetu.

YALE AMBAYO WANGEYATENDA

Waadventista wa Siku ya Saba, zaidi ya watu wengineo wote, watakuwa bila udhuru kwa kutoishikilia Sabato pale sheria ya Jumapili itakapotekelezwa, kwani hatuhukumiwi tu kwa yale tunayoyajua, bali pia kwa yale ambayo tungeyajua kama tungejiwasilisha kwa kila nafasi ya kuelimika:

"Adhabu ya **wale ambao wamekuwa na nafasi nyingi ya kuujua ukweli**, lakini ambao kwa sababu ya upofu na kutoamini wamekuwa wakimpinga Mungu na wajumbe Wake, itakuwa kadri ya nuru waliyoikataa. **Mungu aliwapendelea sana**, huku akiwapatia manufaa ya kipekee na vipaji, ili waiachilie nuru yao iangaze kwa wengine. Lakini katika upotovu wao waliwaongoza wengine mbali na njia. **Mungu atawahukumu kwa sababu ya wema ambao wangeufanya, lakini hawakuufanya**. Atawaita ili watoe hesabu ya nafasi **walizokosa kuzitumia**. Waligeuka kutoka kwenye njia ya Mungu na kuifuata njia yao wenyewe, nao watahukumiwa sawa sawa na matendo yao. Kwa kuenenda kinyume na kanuni za ukweli, walimwaibisha Mungu. Walikuwa wajinga machoni Pake kwa kugeuza ukweli Wake kuwa uwongo. Jinsi walivyokuwa wametofautishwa kwa neema walizokirimiwa, vivyo hivyo watatofautishwa kwa ukali wa adhabu yao." *Review and Herald*, June 25, 1901.

Huku suala hili likipitia ndani ya Uadventista na kwenda ulimwenguni, masharti ya majaribio sawa na yale yaliyotumika juu ya Waadventista yatatumika pia juu ya wale walioko ulimwenguni. Jaribio hilo litaamuliwa na iwapo tutaitikia ukweli baada ya kuarifiwa kuhusu masuala hayo. Kuipokea "alama ya mnyama kwahitaji uchaguzi baada ya kuarifiwa kuhusu Sabato. Soma *The Great Controversy*, 449.

Hakuna atakayeipokea "alama ya mnyama," hadi "suala hilo liwasilishwe mbele yao kwa njia dhahiri." Suala hilo liliwahi kuwekwa wazi mbele ya Waadventista Wasabato muda mrefu kabla ya sheria ya Jumapili. Wao "wameelimishwa kuhusu jukumu lao la kuitunza Sabato ya kweli," hivyo basi kwao "kuivunja amri ya Mungu," na "kulitii agizo litokalo kwenye mamlaka yasiyo juu zaidi ya yale ya Roma," ni "kuyatambua mamlaka" ya Upapa, kuipokea alama ya mnyama, na kujifungia muda wa rehema.

UTOROKAJI MKUU

Katika aya ya arobaini na moja, twawaona wale ambao "huokoka toka mkononi mwake." Ndani ya kirai hiki, neno "mkono" ni ishara ya kiunabii inayoonyesha uwezo na mamlaka yitumikayo na mshindaji.

> BWANA asema hivi, Tazama, Nitamtia Farao Hofra, mfalme wa Misri katika mikono ya adui zake, na katika mikono ya wao wamtafutao roho yake; kama vile nilivyomtia Sedekia, mfalme wa Yuda katika mikono ya Nebukadreza mfalme wa Babeli, adui yake aliyemtafuta roho yake. Yeremia 44:30. Soma pia Zekaria 11:6.

Wakati "mfalme wa kaskazini" ataingia ndani ya ile "nchi ya uzuri," wapo baadhi ya watu ambao watauponyoka mkono wake na wengine ambao wataangamizwa. Neno hili "mkono," hutumika kuwakilisha uwezo na mamlaka yanayotumiwa na Upapa pale uingiapo ndani ya Marekani na kuwaangamiza wengi. Mamlaka ya Upapa ni utunzaji wa Jumapili:

> "Kama ishara ya mamlaka ya Kanisa Katoliki, waandishi wa Katoliki wanatoa dondoo kwamba 'tendo halisi la kubadilisha sabato kuwa Jumapili, ambayo Waprotestanti wanaikiri na kuitambua;… kwa sababu kwa kushika Jumapili, wanatambua na kukiri mamlaka ya kanisa ya kuamuru sikukuu, na kuwahukumu kuwa na hatia' —Henry Tuberville, *An Abridgment of the Christian Doctrine,* page. 58. Kwa hiyo sasa badiliko la sabato ni la nini, ni ishara au chapa ya mamlaka ya kanisa la Romani – 'chapa ya mnyama'?" *The Great Controversy,* 448.

> "'Ishara, au muhuri, wa Mungu hufunuliwa ndani ya utunzaji wa Sabato ya siku ya saba, yaani kumbukumbu ya uumbaji wa Mungu …. Alama ya mnyama ni kinyume cha haya – utunzaji wa siku ya kwanza ya juma. Alama hii huwatofautisha wale wanaoutambua ukuu wa mamlaka ya upapa kutoka kwa wale wanayoyatambua mamlaka ya Mungu.'" *Testimonies,* volume 8, 117.

Wakati Danieli 11:41 inaeleweka katika muktadha huu, matumizi ya Danieli ya neno "mkono," huwakilisha kule kutwaa kwa mamlaka ya kiroho nchini Marekani na Upapa baada ya kupitishwa kwa sheria ya Jumapili. Ushuhuda wa Yohana katika Ufunuo 13:16 ya kuwa "wote" wataipokea chapa ya mnyama kwa "mkono wa kuume" pia hutumia mkono kuutambulisha alama ya mamlaka ya Upapa. Kutekelezwa kwa sheria ya Jumapili huashiriwa na kuja kwa Marekani kwenye "mkono" wa Upapa katika Danieli 11:41. Ni wakati wa kupitishwa kwa sheria ya Jumapili ambapo wale watakaotoroka, watauponyoka mkono wake, kwani hadi wakati huo, halitakuwa jambo la kisheria.

Wakati Uprotestanti utashikana mikono na Ukatoliki, itakuwa kwa hakika ni kusalimisha mamlaka yake ya kiroho kwa Upapa. Matumizi ya kiishara ya neno mkono, na mwendo au kutembea kwa yule "mfalme wa kaskazini" hutumika pia na Roho wa Unabii kuyazungumzia masuala haya yanayofanana na pia vipindi. Hebu tazama jinsi neno hili "mkono" lilivyotumika:

> "Wakati taifa letu litazikana kanuni za serikali yake hata kuipitisha sheria ya Jumapili, ndipo kwa tendo hili Uprotestanti utashikana mikono na upapa." *Testimonies,* volume 5, 712.

> "Uprotestanti ndio utakao badilika. Kule kuzikubali fikra za mabadiliko kwa upande wake kutauleta mahali ambapo **utaweza kuushika mkono wa Ukatoliki**." *Review and Herald,* June 1, 1886.

> "Waprotestanti wa Marekani watakuwa wa kwanza kuunyosha mkono wao kuvuka ng'ambo ya ghuba na kuushika mkono wa uchawi; wote wawili watavuka ng'ambo ya lindi kuu na kushikana mikono na utawala wa Roma; na chini ya ushawishi wa muungano huu wa hao watatu, nchi hii itazifuata nyayo za Roma katika kuzikanyagia chini haki za jinsia." *The Great Controversy,* 588.

> Je! Watu wawili hutembea pamoja wasipokubaliana kufanya hivyo? Amosi 3:3.

Dada White atumia "mkono" sio tu kuashiria wakati ambapo mamlaka ya Roma yanadumishwa Marekani kwa kuitekeleza sheria ya Jumapili, bali pia auonyesha Upapa wakati huu wa historia kama wenye ushindi wa kiroho. Danieli aelezea jinsi "mfalme wa kaskazini" hutembea kupitia Muungano wa Sovieti, kisha kuingia Marekani, na kisha kwenda ulimwenguni kote. Dada White pia aelezea matukio haya kama mwendo pale anaposema, "nchi hii itafuata nyayo za Roma katika kuzikanyagia chini haki za kuabudu."

Edomu, Moabu, na Amoni

Tena ataingia katika hiyo nchi ya uzuri, na *nchi* nyingi zitapinduliwa; lakini nchi hizi zitaokolewa na mkono wake, Edomu, na Moabu, na wakuu wa watu wa Amoni." Danieli 11:41.

Katika sura mbili zilizopita tuliitambulisha "nchi ya uzuri" ya Danieli 11:41 kama Marekani, na pia tukaona kuwa wakati Upapa, unaoashiriwa na "mfalme wa kaskazini", utaingia Marekani, watu wengi watapinduliwa huku wengine wakitoroka toka "mkononi mwake." Wale watakaopinduliwa **watashikana mikono** na Upapa, kuashiria kukubaliana na mamlaka ya kiroho ya utawala wa Papa, ambayo hufanyika pale "mfalme wa kaskazini" "anapoingia" kwenye "nchi tukufu" kwa njia ya kupitishwa kwa sheria ya kitaifa ya Jumapili nchini Marekani.

Mwendo wa Kusonga Mbele

Katika sura iliyopita tuliielezea aya hii kama inayoonyesha uendeleaji wa matukio yanayokunjuka huku suala la sheria ya Jumapili likitekelezwa Marekani. Matukio na masuala haya yanapoendelea kwa muda, yatazidi, huku yakiuchapuza ule "mtikiso." Mtikiso huo wa Uadventista utapelekea kusafishwa kwa mwisho kwa Kanisa la Waadventista Wasabato. Usafishaji huu utasababishwa na uasi wa Waadventista ambao hawakuileta "kweli" ndani ya ujuzi wao binafsi, na hivyo hawakuwa wamejiandaa kusimama dhidi ya mateso yaliyoletwa dhidi ya watu wa Mungu kuhusu suala la Sabato. Wakati huu ushawishi na mamlaka ya Upapa huzidi kuongezeka huku ukiendeleza ushindi wake wa kiroho juu ya ulimwengu kabla ya kumalizia kwenye uharibifu.

Katika kipindi hiki watu wa Mungu husafishwa, hivyo kuruhusu kunyesha kwa mvua ya masika, ambayo itawawezesha watu wa Mungu kusimama wakati wa taabu, na vilevile kuuhubiri ujumbe wa onyo la mwisho. Ujumbe huo wa onyo la mwisho ndio ujumbe wa "kilio kikuu," nao pia huzidi kuongezeka unaposonga ulimwenguni.

> "Neno la Mungu katika sheria Yake ni lazima kutiiwa na kila mtu mwenye akili. Ukweli wa wakati huu, yaani ujumbe wa malaika wa tatu, utatangazwa kwa sauti kuu, **maana yake, kwa nguvu zaidi**, tunapolikaribia jaribio kuu la mwisho." *Ellen G. White 1888 Materials*, 1710.

Kuitoroka Nchi Yao ya Asili

Wakati raia wanapokuwa wakimbizi kutoka kwa serikali onevu, wao huitoroka nchi yao ya asili, ijapokuwa bado huakisi uraia wao mahsusi. Wale watu wa Vietnam waliokuwa ndani ya ile mashua walikuwa wakimbizi, lakini walikuwa bado ni raia wa Vietnam.

Vivyo hivyo, tutawaona Edomu, Moabu na Amoni wakiwawakilisha wale "wakimbizi" wanaotoka Babeli wakati wa ujumbe wa kilio kikuu, hivyo kuuakisi mgawanyiko katika sehemu tatu wa Babeli ya kisasa.

Tunapoanza kujadili Edomu, Moabu na Amoni, sharti tutambue ya kuwa pahala pao katika mfululizo wa matukio ni mwanzo kabisa wa kipindi cha kilio-kikuu, mara tu baada ya sheria ya Jumapili kutekelezwa Marekani. Wakati huo, twawaona Edomu, Moabu na Amoni wakielezewa kama wale ambao "huponyoka" toka mkononi mwa Upapa.

Neno linalotafsiriwa hapa kama "kuponyoka" humaanisha kutoroka "kama vile kwa kuteleza," ama pia "**kuachilia au kuokolewa.**" Ufafanuzi huu wadokeza kuwa kabla ya kuponyoka huko kwao, makabila haya matatu yalikuwa mkononi mwa Upapa. Ujumbe ambao watu wa Mungu wanautangaza katika kipindi hiki ni wito wa kuikimbia Babeli; nazo Edomu, Moabu na Amoni zaashiria wale watu watakaoanza kuukubali ujumbe huo wa mwisho wa Ufunuo 18:4, "Tokeni kwake, enyi watu wangu."

> "Kuhusu Babeli **wakati huu** imetangazwa, 'Dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Mungu amekumbuka maovu yake.' Ufunuo 18:5. Amejaza kipimo cha hatia yake, nao uharibifu u karibu kumshukia. Lakini **Mungu angali bado anao watu ndani ya Babeli**; na kabla ya kuzitekeleza hukumu zake, **watu hao waaminifu** sharti **waitwe ili waondoke**, wasije 'wakashiriki dhambi zake, na kuyapokea mapigo yake.' Huo ndio mwendo unaoashiriwa na malaika anayeshuka kutoka mbingni, akiiangaza dunia kwa utukufu wake, na kulia kwa nguvu kwa sauti kuu, huku akizitangaza dhambi za Babeli. Kuhusiana na ujumbe huu, wito unasikika, **'Tokeni kwake, enyi watu wangu.'** Maonyo haya yanapoungana na ujumbe wa malaika wa tatu, huzidi na kuwa kilio kikuu." *The Spirit of Prophecy*, vol. 4, 422.

Makabila haya matatu ya kiishara ambayo huukubali mwito wa kutoka Babeli, na hivyo kuponyoka mkononi mwa Upapa, vilevile yanawakilishwa na wale "kondoo wengine" ambao Kristo aliahidi kuwaita:

> Na **kondoo wengine** ninao, ambao **sio wa zizi hili**; na hao nao imenipasa kuwaleta; na **sauti yangu wataisikia**; kisha kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja. Yohana 10:16.

Kielelezo kifuatacho cha Kristo kuhusu "siku atakapofunuliwa Mwana wa adamu," kinao ufahamu wa makabila haya:

> Lakini siku ile **Lutu aliyotoka Sodoma** kulinyesha moto na kibiriti kutoka mbinguni vikawaangamiza wote. Hivyo ndivyo itakavyokuwa siku ile atakayofunuliwa Mwana wa Adamu. Luka 17:29-30.

Dada White huangazia nuru zaidi juu ya fungu lililopita pale anapokielezea kipindi hicho cha kilio-kikuu:

"Watumishi wa Mungu, waliojaliwa na uwezo kutoka juu, wenye nyuso angavu, na zinazong'aa kwa wakfu mtakatifu, waliondoka ili kuutangaza ujumbe kutoka Mbinguni. **Watu waliotapakaa kote makanisani** waliukubali **mwito huo**, nao watu hao wa thamani wakaharakishwa **watoke kwenye makanisa hayo yaliyohukumiwa kifo, jinsi Lutu** alivyoharakishwa **kuondoka Sodoma** kabla ya kuangamizwa kwake." *Early Writings*, 278–279.

Kristo alitaja Sodoma na kule **kuponyoka** kwa Lutu kama kielelezo cha mwisho wa ulimwengu, naye dada White humtambulisha Lutu kama mfano wa wale watakaoyaacha "makundi ya kidini" katika kipindi cha kilio-kikuu. Twawaona Kristo na Dada White wakiutumia uzao wa Lutu kama mfano wa hao "kondoo wengine" ambao wataukubali ujumbe wa onyo la mwisho. Kwa kukubaliana na mafungu haya, Danieli 11:41 huyatumia makabila yayo hayo inapotambulisha Moabu na Amoni, kwani makabila haya ni uzao wa Lutu.

Dada White asema kuwa yeye aliona "kikundi baada ya kikundi katika jeshi la Bwana wakijiunga na adui," na kisha "**kabila baada ya kabila** kutoka kwenye kikosi cha adui wakaungana na watu wa Mungu wazishikao amri." Makabila haya matatu hutoka kwenye "makanisa yaliyohukumiwa kifo," vilevile kutoka kwenye "kikosi cha adui."

"Katika njozi, niliviona vikosi viwili vikiwa katika pambano la kutisha. Kikosi kimoja kiliibeba bendera yenye nembo ya ulimwengu; cha pili kikawa kimeongozwa na bendera ya Mfalme Imanueli iliyolowa damu. Bendera baada ya bendera iliachwa kutambaa mavumbini huku kikundi baada ya kikundi kutoka kwenye jeshi la Bwana wakijiunga na adui, na **kabila baada ya kabila kutoka kwenye kikosi cha adui wakiungana na watu wa Mungu wazishikao amri.**" *Testimonies*, volume 8, 41.

Twaona katika makabila haya matatu kielelezo cha wale washiriki wanaoukubali ujumbe wa kilio-kikuu. Makabila haya ni wale wanaotoroka kutoka Babeli. Hapo awali, makabila haya yalikuwa, kama ishara, yamekamatwa na Babeli ya kisasa, lakini baada ya masuala kufafanuliwa, wanaukubali mwito wa kuondoka. Hawa ndio wale "kondoo wengine," ama wale "watoto wengine wa Bwana waliosalia Babeli," ambao Bwana atawaita waondoke katika kipindi cha mvua ya masika.

"**Wakati** wale 'ambao hawakuiamini kweli, bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu' (Wathesaloniki 2:12) wataachwa ili kuipokea nguvu ya upotevu, wauamini uongo, **ndipo** nuru ya kweli itang'aa juu ya wote ambao mioyo yao imefunguka ili kuipokea, nao **watoto wote wa Mungu waliosalia Babeli** wataukubali mwito: 'Tokeni kwake, enyi watu wangu.' Ufunuo 18:4" *Maranatha*, 173.

HISTORIA YA CHUKI NA UPINZANI

Ili kutambua ni nani au ni nini kinachoashiriwa na makabila haya matatu, sharti tuitumie ile kanuni ya kinabii ambayo tuliitumia hapo awali katika mfululizo huu, inayohitaji kwamba tujaribu kuelewa Edomu, Moabu na Amoni kama makabila ya kiroho, wala sio ya kihalisia. Katika unabii, ili kuyaelewa matumizi ya kisasa, sharti kwanza tuyaelewe matumizi ya kale ya kihalisia, na kwa kufanya hivyo, kuendeleza msingi wa habari zitakayoyasimamisha matumizi ya kiroho.

Edomu humaanisha "nyekundu," nalo ni jina lingine la Esau na uzao wake:

Esau akamwambia Yakobo, "Haraka, nipe huo mchuzi mwekundu! Nina njaa kali sana!'' (Hii ndiyo sababu pia aliitwa Edomu.) Yakobo akamjibu, "Niuzie kwanza haki yako ya mzaliwa wa kwanza.'' Esau akasema, "Tazama, mimi niko karibu kufa, itanifaa nini haki ya mzaliwa wa kwanza?'' Yakobo akamwambia, "Niapie kwanza.'' Hivyo Esau akamwapia, akamwuzia Yakobo haki yake ya kuzaliwa. Ndipo Yakobo akampa Esau mkate na ule mchuzi wa dengu. Akala na kunywa, kisha akainuka akaenda zake. Kwa hiyo Esau alidharau haki yake ya mzaliwa wa kwanza. Mwanzo 25:30-34.

Asiwepo mwasherati wala asiyemcha Mungu, kama Esau, aliyeuuza urithi wake wa mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya chakula kimoja. Maana mwajua ya kuwa hata alipotaka baadaye kuirithi baraka, alikataliwa (maana hakuona nafasi ya kutubu), ijapokuwa aliitafuta sana kwa machozi. Waebrania 12:16-17.

Kabila la Edomu lilikuwa ni kakake Israeli. Esau alikuwa ni mwasherati mkufuru ambaye aliukataa urithi wake ili afuate anasa za ulimwengu huu. Moabu humaanisha "amu," nalo ni kabila lililotokana na kujamiiana kwa maharimu baina ya Lutu na binti yake mdogo.

Hivyo binti wawili wa Loti wakapata mimba kwa baba yao. Binti mkubwa akamzaa mwana, akamwita jina lake Moabu, ndio baba wa Wamoabu hata leo. Binti mdogo naye pia akamzaa mwana, naye akamwita Benami ndiye baba wa Waamoni hata leo. Mwanzo 19:36-38.

Twaona kuwa makabila yale matatu ya Danieli 11:41 ni jamaa wa kiroho wa karibu na Israeli ya kiroho, nao hubainishwa kwa tendo la uasherati au kujamiiana kwa maharimu, hivyo kutambulisha kujihusisha kwao na uhusiano usio halali – sifa bainifu ya Babeli ya kisasa. Historia ya makabila haya ya kale huitambulisha ile chuki ya jadi na upinzani dhidi ya kazi ya watu wa Mungu, kielelezo kuwa makabila haya ya kisasa na ya kiroho yangeipinga kiroho kazi ya watu wa Mungu wa kisasa.

Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: ‘Kwa sababu **Edomu ulilipiza kisasi juu ya nyumba ya Yuda** na kukosa sana kwa kufanya hivyo. Ezekieli 25:12.

Nimeyasikia **matukano ya Moabu nazo dhihaka za Waamoni,** ambao waliwatukana watu wangu na kufanya vitisho dhidi ya nchi yao. Hakika, kama niishivyo,” asema BWANA Mwenye Nguvu zote, Mungu wa Israeli, “Hakika Moabu itakuwa kama Sodoma, Waamori kama Wagomora, mahali pa magugu na mashimo ya chumvi, nchi ya ukiwa milele. Mabaki ya watu wangu **watawateka nyara**, **mabaki ya taifa langu watarithi nchi yao**.’’ Hiki ndicho watarudishiwa kwa ajili ya kiburi chao, kwa **kutukana na kudhihaki watu wa BWANA Mwenye Nguvu zote**. Sefania 2:8-10.

Fahamu kuwa ilikuwa imetabiriwa ya kuwa masalio wa Mungu hawangewateka tu, bali pia wangewamiliki. Hapo zamani za kale makabila haya matatu yaliwapinga watu wa Mungu, nayo ibada yao bandia ikawa daima ni mtego kwao. Zamani zile, Edomu, Moabu na Amoni, japo walikuwa ni jamaa wa karibu kwa Israeli, walikuwa ni maadui wa watu wa Mungu, huku wakiendeleza ibada bandia kinyume na ibada ya kweli ya Mungu. Uhusiano wao na upinzani wao dhidi ya Israeli ya kale kulipelekea Mungu kutofautisha kwa namna maalum kuhusu kukubaliwa kwao kwenye ibada halisi ya Mungu. Soma 1 Wafalme 11:5, 7; 2 Mambo ya Nyakati 25:14.

Hapatakuwa na **Mwamoni au Mmoabu** au yeyote wa wazao wao atakayeruhusiwa kuingia katika kusanyiko la BWANA, hata mpaka kizazi cha kumi. Kwa kuwa hawakuja kuwalaki wakiwa na mkate na maji mlipokuwa njiani mlipotoka Misri, tena walimwajiri Balaamu mwana wa Beori kutoka Pethori iliyoko Aramu Naharaimu ili kuwalaani ninyi. Hata hivyo, BWANA Mungu wenu hakumsikiliza Balaam bali aligeuza laana kuwa baraka kwenu kwa sababu BWANA Mungu wenu anawapenda. Msitafute mapatano ya urafiki nao maisha yenu yote. Usimchukie **Mwedomu**, kwa kuwa yeye ni ndugu yako. Usimchukie Mmisri, kwa sababu uliishi kama mgeni katika nchi yake. Kizazi cha tatu cha watoto watakaozaliwa nao wanaweza kuingia katika kusanyiko la BWANA. Kumbukumbu La Torati 23:3-8.

Dada White atuarifu kuwa Danieli na Ufunuo “hukamilishana.” Yakitazamwa kama kitu kimoja cha kuashiria, makabila hayo matatu huakisi ule mgawanyiko mara tatu wa Babeli ya kisasa, hivyo kukamilishana na maelezo ya Babeli ya kisasa yaliyoko kwenye kitabu cha Ufunuo.

BABELI NA MUUNGANO ULIO MARA TATU

Na yule **mwanamke** uliyemwona, ni **mji ule mkubwa**, wenye ufalme juu ya wafalme wa nchi. Ufunuo 17:18.

Katika unabii, “mji mkuu” huwakilisha ufalme. Soma Ufunuo 11:8; 21:10. Ujumbe wa malaika wa pili ni mwito wa kuondoka kwenye ufalme wa Babeli, kwani yatambulishwa kama “mji ule mkuu.”

Kisha mwingine, malaika wa pili, akafuata, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli, **mji ule ulio mkubwa**, maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake. Ufunuo 14:8.

Ufunuo huitambulisha asili hii ya mara tatu ya “mji mkuu,” (yaani ufalme wa Babeli):

Na **mji ule mkuu ukagawanyikana mafungu matatu**, na miji ya mataifa ikaanguka; na Babeli ule mkuu ukakumbukwa mbele za Mungu, kupewa kikombe cha mvinyo ya ghadhabu ya hasira yake. Ufunuo 16:19.

Nikaona roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura, zikitoka katika kinywa cha **yule joka**, na katika kinywa cha yule **mnyama**, na katika kinywa cha yule **nabii wa uongo**. Ufunuo 16:13.

Mpangilio huu ulio mara tatu wa Babeli ya kisasa hujumlisha yule joka, mnyama na nabii wa uwongo. Shirikisho hili mara tatu huunganishwa na uchawi, unaoashiriwa na yule joka; Ukatoliki, ukiashiriwa naye mnyama; na Uprotestanti ulioasi, ukiashiriwa na yule nabii wa uwongo. Uprotestanti hutimiza Ufunuo 13:11, na huongea kama joka kwa kuitunga sheria ya kitaifa ya Jumapili. Ni katika kipindi hiki basi ambapo nguvu hizi tatu chafu za kiroho hutambulishwa kuwa zinakuja pamoja ili kuunda muungano huo mara tatu.

“Kupitia amri hiyo ya kuitekeleza asasi hiyo ya Upapa kwa kuivunja sheria ya Mungu, **taifa letu litajitenganisha kabisa** na haki. Wakati Uprotestanti utaunyosha mkono wake ng’ambo ya ghuba na kuushika mkono wa utawala wa Roma, wakati atafikia juu ya lindi kuu na kushikana mikono na uchawi, wakati, chini ya ushawishi wa **muungano huu ulio mara tatu**, nchi yetu itaikana kila kanuni ya Katiba yake kama serikali ya Kiprotestanti na jamhuri, na kutoa nafasi ya kuenezwa kwa uwongo na udanganyifu wa kipapa, basi twaweza kujua ya kuwa wakati umewadia wa Shetani kufanya maajabu na kuwa mwisho umekaribia.” *Testimonies*, volume 5, 451.

Huku mamlaka hizi tatu zikiungana dhidi ya sheria za Mungu na watu Wake, hudhihirisha chuki na upinzani sawa na wenzao wa jadi kama ilivyoonyeshwa kwenye historia ya Edomu, Amoni na Moabu. Kwa hivyo makabila haya matatu huakisi mgawanyiko mara tatu wa Babeli ya kisasa, na pia kuwakilisha wale watu watakaoitoroka Babeli ya kisasa. Muungano huo mara tatu kati ya lile joka, mnyama na nabii wa uwongo, ambao hujumlisha ule mji mkuu wa Babeli, utakamilika rasmi wakati wa sheria ya Jumapili, wakati ambao Edomu, Moabu na Amoni wanaonyeshwa wakiponyoka toka mkononi mwa Upapa.

THIBITISHO LA MANABII

Kwa kukubaliana na Danieli na Ufunuo, unabii mwingi ndani ya Biblia unazoelezea matukio ya wakati wa mwisho husimulia kuhusu adui watatu wanaopingana na kazi ya Mungu na watu Wake:

Katika Hesabu 22, twaupata wazi usambamba wa kipindi cha mvua ya masika pale wana wa Israeli walikaribia kuingia ndani ya Nchi ya Ahadi. Kisha Moabu, Midiani na Balaamu wakainuka ili kuyapinga makusudio ya Mungu kwa watu Wake.

Katika hadithi ya enzi ya Nehemia, hadithi ambayo Dada White hutambulisha kama ya "kuashiria" kazi ambayo watu wa Mungu leo hii sharti waitekeleze, twampata Sanballat, Mmoabu; Tobia, Muamoni; na Geshem, Mwarabu, wakiinuka ili kuipinga kazi ya Mungu na watu Wake.

Katika historia ya ushindi wa Yehoshafati ipatikanayo 2 Mambo Ya Nyakati 20, twapata kielelezo cha ushindi wa mwisho wa watu wa Mungu pale Yehoshafati aingiapo kwenye pambano dhidi ya Edomu, Moabu, na Amoni, huku waimbaji wakiongoza katika mwendo huo.

Katika historia ya Gideoni ipatikanayo Waamuzi 6-8 twapata kielelezo chenye nguvu kuhusu hatua za mwisho za historia ya dunia, pale Gideoni afanyapo vita dhidi ya Midiani, uzao wa Ibrahimu; Amaleki, uzao wa Esau; na wana wa Mashariki.

Lakini mojawapo ya mafungu muhimu sana ya kinabii yanayowatambulisha maadui hao watatu hupatikana Isaya 11:10-15. Dada White afasiri aya za kwanza tatu katika fungu hili:

> "**Bwana MUNGU, akusanyaye waliofukuzwa katika Israeli** asema, Pamoja na hayo **nitamkusanyia na wengine, zaidi ya hao** walio wake waliokusanywa' Isaya 56:8.
>
> "'Tafuteni katika kitabu cha Bwana na mkasome;.' Isaya 34:16. 'Na itakuwa katika siku hiyo, shina la Yese lisimamalo kuwa **ishara** kwa kabila za watu, yeye ndiye ambaye mataifa watamtafuta; na mahali **pake pa kupumzikia** patakuwa na utukufu. Na itakuwa katika siku hiyo, **Bwana atapeleka mkono wake** mara ya pili, ili ajipatie watu wake watakaosalia, kutoka Ashuru, na kutoka Misri, na kutoka Pathrosi, na kutoka Kushi, na kutoka Elamu, na kutoka Shinari, na kutoka Hamathi, na kutoka visiwa vya bahari. Naye **atawatwekea mataifa bendera**, atawakutanisha watu wa Israeli waliotupwa, atawakusanya watu wa Yuda waliotawanyika, kutoka ncha nne za dunia.' Isaya 11:10-12.
>
> "**Maneno haya yanatoa muhtasari wa kazi yetu**. Andiko hili lapasa kupokelewa na watu wetu kama ujumbe wa sasa. **Habari za kufurahisha za wokovu zafaa kupelekwa kwa wale ambao hawajawahi kuzisikia.**" *Review and Herald*, June 23, 1904.
>
> Fungu hili katika Isaya laitambulisha kazi yetu kuhusiana na suala la Sabato, kwani bango humaanisha bendera au beramu: "bango – 5251: kutoka 5264; bendera; pia tanga; kwa matumzi mlingoti; kwa jumla selo; kitamathari ishara: – bendera, mlingoti, selo.
>
> "5264: kubuga kwa mbali, yaani kuonekana waziwazi kama ishara; kuinua kioleza: – kuinua kama bendera, mshika bendera." *Strong's*.
>
> Bendera hiyo au bango inayohusishwa na "kitabu cha sheria," na ambayo "itasimamishwa," ni Sabato: "Ni wakati huu ambapo **Sabato ya kweli sharti iletwe mbele ya watu** kwa njia ya kalamu na sauti. Huku amri ya nne ya zile Amri Kumi na wale waitunzao wakidharauliwa na kudhihakiwa, waaminifu walio wachache wanajua ya kuwa huu sio wakati wa kuzificha nyuso zao, bali wa **kuinua sheria ya Yehova kwa kuikunjua bendera** ambayo juu yake umeandikwa ujumbe wa malaika wa tatu, 'Hapa ndipo penye hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu.' Ufunuo 14:12. *Evangelism*, 281; soma pia *Testimonies*, volume 6, 352–353; na *Early Writings*, 74.
>
> Dada White vilevile afasiri juu ya aya ifuatayo katika unabii wa Isaya:
>
> Wivu wa Efraimu utatoweka, na adui wa Yuda watakatiliwa mbali, Efraimu hatamwonea Yuda wivu wala Yuda hatakuwa na uadui na Efraimu. Isaya 11:13.
>
> "Msalaba wa Kristo ni dhamana ya ushirika na muungano wetu. Sharti wakati ufike ambapo **walinzi watasikilizana**; wakati tarumbeta itatoa sauti fulani; wakati ambapo 'Ephraimu **ataacha kumwonea wivu** Yuda, naye Yuda **aache kumwuudhi** Ephraimu tena." *Review and Herald*, January 3, 1899.

Kwa hivyo twafahamu ya kuwa fungu hili laitambulisha kazi yetu kuhusiana na suala la Sabato. Pia latambulisha kipindi ambacho watu wa Mungu wataungana na kuzileta "habari njema za wokovu" "kwa wale ambao hawajawahi kuzisikia."

Aya inayofuata katika unabii wa Isaya huyatambulisha makabila hayo matatu yanayoponyoka kutoka mkononi mwa "mfalme wa kaskazini" katika unabii wa Danieli:

> Nao watashuka, watalirukia bega la Wafilisti upande wa magharibi; nao pamoja watawateka wana wa mashariki; watanyosha mkono juu ya Edomu na Moabu; na wana wa Amoni watawatii. Na Bwana atauangamiza kabisa ulimi wa bahari ya Misri; na kwa upepo wake uteketezao atatikisa mkono wake juu ya Mto, naye ataupiga, uwe vijito saba, na kuwavusha watu wenye viatu vikavu. Itakuwako njia kuu kwa mabaki ya watu wake watakaobaki, watokao Ashuru, kama vile ilivyokuwako kwa Israeli, katika siku ile waliyotoka katika nchi ya Misri. Isaya 11:14-16.

Suala linaloukabili ulimwengu wakati huu ni sheria ya Mungu, na tunawaona watu wa Mungu walioungana "wakiweka mikono yao juu ya Edomu, Moabu, na watoto wa Amoni." Makabila hayo matatu waliouponyoka mkono wa Upapa katika unabii wa Danieli, huja chini ya mkono au utawala wa watu wa Mungu na "kuwatii," kuashiria kuwa wamekubalia na utawala na mamlaka ambayo huwashawishi watu wa Mungu. Hivyo makabila haya matatu hawatekwi nyara tu, bali pia humilikiwa katika kuutimiza unabii wa Sefania 2:8-10, ambao tuliodondoa hapo awali.

> Naam, watu wa kabila nyingi na mataifa hodari watakuja Yerusalemu kumtafuta Bwana wa majeshi, na kuomba fadhili za Bwana. Bwana wa majeshi asema hivi, Siku hizo watu kumi, wa lugha zote za mataifa, wataushika upindo wa nguo yake yeye aliye Myahudi; naam, wataushika wakisema, Tutakwenda pamoja nanyi, kwa maana tumesikia kwamba Mungu yu pamoja nanyi. Zekaria 8:22-23.

Fungu hili humalizia kwa kielelezo cha ukombozi wa mwisho huku masalio wakiifuata "barabara kuu" iliyoandaliwa kwa sababu yao "kama ilivyokuwa kwa Israeli siku ile alipotoka nchi ya Misri."

Twawaona Edomu, Moabu, na Amoni hapa wakionyeshwa kuwa wakati wa mwisho kabisa wa mvua ya masika, kwani ukombozi wa mwisho ndilo onyesho linalofuata katika fungu hili la Isaya. Isaya atumia Edomu, Moabu na Amoni katika kuelezea kufungwa kwa ujumbe wa kilio-kikuu, huku makabila haya matatu katika Danieli 11:41 yakielezea mwanzo wa ujumbe wa kilio-kikuu. Ipo tofauti moja tu kati ya makabila haya matatu ya Danieli na Isaya. Tofauti hiyo ni kwamba katika Danieli twamwona "**mkuu wa** wana wa Amoni," na katika Isaya, ni "wana wa Amoni" tu.

Neno "mkuu" katika Danieli 11:41 lamaanisha "malimbuko", nalo hutokana na neno-mzizi linalomaanisha "mtikiso" Edomu, Moabu, na Amoni katika Danieli ndio **malimbuko** ya ujumbe wa kilio-kikuu ambao huanza kujiunga na watu wa Mungu wakati wa kuipitisha ile sheria ya Jumapili nchini Marekani, ambao pia ni wakati **mtikiso** unapohama kutoka kwa Uadventista hadi ulimwenguni. Wakati mvua ya masika inapoelezwa kuisha na Isaya, makabila yale matatu sio tena malimbuko, na kwa hivyo, hao sio tena "mkuu" wa wana wa Amoni.

Wakati tutayaelewa makabila haya matatu kama mfano katika Danieli wa ule mgawanyiko mara tatu wa Babeli ambayo imetambulishwa na Ufunuo, tutautambua uhusiano wenye nguvu kati ya vitabu hivi viwili vya unabii. Mapatano haya ndiyo tuliyoambiwa tuyatarajie tunapokuja kuvielewa vitabu hivi vya unabii "jinsi itupasavyo."

Danieli 11:41 hutoa habari kuhusu matukio ambayo yanazidi kusonga mbele. Matukio kama vile mtikiso, mateso, kusafishwa kwa watu wa Mungu, sheria ya Jumapili, na mvua ya masika. Iwapo ufahamu huu wa matukio ni kamili, je, si basi yapasa ujuzi wetu binafsi uendelee kadri ya nyakati tunazoziishi leo? Nguvu moja kuu katika kuelewa Danieli 11:40-45 ni matukio yanayotukia ulimwenguni mwetu leo. Bila shaka, twaweza kuziona ishara za nyakati zikikunjuka, ambazo zashuhudia kuwa masuala yanayoelezewa katika sura za mwisho kuhusu Danieli 11:41 yanazidi kukaribia sana kila kukicha.

> "Ijapokuwa akili za mwanadamu zimeendelea sana, yeye asije akadhania hata wakati mmoja ya kuwa hamna haja ya kuyachunguza maandiko kikamilifu na kwa mwendelezo ili kupata nuru zaidi. Sisi kama watu tumeitwa tuwe wanafunzi wa unabii kibinafsi." *Testimonies*, volume 5, 708.

Kurejea Kutoka kwa Wafu

Naye ataunyosha mkono wake juu ya nchi hizo, hata na nchi ya Misri haitaokoka. Lakini atakuwa na nguvu juu ya hazina za dhahabu na fedha, na juu ya vitu vyote vya Misri vyenye thamani; na Walibia na Wakushi watafuata nyayo zake. Danieli 11:42-43.

Hapo awali tulitambulisha matumizi ya kiunabii ya neno "mkono" kama kielelezo cha utawala ambao huuleta utawala mwingine chini ya mamlaka, ushawishi na udhibiti wake. Jinsi mfululizo wa matukio yanayoelezwa na Danieli 11:40-45 ulianzia aya ya arobaini, tulimwona "mfalme wa kaskazini" akimfagilia mbali "mfalme wa kusini." Kisha hupita katika nchi zilizokuwa sehemu ya milki ya mfalme huyo wa kusini. Tuliutambulisha ujumbe wa aya ya arobaini kama kuporomoka kwa Muungano wa Sovieti mnamo 1989, kupitia juhudi za pamoja za Upapa na Marekani. Aya ya arobaini yalitambulisha tukio kubwa la kihistoria ambalo lilitumika na Bwana kuutambulisha mwanzo wa aya za mwisho za Danieli kumi na moja. Ufalme wa kusini umefagiliwa mbali.

Katika Danieli 11:41 twaiona Marekani ikiletwa chini ya **utawala wa kiroho** wa Upapa, kupitia kwa ishara zitumikazo ndani ya aya hiyo. Hapo awali tulijadili lile fundisho la Dada White, ya kuwa "mengi katika historia" ya Danieli 11 "yatajirudia" huku aya za mwisho za sura hiyo zikitimia. Baadhi ya historia hizo yalikuwa ni matukio yaliyohusiana na kuinuka kwa Upapa, ambayo yalionyesha mwanzo wa Enzi za Giza. Kuinuka kwa Upapa ili kuutawala ulimwengu kulikuwa ni marudio ya historia, kwani Roma ya kikafiri iliyashinda **maeneo matatu ya kijiografia** ili ije kwa utawala wa ulimwengu, na vivyo hivyo, Upapa ulilazimika kuzing'oa **pembe tatu** kabla ya kupaa na kuutawala ulimwengu.

Roma ya kisasa yaonyeshwa **kwanza** ikilipiza kisasi na kuufagilia mbali ufalme wa kusini – yaani "ufalme" wa kumkana Mungu ambao ulilileta jeraha lake la kufisha mnamo 1798. Kisha kikwazo chake cha **pili** ni ile "nchi ya uzuri" ya Marekani. Kufuatia Marekani, twaona kikwazo cha **tatu** pale inapoileta "Misri," ama ulimwengu uliosalia, chini ya utawala wake wa kiroho, hivyo kukirejelea cheo chake cha zamani kama mtawala wa ulimwengu.

> "Vitabu vya Danieli na Ufunuo ni vya athari kuu kwetu, navyo vyafaa kusomwa kwa bidii." *Review and Herald*, June 21, 1898.

Roma ya kikafiri, Roma ya Kipapa ya Enzi za Giza, na Upapa wa leo, kila moja huvishinda vikwazo vitatu ili kukichukuwa kiti cha enzi cha ulimwengu. Japo historia hizi zaenda sambamba hasa kuhusu vikwazo hivyo, zinatofautiana kwa namna kadhaa. Roma ya kikafiri **kihalisi** ilikichukua kiti cha enzi cha ulimwengu ikitumia uhodari wake mwenyewe wa kijeshi. Roma ya Kipapa ya Enzi za Giza ilikinyakua kiti cha enzi cha dunia **kihalisi** pale ilipozishinda zile pembe tatu, japo ilifanya hivyo bila jeshi lake mwenyewe, badala yake waliyatumia majeshi yaliyojihami ya washirika wao. Baada ya pembe hizo tatu kuondolewa kihalisi, ndipo utumwa wa kiroho ukatekelezwa. Upapa wa leo utaushinda **kiroho** ufalme wa kusini, ile nchi tukufu na kisha Misri, japo matokeo halisi yatafuata.

Katika Danieli 11:41 Marekani itakuja chini ya utawala wa kiroho wa Upapa pale itakapoitunga sheria ya kitaifa ya Jumapili – alama ya mamlaka ya Upapa. Katika aya ya arobaini na moja utiifu huo wa Marekani unaowakilishwa na "mkono" unagusiwa kwa kuwatambulisha wale wanaouponyoka mkono wa Upapa.

KIKWAZO CHA MWISHO CHA MFALME WA KASKAZINI

Katika Danieli 11:42 twamuona "mfalme wa kaskazini" tena "akiunyosha mkono wake." Mara hii ni dhidi ya kikwazo chake cha mwisho, ambacho hutambulishwa kama "nchi nyingi" na "nchi ya Misri." "Nchi ya Misri" huashiria ulimwengu na chi zake zote.

"Kwa nini huwa ni jambo ngumu sana kuongoza maisha ya kujinyima na ya unyenyekevu? Kwa sababu wanaokiri kuwa Wakristo hawajaufia **ulimwengu**. Ni jambo rahisi kuishi baada ya kufa. Lakini wengi wanatamani liki na vitunguu vya Misri. Wanayo tabia ya kuvalia na kutenda kama ulimwengu iwezekanavyo na bado wataka kwenda mbinguni. Hao hupanda juu kwa kupitia njia nyingine. Hawaingii kupitia mlango mwembamba na njia nyembamba." *Testimonies*, volume 1, 131.

"Mimi hujawa na huzuni ninapowaza kuhusu hali yetu kama watu. Bwana hajatufungia mbingu, lakini mwendo wetu wa kuendelea kurudi nyuma umetutenganisha na Mungu. Kiburi, tamaa, na kupenda **ulimwengu** vimedumu moyoni bila kuogopa kutengwa au kuhukumiwa… Kanisa limegeuka nyuma na kuacha kumfuata Kristo Kiongozi wake, nalo linarudi nyuma upesi kuelekea **Misri** … Je, hatujakuwa tukiutafuta urafiki na kusifiwa na **ulimwengu** badala ya uwepo wa Kristo na ujuzi zaidi wa mapenzi Yake?" Ibid., volume 5, 217–218.

"Wengi hawapati nguvu, kwa sababu hawamwamini Mungu kupitia Neno lake. Wanaufuata **ulimwengu**. Kila siku huweka hema zao karibu zaidi na **Misri**, badala ya kupiga kambi mwendo wa siku moja tu karibu na Kanani ya mbinguni." *Signs of The Times*, March 6, 1884.

"Mapigo yaliyomwaga juu ya Misri wakati Mungu alipokuwa karibu kuikomboa Israeli yalikuwa sawa na yale ya kutisha kabisa na ya hukumu kubwa zitakazo mwagwa ulimwenguni muda mfupi kabla ya Ukombozi wa mwisho wa watu wa Mungu." *The Great Controversy*, 627–628.

"Bwana Mungu wa Israeli ataitekeleza hukumu yake juu ya miungu ya **ulimwengu huu**, kama alivyofanya juu ya miungu ya **Misri**." *Manuscript Releases*, volume 10, 240.

Muktadha wa fungu tunalolizingatia waonyesha kuwa hatua inayofuata ya Upapa, baada ya kuipitisha sheria ya Jumapili nchini Marekani, ni kuenda dhidi ya nchi zinazosalia za ulimwengu. Huu pia ndio mfululizo wa matukio ambao Roho wa Unabii anautambulisha:

"Kwa vile Marekani, nchi ya uhuru wa kuabudu, itashirikiana na Upapa katika kuilazimisha dhamiri na kuwashurutisha watu waiheshimu sabato bandia, watu wa kila nchi duniani **wataongozwa kuufuata mfano wake.**" *Testimonies*, volume 6, 18.

"Mataifa ya kigeni yatafuata mfano wa Marekani. Japo ndiyo itakayoongoza, hatari sawa na hiyo itawapata watu wetu katika sehemu zote ulimwenguni." Ibid., 395.

Sio tu kwamba Dada White anaushikilia mfululizo huu wa kushindwa kwa ulimwengu na Upapa, bali huu pia ndio mpangilio wa matukio katika Ufunuo kumi na tatu. Kwanza, kwa kuipitisha sheria ya kitaifa ya Jumapili, Marekani hunena "kama joka", na pia kuiunda sanamu ya mnyama:

Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa Mwana-Kondoo, akanena kama joka. Ufunuo 13:11.

Neno "akanena" huelezea kitendo cha serikali: "'Kunena' kwa taifa ni tendo la mamlaka zake za bunge na mahakama." *The Great Controversy*, 442.

"Sanamu ya mnyama" ni maelezo ya jinsi utawala wa kilimwengu hutumiwa kuilazimisha imani ya dini:

"**Wakati** makanisa ya nchi yetu, huku yakiungana katika sehemu za imani ambazo wanazishikilia kwa pamoja, yataishawishi serikali kuyatekeleza makataa yao na kuzihimili asasi zao, hapo ndipo Marekani ya Kiprotestanti itakuwa imeitengeneza sanamu ya uongozi wa Roma. *The Spirit of Prophecy*, volume 4, 278.

Mambo hayo mawili, yaani kunena kama joka na kuitengeneza sanamu ya mnyama yatafanyika rasmi wakati wa sheria ya kitaifa ya Jumapili. Yapo, bila shaka, matukio mengi yanayotuongoza hadi kwenye upeo wa tendo hili la uasi, lakini ni **baada** ya lile tukio la Ufunuo 13:11, ambapo Marekani itaulazimisha ulimwengu pia kuisimamisha sanamu ya mnyama:

Akiwaambia **wakaao juu ya dunia** kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi. Ufunuo 13:14.

Ulimwengu utaitengeneza sanamu yao wenyewe kwa mnyama, nayo Marekani itauwezesha. Kwa ufafanuzi, ili ulimwengu uisimamishe sanamu ya mnyama, na hivyo "kutekeleza" na "kuhimili" "makataa" ya "makanisa," sharti uwe na mfumo wa kilimwengu katika nafasi yake, kama vile Umoja wa Mataifa.

Akapewa kutia pumzi katika ile sanamu ya mnyama, hata ile sanamu ya mnyama inene, na kuwafanya hao wote wasioisujudu sanamu ya mnyama wauawe. Ufunuo 13:15.

KUDANGANYWA KUPITIA MIZIMU

Wakati Marekani itaipitisha ile sheria ya Jumapili, haitanena tu kama joka, bali pia itaisimamisha sanamu ya mnyama. **Baada** ya tendo hili, "nchi tukufu" ya Marekani itaudanganya ulimwengu mzima kupitia nguvu zake za mizimu ambayo ziliwahi kuhusishwa sana na historia ya Misri:

"Nilielekezwa nyuma kwa wana wa Israeli walipokuwa **Misri**. Niliona [kuwa] wakati Mungu alikuwa akifanya kazi kupitia Musa mbele ya Filauni, waganga nao walikuja na kusema kuwa wangetenda hivyo hivyo. Niliona kuwa **kazi sawa na hiyo** sasa inaendelea **ulimwenguni** na pia miongoni mwa makanisa, ifananayo na ile kazi ya wachawi wa kale." *Manuscript Releases*, volume 19, 129–130.

Kupitia udanganyifu huu, ulimwengu mzima utafanywa kuuabudu Upapa:

Naye awakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya mbele ya huyo mnyama. Ufunuo 13:14.

Utumwa wa kiroho unaoletwa hapa na Yohana unawakilishwa na Danieli katika aya ya arobaini na mbili pale "mfalme wa kaskazini anapounyosha "mkono" wake juu ya "nchi nyingi" za "Misri."

Wakati Marekani "aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza, ambaye jeraha lake la mauti lilipona," (Ufunuo 13:12) ulimwengu kwa kweli utakuwa ukimwabudu shetani, kwani kumwabudu "mnyama," ni "kumwabudu yule joka aiyempa mnyama mamlaka."

"**Shetani**, katika kiburi chake na ujeuri, alikuwa **amejitangaza** kuwa **mtawala wa ulimwengu** aliye halali na wa kudumu, mmiliki wa mali yake yote na utukufu, huku akidai kuabudiwa na wale wote waishio humo, kana kwamba yeye ndiye aliyeiumba dunia na vyote vilivyomo." *Review and Herald*, September 1, 1874.

Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, **Ewe Lucifer**, mwana wa asubuhi jinsi ulivyokatwa kabisa, ewe uliyewaangusha mataifa! Nawe ulisema moyoni mwako, nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, katika pande za mwisho za kazikazini. Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na yeye Aliye juu Isaya 14:12–14.

Tangu kuanguka kwa shetani, yeye amekuwa akifanya kazi ya kujiimarisha kama mtawala wa dunia hii." *Review and Herald*, Machi 9, 1886.

MAKUNDI MAWILI ULIMWENGUNI

Baada ya Yohana kuwatambulisha "wale waishio duniani" wakiitengeneza "sanamu ya mnyama," yeye asema katika Ufunuo 13:16 kuwa watu "wote" wataathiriwa na sanamu hii. Ulimwengu mzima utaifuata Marekani, lakini Yohana akishawaelezea hao "wote" watakaoathiriwa na tendo hili, kisha huligawanya kundi hili katika makundi mawili – "wadogo kwa wakubwa, matajiri kwa maskini, walio huru kwa watumwa." Danieli vilevile ameugawanya ulimwengu katika "matajiri kwa maskini." Misri ya kale ilikuwa na majirani wawili waliokuwa na historia ya kuvutia.

Watu wa Libya, magharibi mwa Misri, waliishi pembezoni mwa jangwa, jambo ambalo liliwazuilia kuupata ustawi wa kiwango chochote. Kote katika historia yao walikuwa wakilitupa jicho la kutamani kuelekea Misri na bonde lenye rutuba la mto Nile. Waliwahi kujaribu kuivamia Misri mara kadhaa, lakini walirudishwa nyuma. Misri huashiria ulimwengu mzima, huku nayo Libya ikiwakilisha kile kijulikanacho siku hizi kama Ulimwengu wa Tatu. Libya huashiria zile nchi maskini, zilizonyimwa nafasi ya kujiendeleza, na zinazodhulumiwa, na ambazo hutamani kuufikia ustawi wa zile nchi tajiri za Ulimwengu wa Magharibi.

Ethiopia ya kale ilijumlisha sio tu Nubia, bali pia ile sehemu ya Arabia ya magharibi inayopakana na Bahari ya Shamu. Wamisri waliionea wivu Ethiopia kwa sababu ya migodi ya dhahabu iliyoko kwenye milima yake na vilevile utajiri wake wa mifugo, pembe za ndovu, ngozi, na mpingo, na pia kwa sababu bidhaa zilizotoka Afrika ya Kati ziliingia Misri kupitia wafanya biashara wa Ethiopia. Kama vile Misri ya kisasa huwakilisha ulimwengu, nayo Libya zile nchi maskini za Ulimwengu wa Tatu, vivyo hivyo Ethiopia huwakilisha zile nchi tajiri zaidi ulimwenguni.

Danieli ajiunga na ushuhuda wa Yohana pale anapotambulisha ya kuwa Upapa utautawala ulimwengu mzima, wadogo kwa wakubwa, matajiri kwa maskini, walio huru na watumwa – Libya na Ethiopia. Soma Danieli 11:43; Ufunuo 13:16.

> "Tunapokaribia mwisho wa historia ya ulimwengu huu, unabii ulioandikwa na Danieli wahitaji uangalifu wetu wa kipekee, kwani wahusiana na wakati huu tunaoishi. Wafaa uunganishwe na mafundisho ya kitabu cha mwisho cha Maandiko ya Agano Jipya." *Prophets and Kings*, 547.

Danieli aongeza kuwa watu wa Libya na Ethiopia watakuwa katika nyayo zake. Tazama Danieli 11:43.

> "**nyayo** – 4703: kutoka 6805; hatua; kitamathali urafiki: – kwenda, hatua.
>
> "6805: mzizi wa asili; kutembea, i.e. kutembea mara kwa mara; (juu) kupanda; **kutembea**; (chini) kutupa: – lete, nenda, tembea, ruka juu." *Strong's Exhaustive Concordance*.

Kuwa katika nyayo za "mfalme wa kaskazini" ni kuandamana pamoja naye huku akiupitia ulimwengu mzima. Yohana ataja kuwa mnyama wa pili huifanya "dunia na wale waishio ndani yake kumwabudu yule mnyama wa kwanza." Ufunuo 13:12. Katika kitabu, *Keys of This Blood*, kilichoandikwa na Malachi Martin, twalipata fungu la kuvutia. Martin ni mwenyeji wa Vatikani ambaye ameviandika vitabu vingi kuhusu Ukatoliki. Ndani ya *Keys of This Blood*, Martin afafanua ni kwa nini yeye anaamini ya kuwa papa ataketishwa juu ya kiti cha enzi na kuutawala ulimwengu mzima.

Anapozungumzia muundo wa nchi za ulimwengu, Malachi Martin aelezea kwa kina jinsi papa anavyozitazama. Hizi hapa ni dondoo kutoka *Keys of This Blood*, zikionyesha jinsi "ramani ya kisasa" ya ulimwengu ingechorwa na papa:

> "Kwa kifupi, ramani hiyo ya kisasa ya aibu ingekuwa ni dhihirisho la ukatili ambao tumefikia kuuelezea wazi kama kugawanywa kwa ulimwengu katika maeneo ya **Kaskazini na Kusini**, maana yake, kwa lugha rahisi, kuyagawanya mataifa, na watu walioko ndani ya mataifa, katika **matajiri na maskini** …
>
> "Ni ramani ya aibu kiasi hicho ambayo Papa Yohana Paulo aukabidhi ulimwengu katika makadirio yake ya kimaadili ya mpangilio wa kisiasa ambao unatuandalia siku zetu za usoni….
>
> "Katika ramani hiyo ya kisasa ya ulimwengu ya fedheha ambayo imekuwa kiini cha uangalifu wa Yohana Paulo, Kaskazini na Kusini hazijitokezi kama istilahi za kijiografia. Badala yake, ni mipaka ya kidunia ambapo **utajiri na umaskini** huyagawanya sio tu mataifa, bali pia jamii zilizomo ndani ya mataifa….
>
> "Yawe yanatumika ndani ya mipaka ya Marekani, au ulimwenguni kwa jumla, makadirio hayo ya kimadili ya Yohana Paulo kuhusu **Kaskazini na kusini** ni dhahiri. Katika uchumi unaobadilika kimadili, yeye asisitiza, matajiri hawafai kutajirika zaidi iwapo maskini watazidi kuwa maskini." *Keys of This Blood*, Malachi Martin, 163–164, 171.

MISRI HAITAPONYOKA

Katika Danieli 11:42, nchi ya "Misri" yawakilisha ulimwengu mzima, ambao una nchi nyingi ambazo, kulingana na Danieli, hazitaponyoka. Neno linalotafsiriwa "ponyoka" katika aya hii ni tofauti na neno linalotafsiriwa "ponyoka" katika aya iliyopita. Aya iliyopita iliwasilisha wazo la kuokolewa kwa kuteleza kutoka kwenye mkono ambao awali ulikuwa umekumbatia. Neno **ponyoka** katika aya hii lawasilisha maana ya kutopata wokovu kutoka kwa ngumi ya chuma ya Roma.

> "**ponyoka** – 6413: kike cha 6412; ukombozi; sehemu iliyotoroka: – ukombozi, (yaani) kuponyoka, masalio.
>
> "6412: mkimbizi: – (ambaye ame) toroka, mtoro." *Strong's*.

Katika aya ya arobaini na moja, wakati Marekani itaipitisha sheria ya kitaifa ya Jumapili, nena kama joka, na kuisimamisha sanamu ya mnyama, watu wengi wataaangushwa – wala **sio** nchi nyingi. Kisha ulimwengu utaifuata Marekani, na nchi nyingi, kwa hakika, nchi zote za dunia zitapinduliwa huku zikitembea hatua kwa hatua na Upapa.

Aya ya arobaini na mbili hututanguliza kwa papa katika harakati ya kuuleta ulimwengu katika upatanifu na Upapa. Hapo twakiona kikwazo cha tatu kikishindwa, jambo ambalo huuruhusu Upapa kupaa kwenye kiti cha enzi cha ulimwengu. Kufikia hapo "mfalme wa kaskazini" huacha kuwa kanisa tu, na kukirejelea cheo cha mtawala wa ulimwengu. Cheo hiki cha mamlaka kiliondolewa katika Danieli 11:40 pale "mfalme wa kusini" "aliposhindana naye" mnamo 1798. Lile jeraha la kufisha litapona kabisa wakati Upapa utanyosha mkono wake juu ya ulimwengu na nchi zake, na hatimaye kupewa "udhibiti" wa uchumi wa ulimwengu.

Twajua kuwa ataudhibiti uchumi wa ulimwengu, kwani Yohana atwambia "ya kuwa mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake." Ufunuo 13:17. Danieli aunganisha ushuhuda wake na ule wa Yohana huku akitaja kuwa kwa wakati huu "mfalme wa kaskazini" "Atamiliki hazina za dhahabu, fedha na utajiri wote wa Misri." Danieli 11:43.

Danieli anatumia Misri ili kuonyesha tukio la kuyatambulisha matukio haya ya nyakati za mwisho. Yeye hutumia Misri kuashiria ulimwengu, na pia kuwatumia majirani wa kale wa Misri kuugawanya ulimwengu katika makundi ya matajiri na maskini, walio huru na watumwa. Historia ya Misri hutuhusu kuuona ushawishi wa uchawi utakaoupoteza na kuunasa ulimwengu hata kuukubali udanganyifu huu, kwani twaukumbuka wajibu wa wale wachawi wa Misri katika kuyastahamili yale mapigo ya Mungu. Hadithi ya Misri pia hutupa onyesho kamili la kutusaidia kuutambua wokovu wa mwisho wa watu wa Mungu kama ulivyowakilishwa na uvukaji wa Bahari ya Shamu. Hata hivyo, kuitambua Misri kama kielelezo cha ulimwengu hutupatia habari hata zaidi zinazoathiri kipindi hiki.

UASI HULETA MAANGAMIZI

Twauona Upapa ukipokea "umiliki juu ya hazina za dhahabu, fedha na utajiri wote wa Misri." Danieli 11:43. Katika Danieli 11:41 Marekani yaitunga sheria ya kitaifa ya Jumapili huku ikianza kutembea pamoja na Upapa. Kufikia hapa, sheria za chanzo na athari huanza kuyaathiri mazingira ya dunia zaidi na zaidi.

"Kwa hatua za kasi twakaribia kipindi hiki. Wakati makanisa ya Kiprotestanti yataungana na serikali ya kilimwengu ili kuishikilia dini bandia, ambayo ilipelekea mababu zao kuteswa vikali kwa kuipinga: wakati serikali itayatumia mamlaka yake kuyatekeleza makataa ya kanisa na kuzihimili asasi zake – ndipo Marekani ya Kiprotestanti itakuwa imeitengeneza sanamu ya Upapa, kisha utakuwepo **uasi wa kitaifa ambao utamalizia tu kwa maangamizi ya kitaifa**." *Signs of the Times*, March 22, 1910.

Huku Marekani, na kisha ulimwengu, ikitunga na kuutekeleza uasi dhidi ya Mungu, kila hatua mbali na kweli itafuatwa na hukumu za uharibifu hata zaidi.

"Kanuni za Roma Katoliki zitachukuliwa chini ya uangalifu na ulinzi wa serikali. Uasi huu wa kitaifa utafuatwa upesi na maangamizi ya kitaifa." *Last Day Events*, 134.

Kila hatua katika uasi italeta uharibifu zaidi ulimwenguni. Wakati Danieli anapomtambulisha "mfalme wa kaskazini" akiunyosha mkono wake juu ya Misri na nchi nyingi za ulimwengu katika Danieli 11:42, uasi huo utakuwa karibu kufikia kilele chake. Wakati huo, ulimwengu utateswa na hukumu za Mungu huku Roho wa Mungu akiondolewa na uasi wa mwanadamu ukikaribia kukomaa. Katika hali hii, watu wa ulimwengu hakika watakuwa wakimtafuta mwokozi atakayewaahidi kuwa wataurejelea ustawi wa kilimwengu. Twaona katika hali hii njama ya papa wa Roma kufanya ahadi za amani kwa watu walioharibikiwa. Hali hii ya hatari yaenda sambamba na historia ya yale mapigo ya Misri.

"Lakini **Misri ilifanywa ukiwa na mapigo** kabla ya Filauni kukubali kusikiliza NDIMI aliye mkuu. Aliushikilia ukaidi wake hadi Misri ikaharibiwa, nao Wamisri, kutoka mtumwa aliye chini sana hadi mfalme aliyeketi kitini chake cha enzi, walizitazama maiti za vifungua-mimba wao." *Review and Herald,* April 23, 1901.

Katika hali hii ya ukiwa watu wa Misri walikuwa na hofu na wakawa tayari kuzisalimisha "hazina zao za dhahabu na za fedha, na vitu vyote vya thamani."

"Wamisri walikuwa wametajirishwa na kazi waliofanyiwa na Waisraeli kwa njia haramu, na kwa vile walikuwa karibu kuanza safari yao kuelekea makao yao mapya, ilikuwa sawa kwao kudai ujira wa kazi ya miaka mingi. Walitakikana kudai bidhaa za thamani, ambazo zingekuwa rahisi kusafirisha, naye Mungu angewapa fadhila machoni mwa Wamisri. Miujiza hiyo ya nguvu iliyofaywa ili kuwakomboa ingewatia hofu wadhulumu wao, ili matakwa ya watumwa hao yatimizwe." *Patriarchs and Prophets,* 253.

Huku kipindi cha zile hukumu angamizi kikiwakabili wanadamu, wakati uasi wa ulimwengu utakabidhi utawala kwa Upapa, hali ulimwenguni itawatia hofu wanadamu kiasi kwamba watu watabadili kwa urahisi faida zao za kiuchumi na ahadi bandia za amani. Bila shaka, historia ya Misri hutupa ufahamu wa nguvu wa Danieli 11:42-43.

Habari za Taabu

Lakini habari zitokazo mashariki na kaskazini zitamfadhaisha; naye atatoka kwa ghadhabu nyingi ili kuharibu, na kuwaondolea mbali watu wengi. Danieli 11:44.

Neno linalotafsiriwa kama **fadhaisha** katika aya ya arobaini na nne limetumika pia katika Danieli 5:6, 9:

> Ndipo uso wa mfalme ukambadilika; fikira zake zikam**fadhaisha**; viungo vya viungo vyake vikalegea; magoti yake yakagongana. … Ndipo mfalme Belshaza **akafadhaika** sana, uso wake ukambadilika, na wakuu wake wakaona fadhaa.

Katika kamusi ya *Strong's Concordance* ufafanuzi unaowasilishwa kimsingi ni kutetemeka moyoni, au kushtuka ghafla, kufadhaika, kuogopa, kuhofia. "Mfalme wa kaskazini" katika Danieli 11:44 hutambua ujumbe unaosababisha mjibizo ndani yake, sawia na ule mjibizo wa Belshazzar pale maandishi ya siri yalipotokea juu ya ukuta.

"Habari" huwakilisha ujumbe ambao utamsumbua sana "mfalme wa kaskazini". Tafsiri ya ujumbe ambao humshtua na kumkasirisha hutambulishwa katika ishara ya kiunabii kuhusu mashariki na kaskazini. Pande hizi huhusishwa na Kristo. Mashariki huashiria kuja kwa Kristo, nayo kaskazini ni upande ambao maadui wa watu wa Mungu hutokea wanapowavamia, kama pale walipotumiwa na Mungu kuzifikisha hukumu zake za kisasi dhidi ya uasi wa Israeli. Kaskazini huashiria ujumbe wa hukumu.

> "Mara kutatokea upande wa mashariki wingu dogo jeusi, likikaribia kulingana na nusu ya ukubwa wa mkono wa mwanadamu. Ni wingu ambalo linamzunuka Mwokozi na ambalo kwa mbali linaonekana kana kwamba limefunikwa na giza. Watu wa Mungu wanajua kuwa hii ni ishara ya mwana wa Adamu." *The Great Controversy*, 640.

> Neno hili ndilo lililomjia Yeremia, katika habari za watu wote wa Yuda; katika mwaka wa nne wa Yehoyakimu, mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda mwaka ule ndio mwaka wa kwanza wa Nebukadreza, mfalme wa Babeli; ambalo Yeremia, nabii, aliwaambia watu wote wa Yuda, na wenyeji wote wa Yerusalemu, kusema,… angalieni, nitapeleka watu na kuzitwaa jamaa zote za upande wa **kaskazini**, asema Bwana, nami nitatuma ujumbe kwa Nebukadreza, mfalme wa Babeli, mtumishi wangu, nami **nitawaleta juu ya nchi hii**, na juu yao wakaao ndani yake, na juu ya mataifa haya yote yaliyopo pande zote; nami nitawaangamiza kabisa, na kuwafanya kitu cha kushangaza, na kitu cha kuzomewa, na ukiwa wa daima.Yeremia 25:1-2, 9.

> "Yeye aliongozaye kanisa Lake na hatima ya mataifa aiendeleza kazi ya mwisho itakayotekelezwa katika ulimwengu huu. Yeye huwapatia malaika zake jukumu la **kuzitekeleza hukumu zake**. Hebu wachungaji na waamke, hebu na waifahamu hali ilivyo. Kazi ya hukumu huanzia hekaluni. 'Na tazama, **watu sita wakaja,** wakitokea kwa njia ya lango la juu, lielekealo upande wa **kaskazini,** kila mmoja ana kitu chake cha kufisha mkononi mwake; na mtu mmoja kati yao amevaa bafta, naye ana kidau cha wino cha mwandishi kiunoni. Wakaingia, wakasimama karibu na madhabahu ya shaba.' Soma Ezekieli 9:2-10. Amri ni, 'Waueni kabisa, mzee, na kijana, na msichana, na watoto wachanga, na wanawake; lakini msikaribie mtu ye yote mwenye hiyo alama; tena anzeni katika patakatifu pangu. Basi wakaanza kwa wazee waliokuwa mbele ya nyumba' Kwa hiyo wakaanza na wale wazee waliokuwa mbele ya hekalu.' Asema Mungu. 'Nitaleta njia yao juu ya vichwa vyao.'" *Testimonies to Ministers*, 431–432.

Mashariki na kaskazini haziwakilishi tu ujumbe wa hukumu na kurudi kwa Kristo, bali pia humtambulisha Kristo mwenyewe:

> Ni nani aliyemwinua **mmoja atokaye mashariki,** ambaye katika haki amemwita mguuni pake? Ampa mataifa mbele yake, na kumtawaza juu ya wafalme; awatoa wawe kama mavumbi kwa upanga wake, kama makapi yaliyopeperushwa kwa upinde wake.… Nimemwinua **mtu toka kaskazini,** naye amekuja; **toka maawio ya jua** amekuja anitajaye jina langu; naye atawajilia maliwali kama akanyagaye matope, na kama mfinyanzi afinyangaye udongo. Ni nani aliyeihubiri habari tokea mwanzo, tupate kuijua? Na tokea zamani, tupate kusema, Yeye ni mwenye haki? Naam, hapana hata mmoja aliyetujulisha; naam, hapana hata mmoja aliyetuonyesha; naam, hapana hata mmoja aliyesikia maneno yenu. Mimi kwanza nitauambia Sayuni, Tazama; hawa ndio; nami nitampa Yerusalemu mletaji wa habari njema. Isaya 41:2, 25-27.

Fungu hili la Isaya humtambulisha Kristo kama yule Mmoja ambaye angeinuliwa kutoka mashariki na kaskazini. Ni ujumbe wa haki ya Kristo, ambao ndio ujumbe wa mwisho wa huruma kwa ulimwengu unaokufa – yaani ujumbe wa tabia ya Kristo. Soma *Christ's Object Lessons*, 415. Katika Danieli 11:44 hupatikana "habari njema" ya Isaya 41, na vilevile "habari njema" alizozitangaza Kristo mwanzoni mwa huduma Yake:

> Roho ya Bwana MUNGU i juu yangu; kwa sababu Bwana amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema; amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao, na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao. Kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa, na siku ya kisasi cha Mungu wetu; kuwafariji wote waliao; Isaya 61:1-2.

Tofauti kati ya "habari" za Danieli 11:44 na ule ujumbe wa Kristo alipokuwa duniani ni kwamba wakati huo haukuwa – "siku ya kisasi ya Mungu." Ni kule kukitambua "kisasi" kinachohusishwa na habari katika Danieli 11:44, ambako humfanya "mfalme wa kaskazini" kutetemeka na kuogopa.

"Habari njema" za haki ya Kristo kila mara huambatana na umwagaji wa Roho Mtakatifu:

> "Je, ni yapi yaliyokuwa matokeo ya umwagaji wa Roho Mtakatifu Siku ya Pentekoste? **Habari njema za Mwokozi aliyefufuka** zilipeperushwa hadi miisho ya ulimwengu wenye wakazi." *The Acts of the Apostles*, 48.

Ujumbe huu wa habari njema utatangazwa tena hivi karibuni. Mara hii hautakuwa katika muktadha wa "Mwokozi aliyefufuka," bali ni katika muktadha wa kurudi kwa Kristo na mwisho wa hukumu ambayo inatangulia – "siku ya kisasi cha Bwana." Isaya 34:8. Ujumbe huu utasababisha hofu na kisasi kutoka kwa vikosi vinavyohusishwa na mfalme wa kaskazini.

Danieli 11:40-43 husimulia kutiwa jeraha la kufisha juu ya Upapa mnamo 1798, kukifuatiwa na kurejea kwa Upapa kwenye nafasi ya utawala iliyokuwa yake kwa hatua tatu. Kwanza, hulipiza kisasi dhidi ya vikosi vya yule "mfalme wa kusini," na kisha huingia "nchi ya uzuri" ya Marekani. Kisha mataifa yote ya ulimwengu, yakiashiriwa na nchi ya "Misri", huchukuliwa mateka. Baada ya kuvishinda vikwazo hivi vitatu, twamwona "mfalme wa kaskazini" akidhibiti pesa zote za dunia, ikitambulisha kuwa Upapa umeirejelea kikamilifu ile nafasi aliyoimiliki kwa muda wa miaka 1260 ya utawala wa Upapa.

Baada ya hayo, katika aya ya arobini na nne, Danieli hutuelekeza kwenye pambano la mwisho baina ya Upapa na Mungu. Kutiwa muhuri kwa watu wa Mungu kunaanza kwenye aya ya arobaini na moja, huku sheria ya Jumapili ikianzaa Marekani, lakini aya ya arobaini na nne hutambulisha moja kwa moja ujumbe wa kutiwa muhuri, huku pia ikieleleza upinzani wa kishetani kwa ujumbe huo. Ujumbe wa kutiwa muhuri ni ujumbe kutoka mashariki, yaani ujumbe wa malaika watatu:

> Nikaona malaika mwingine, akipanda **kutoka maawio ya jua**, mwenye muhuri ya Mungu aliye hai; akawapigia kelele kwa sauti kuu wale malaika wanne waliopewa kuidhuru nchi na bahari, akisema, Msiidhuru nchi, wala bahari, wala miti, hata tutakapokwisha kuwatia muhuri watumwa wa Mungu wetu juu ya vipaji vya nyuso zao. Ufunuo 7:2-3.
>
> "Kisha nilimwona **malaika yule wa tatu**. Malaika aliyekuwa akiniongoza alisema, "kazi yake ni ya kuogofya. Utume wake ni wa kutisha. Ni malaika anayechagua ngano kutoka katika magugu, na **kuweka muhuri**, au kufunga ngano kwa ajili ya ghala la mbinguni. Mambo haya yanafaa kushughulisha akili zote, na usikivu wote." *Early Writings*, 118.

Kupitia ujumbe wa malaika wa tatu kanisa, na kisha ulimwengu – itajaribiwa. Huo ndio ujumbe unaomkasirisha "mfalme wa kaskazini":

"Wakati ujumbe wa malaika wa tatu unapofungwa, hakutakuwepo tena na rehema kwa ajili ya kuwasihi wakazi wa dunia wenye dhambi. Watu wa Mungu wamekamilisha kazi yao. Wamepokea "mvua ya masika" burudishop kutoka mbele za Bwana, na wameandaliwa kwa ajili ya saa ya kujaribiwa iliyo mbele yao. Mbinguni malaika wanakwenda huku na huko kwa haraka. Malaika anarudi kutoka duniani na kutangaza kwamba kazi yake imekamilika; **jaribu la mwisho** limeletwa ulimwnguni, na wote ambao wamethibitika wenyewe kuwa waaminifu kwa sheria za Mungu wamepokea Muhuri wa Mungu aliye hai. Kisha Kristo anakomesha huduma yake ya uombezi katika hekalu la mbinguni. Anainua mikono yake na kusema kwa sauti kuu, "Imekwisha" na jeshi lote la malaika huvuta taji zao wakati anapotoa tangazo kuu: Mwenye kudhulumu azidi kudhulumu; na mwenye uchafu azidi kuwa mchafu; na mwenye haki azidi kutakaswa. Ufunuo 22:11 kila kesi imeamuliwa kwa ajili ya uzima au mauti. Kristo amefanya upatanisho kwa ajili ya watu wake na kufuta dhambi zao. Hesabu ya raia wake imefanyika. Ufalme na mamlaka, na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu yote, karibu kuwekwa kwa waridhi wa wokovu, na Yesu atatawala kama mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana (Daniel 7:27).

"Wakati anapotoka hekaluni, giza kuu huwafunika wakazi wa dunia. Katika wakati huo wa kutisha wenye haki ni lazima waishi mbele za Mungu Mtakatifu bila Mwombezi. **Kizuizi kilichokuwa kimewekwa kwa waovu kinaondolewa, na shetani anapata mamlaka kamili ya uovu wa mwisho.** Uvumilivu wa Mungu wa muda mrefu umekwisha. Ulimwengu umekataa rehema zake, umekataa upendo wake, na kuikanyaga sheria yake. Waovu wamevuka mpaka wa rehema yao; Roho wa Mungu, ambaye aliendelea kupingwa hatimaye ameondolewa. Pasipokuwa na ulinzi wa neema ya Mungu, wanakuwa hawana ulinmzi wo wote kwa waovu. Ndipo shetani atawaswaga ghafla wakazi wa dunia katika taabu moja kuu ya mwisho. Wakati malaika wanaacha kuzuia pepo kali za tamaa ya mwanadamu, vurugu za aina zozote zitaachiliwa. Ulimwengu mzima utahusika katika maangamizo ya kutisha sana kuliko yale yaliyoijia yerusalemu ya zamani.

"Malaika mmoja tu aliangamiza wazaliwa wa kweanza wa misri na kuijaza nchi kwa maombolezo. Wakati Daudi alipopmkosea Mungu kwa kuwahesabu watu, malaika mmoja tu alisababisha maangamizo hayo ya kutisha ambayo yalikuwa ni kuadhibiwa kwa dhambi yake. Uwezo wa kuangamiza unaofanana na huo uliotumiwa na malaika wakati Mungu anapoamuru, utatumiwa na malaika waovu wakati anaporuhusu. Sasa Majeshi yako tayari, na yanangoja tu ruhusa ya Mungu, ili yaeneze maangamizi kila mahali.

Wale wanaoheshimu na kuitii sheria ya Mungu wamekuwa wakishutumiwa kwa kuleta hukumu za Mungu ulimwenguni, na watachukuliwa kama wanaosababisha majanga ya kutisha ya asili na vurugu na umwagaji damu, miongoni mwa watu wanaoijaza dunia kwa matatizo. **Nguvu iliyoambatana na onyo la mwisho iliwakaribisha waovu; hasira yao inawaka dhidi ya wote walioupokea ujumbe, na shetani atawachochea roho ya chuki na mateso kwa kiwango cha juu sana.**

Kwa vile Sabato itakuwa ndiyo kiini kikuu cha pambano katika ulimwengu wote wa Kikristo, na mamlaka za dini na serikali zitaungana kulazimishja utunzaji wa Jumapili, kuendeleza kukataa kuwa watu wa kuchukiwa sana na ulimwengu. Itasisitizwa kwamba watu wachache wanaoipinga taasisi ya kanisa na amri ya serikali hawapaswi kuvumiliwa; na kwamba ni afadhali wao wateseke kuliko mataifa yote kuingizwa katika vurugu na uhalifu. Hoja kama hiyo ilitolewa miaka elfu moja na mia nane iliyopita dhidi ya Kristo na Wakuu wa watu. Kayafa mwerevu alisema, yatufaa sisi, mtu mmoja afe kwa ajili ya watu, wala lisiangamie taifa zima. Yohana 11:50 Hoja hii itaonekana mwishoni; na hatimaye amri itapitishwa dhidi ya wale wanaotakasa Sabato ya amri ya nne, ikiwatangaza hadharani kama watu wanaostahili adhabu kali sana na baada ya muda fulani watu watapewa uhuru wa kuwauwa. Uromani katika ulimwengu wa kale na Uprotestanti ulioasi katika ulimwengu Mpya wataendeleza jambo hilo hilo kwa wale wanaoziheshimu amri zote za Mungu.

Kisha watu wa Mungu watatumbukizwa katika hayo matukio ya mateso na taabu yaliyoelezwa na nabii kama wakati wa taabu ya Yakobo. Hiov ndivyo asemavyo Bwana: tumesikia sauti ya tetemeko na ya hofu na wala si ya amani… Nyuso zote zimegeuka rangi. Ole! Maana siku ile ni kuu, hata hapana inayofanana nayo; maana ni wakati wa taabu yake Yakobo; lakini ataokolewa nayo." Yeremia 30:5-7." *The Great Controversy*, 613–616.

Ujumbe wa kilio kikuu huanza kutangazwa kikamilifu baada ya kupitishwa kwa sheria ya kitaifa ya Jumapili. Mateso yatazidishwa kuanzia wakati huo kuendelea – na hatimaye kujumuisha ufiaji dini:

"Wakati kazi hii kubwa itafanyika katika pambano hilo, **kabla ya kabiliano la kumalizia**, wengi watafungwa jela, wengi watatoroka kutoka mijini na vijijini ili waziokoe nafsi zao, na **wengi watakuwa wafia dini** kwa ajili ya Kristo katika kusimama ili kuitetea kweli." *Maranatha*, 199.

"**Ulimwengu mzima** utachochewa na chuki dhidi ya Waadventista Wasabato, kwa sababu hawatauinamia Upapa, kwa kuitunza Jumapili, ambayo ni asasi ya utawala huu upingao Kristo. Ni kusudi la Shetani kufanya **waondolewe kutoka duniani**, ili utawala wake ulimwenguni usipate upinzani." *Review and Herald*, August 22, 1893.

UWASILISHAJI ULIO DHAHIRI ZAIDI

"Wakati wa taabu na uchungu ulio mbele yetu unahitaji imani ambayo inaweza kustahimili uchovy, kuchelewa na njaa – imani ambyo haitaweza kuzimia katika kujaribiwa vikali… Wakati wa taabu, amabo mfano wake haujawahi kuwepo kamwe," Danieli 12:1 U karibu kufunuliwa kwetu na tutahitaji uzoefu ambao kwa sasa hatuna na ambao watu wengi sana nio wavivu mno kuupata. Mara nyingi taabu inakuwa ni jambo kubwa mno la kuwaziwa kuliko inavyokuwa katika uhalisia; **lakini hivi sivyo ulivyo ukweli wa nhatri iliyo mbele yetu. Onyesho la waziwazi kabisa haliwezi kufikia kiwango cha ukubwa wa majaribu ya wakati wa taabu.** *The Great Controversy*, 621–622.

Wakati rehema itafungwa kwa ulimwengu, hapatakuwepo tena wafia dini.

Katika aya ya arobaini na nne, papa na washirika wake huenda "kuharibu na kuwaondolea mbali watu wengi." Ujumbe kutoka mashariki na kaskazini, yaani ujumbe wa malaika wa tatu, utafungwa pale rehema kwa walimwengu itakapofungwa, nao maadui wa watu wa Mungu wataletwa kikamilifu chini ya utawala wa roho wa shetani:

"Nilielekezwa kwenye wakati ambao ujumbe wa malaika wa tatu ulipokuwa unafungwa. Uwezo wa Mungu ulikuwa juu ya watu wake; walikuwa wameimaliza kazi yao na walikuwa tayari kwa wakati wa taabu uliokuwa ukiwajia. Walikuwa wameisha pata mvua ya masika, au burudisho kutoka mbele za Bwana, na Ushuhuda wa milele ulikuwa umeamshwa. Onyo kuu la mwisho lilikuwa limetangazwa kila mahali, **nalo lilikuwa likiwachochea na kuwakasirisha wakazi wa dunia** ambao hawakuukubali ujumbe huo." *Early Writings*, 279.

Danieli 11:45 yaelezea ni wapi "mfalme wa kaskazini," kanisa la Mungu, na wakazi wa dunia watasimama kuhusiana wao wenyewe wakati neema itafungwa. "Mfalme wa kaskazini" amekuwa akijaribu kuuzuia ujumbe wa kilio-kikuu usiwafikie wakazi wa dunia. Nao "mlima mtakatifu wa uzuri," kanisa la Kristo, limekuwa likiutangaza ujumbe wa onyo la mwisho. Mataifa, jamaa, na makabila ya ulimwengu ambao wangeupokea ujumbe huo wa mwisho huwakilishwa kama "bahari." "Mfalme wa kaskazini" naye ajaribu kuuzuilia ujumbe huu kwa kusimama kati ya wale wanaoutangaza ujumbe huo na wasikilizaji watarajiwa. Aya hii ya mwisho yausimulia muundo wa pambano katika bonde la Megido.

Hakuna wa Kumsaidia

Naye atapanda hema zake za kifalme ndani ya bahari na mlima mtakatifu wa uzuri; lakini ataufikia mwisho wake, wala hakuna atakayemsaidia. Danieli 11:45.

Danieli 11:45 huelezea ni wapi "mfalme wa kaskazini" ataufikia mwisho wake. Ijapokuwa tafsiri ya Biblia ya King James yadokeza kuwa Upapa uko **ndani** ya mlima ulio mzuri na mtakatifu, tafsiri zingine kadhaa zaonyesha kuwa aya hiyo yafaa kutafsiriwa kwa kuonyesha kuwa Upapa huziweka hema zake za kifahari (hema za kivita) **kati** ya bahari **na** mlima huo mtakatifu:

> Naye atapanda hema zake ya kifalme **kati** ya bahari **na** mlima mtakatifu wa uzuri (Sayuni); hata hivyo, atafikia mwisho wake, wala hakuna ye yote atakayemsaidia. Danieli 11:45. Tafsiri ya Amplified. Tazama pia American Standard Version na Young's Literal Translation.

> "Mlima mtakatifu wa uzuri," ni kanisa la Mungu, kulingana na aya zifuatazo:
>
> Na itakuwa **katika siku za mwisho,** mlima wa **nyumba ya Bwana** utawekwa imara juu ya milima, nao utainuliwa juu ya vilima; na mataifa yote watauendea makundi makundi. Na mataifa mengi watakwenda na kusema, Njoni, twende juu **mlimani kwa Bwana**, **nyumbani kwa Mungu** wa Yakobo, naye atatufundisha njia zake, nasi tutakwenda katika mapito yake maana katika Sayuni itatoka sheria, na neno la Bwana katika Yerusalem. Isaya 2:2-3.

> "Bahari" ni watu wa ulimwengu:
>
> Kisha akaniambia, Yale **maji** uliyoyaona, hapo aketipo yule kahaba, **ni jamaa na makutano na mataifa na lugha**. Ufunuo 17:15.

Mojawapo ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara kuhusu Danieli 11:40-45, ni iwapo "mlima mtakatifu wa uzuri" wa aya ya arobaini na tano ni sawa na ile "nchi ya uzuri" ya aya ya arobaini na moja. Hebu tuzilinganishe. Ishara zote mbili zinacho kivumishi kinachotafsiriwa kama "zuri," lakini tukiliacha neno hilo "uzuri" nje ya virai hivyo viwili, twaiona tofauti iliyoko kati ya nchi na mlima. Nchi na mlima mtakatifu ni vitu viwili tofauti, hata kama vyote ni "vizuri."

Nchi ya aya ya arobaini na moja ni pahali ambapo watu wa Mungu na kweli waliwekwa ili kuwezesha utangazaji wa ujumbe wa onyo la mwisho. Kanisa lililoinuliwa ili kuutangaza ujumbe huu ndio mlima mtakatifu wa uzuri wa aya ya arobaini na tano. Vyote viwili ni "vizuri," kwa namna yao yenyewe, lakini vyaashiria vitu viwili tofauti, japo vina uhusiano wa karibu. Kanisa, na nchi lilipolelewa kanisa hilo, ni vitu viwili tofauti.

Aya hii yaelezea wakati ambapo wanadamu hatimaye watagawanyika katika makundi mawili. Upapa unasimuliwa ukiwa katikati mwa makundi hayo mawili ya watu, kwani Upapa umekuwa ndicho chombo cha kimsingi kinachotumika na shetani ili kuwazuilia watu wa ulimwengu wasije wakausikie ujumbe huo wa onyo la mwisho. Nafasi ya Upapa ikiwa ni katikati, wale watu wanaoukataa ujumbe huo wa onyo la mwisho wako upande mmoja, nao watu wa Mungu wamesimama upande mwingine:

> "Kuna makundi mawili tu ulimwenguni leo, na ni makundi mawili tu ndio yatakayotambuliwa hukumuni – wale wavunjao sheria ya Mungu, na wale wanaoitunza sheria Yake. **Nguvu mbili pinzani zadhihirika katika pambano hilo kuu la mwisho**. Katika upande mmoja amesimama Muumba wa mbingu na nchi. Wote walio upande Wake wanao muhuri Wake. Wao ni watiifu kwa amri Zake. Katika upande wa pili amesimama mfalme wa giza, pamoja na wale waliochagua uasi na ukaidi." *Review and Herald*, May 7, 1901.

Danieli 11:45 huelezea kuhusu ule mstari unaowagawanya wanadamu kama ulivyoelezwa na hema za kifalme za yule "mtu wa kuasi". Katika upande mmoja wapo wale wanaoakisi tabia ya mtu huyo wa kuasi ambayo ni kujiinua, huku upande mwingine tukiwaona wale wanaoakisi upendo wa Yesu ambao ni wa kujitolea. Katika aya hii kanuni ya kimsingi ya siri ya kuasi – yaani kujiinua – imeashiriwa na "mfalme wa kaskazini" anavyozipanda hema zake za kivita ambazo ni za kifalme kwa ujeuri machoni pa ulimwengu mzima, na kujitangaza kuwa mfalme wa wale wanaowakilishwa na bahari, huku pia akijiandaa kuwaangamiza wale ambao ni wa "mlima mtakatifu wa uzuri". Katika kilele cha tendo hili la jeuri, "mfalme wa kaskazini" ataufikia mwisho wake – wala hakuna atakayemsaidia.

Katika kamusi ya *Strong's Exhaustive Concordance*, twapata ufafanuzi ufuatao:

"panda – 5193: mzizi wa kale; ifaavyo ***kupigilia*** **ndani, yaani *kaza***; hasa kupanda (kikawaida au kitamadhari):– imarisha, panda.

"hema – 168: kutoka 166; hema (kama **ionekanavyo dhahiri kutoka mbali**): – mfuniko, (makazi) (pahali), nyumbani, tabenakulo, hema.

"166: mzizi wa asili; kuwa *angavu*: – **kung'aa**.

"kifalme – 643: laonekana lenye asili ya kigeni; kibanda au kasri-hema – kasri."

Kitendo cha kujitia kati ya ujumbe wa Mungu na wanaotarajiwa kuupokea hutumika katika aya ya arobaini na tano, na pia ni kielelezo cha kawaida katika Roho ya Unabii:

"Ijapokuwa ameshindwa kumtoa Mungu kutoka kwenye kiti Chake cha enzi, Shetani amemshtaki Mungu kwa sifa za kishetani na kudai sifa za Mungu kuwa ndizo zake mwenyewe. Yeye ni mwongo, na kupitia ujanja wake kama wa nyoka, kupitia vitendo vyake vya ukora, amejivutia kwake mwenyewe ibada ambayo mwanadamu afaa kumpa Mungu, na **amekipanda kiti chake cha enzi cha kishetani *katikati* ya mwanadamu anayeabudu na Mungu Baba**." *Manuscript Releases*, volume 7, 215.

"Kabla tu ya kuja kwa Mwana wa adamu, ipo – na imekuwepo kwa miaka iliyopita – juhudi ya adui kukitia kivuli chake cha kishetani **katikati** ya mwanadamu **na** Mwokozi wake." *Manuscript Releases*, volume 6, 7.

"Yeye, Mwalimu mkuu, alikuwa ulimwenguni; alikuwa ni nuru ya ulimwengu; lakini shetani aliingiza kivuli chake cha kishetani katikati Yake na roho ambazo Kristo alikuja kuziokoa." *The Signs of the Times*, March 20, 1901.

"Twawasihi enyi mnaoipinga nuru ya kweli, **msimame nje ya njia ya watu wa Mungu**. Acheni nuru itokayo Mbinguni iwaangazie kwa miale iliyo angavu na thabiti." *Review and Herald*, May 27, 1890.

"Mtu awaye yote asithubutu kujitia **katikati** ya watu **na** ujumbe wa mbinguni. Ujumbe wa Mungu utawafikia watu; na hata ikiwa hakuna sauti miongoni mwa watu ya kuutangaza, mawe yenyewe yatapaza sauti." *Counsels to Writers and Editors*, 38.

"Sabato ni jaribio la Mungu, na hakuna mtu yeyote, awe ni mfalme, kuhani, au mtawala, aliyeruhusiwa kuja **katikati** ya Mungu **na** mwanadamu." *Testimonies*, volume 9, 234.

Katika sura iliyopita tulijadili Danieli 11:44, na hisia za "mfalme wa kaskazini" kuhusu ujumbe wa haki ya Kristo, kama ulivyoashiriwa na "habari" zitokazo "mashariki na kaskazini." Aya hiyo ilitambulisha hofu na ghadhabu ya mfalme huyo wa kaskazini pale alipoutambua ujumbe wa kilio-kikuu. Anapoondoka ili "kuwaangamiza na kuwaondolea mbali wengi," rehema inafungwa na ulimwengu hugawanyika kwa makundi mawili. Aya ya arobaini na tano huendelea kuelezea kwa kuusimulia mgawanyiko huu, lakini pia hutumia ishara za kinabii zinazoelekeza hadi Harmagedoni, ambayo imeelezewa katika Ufunuo kumi na sita.

KATI YA BAHARI

Mashariki mwa Bahari ya Mediterania, kusini magharibi mwa Bahari ya Galili, na kaskazini mwa Bahari ya Chumvi, ni Megido. Takriban maili 35 kusini mwa Megido na Yerusalemu ni Mlima Gerizim na Ebali, milima ya laana na mibaraka. Katika mandhari hii ya kijiografia twauona mwisho wa Upapa kama ulivyowasilishwa kama ishara katika Danieli 11:45. Historia ya Biblia kuhusu maeneo haya ni nyingi huku habari zikielekeza kiishara kwenye pambano litakalotamatishwa na kuja kwa pili kwa Kristo.

Wafasiri wengi wa Biblia hutambua mahali pa mfalme wa kaskazini, katika Danieli 11:45, kuwa katikati ya jiografia hii ya Agano la Kale. Kuashiria huku kwa kijiografia, bila shaka, kwalitambulisha pambano la Harmagedoni lipatikanalo katika Ufunuo kumi na sita. Sharti tuwe na uthabiti katika kuzitumia kanuni zetu za kinabii, na, ijapokuwa kidokezo hiki cha Megido huonekana kwa urahisi katika Danieli 11:45, sharti tuendelee kutafuta pahali hapo pa aya hii kiroho – wala sio kihalisi.

Katika Ukatoliki, Uprotestanti, na hata Uadventista wa leo, twawapata watu wanaoitafsiri aya hii kama Israeli ya kihalisi. Habari za kijiografia na za kihistoria zilizoko ndani ya aya hii huelezea mahali ulimwengu mzima ulipo kiroho wakati wa pambano la Harmagedoni. Kuutambua "mlima mtakatifu wa uzuri" kama Yerusalemu ya kisasa haitaambatana na aya tano zilizopita, kwani zote zimeeleweka katika mandhari ya kiroho ambayo ni ya kisasa. Iwapo mtu atachagua kuutambua "mlima mtakatifu ulio mzuri" katika aya hii kama Yerualemu ya kisasa, basi uthabiti wa matumizi ya kiunabii hudai kuwa ishara zote katika mfululizo huu sharti ziwe na vifanani vya kihalisia. Jambo hili haliwezekani, kwani "Edomu" ya aya ya arobaini na moja – haimo tena kama taifa au jamii.

Ikiwa tutalipitia wasilisho hili la Danieli 11:40-45 kutoka sura ya kwanza hadi ya mwisho, tutapata kuwa tumezitumia kwa njia thabiti uashiriaji (kiroho) matumizi kwa maumbo na ishara, kwa makubaliano kwamba matukio haya hutendeka baada ya msalaba.

MWITO WA MWAMKO

Tumeona vilevile kuwa mfululizo wa ushindi wa Upapa pale unapoirejelea "nafasi yake ya awali ya utawala," ni sawa na ule mfululizo uliosimuliwa katika kitabu cha Ufunuo. Pia tuliutambulisha mfululizo huu kama marudio kamili ya "historia" inayosimuliwa katika Danieli 11:30-35, ambayo Dada White aliitambulisha kama ruwaza ya kulinganisha na matukio ya mwisho yaliyoandikwa katika Danieli kumi na moja.

Huku tukifahamu kuwa matukio ya mwisho ya unabii yangezungumzia yule "mtu wa kuasi," tulitambulisha pia kuwa ndani ya vitabu vya Danieli na Ufunuo kungekuweko na "ongezeko la maarifa" ambalo "lingewaandaa watu wa Mungu kusimama" katika siku hizi za mwisho, na kuwa ongezeko hili maalum la maarifa lingejumlisha maarifa kumhusu yule "mtu wa kuasi." Hatukusadikisha tu baadhi ya uhusiano kati ya aya hizi na kitabu cha Ufunuo, bali maudhui ya aya hizi yaweza kuthibitishwa na matukio yanayobainika katika ulimwengu wa leo. Tulizingatia kuwa hitaji letu kubwa zaidi kama watu wa Mungu ni uamsho na matengenezo, na tukafahamu kuwa Dada White alisema kuwa uamsho huu unaohitajika utakuja kutokana na ufahamu upatikanao ndani ya unabii wa Danieli na Ufunuo.

Tulianza somo hili kwa kuyalinganisha matukio yaliyosimuliwa katika sura ya kwanza ya *Testimonies*, vol 9, na hapo tukapata kuwa Dada White aliyatambulisha matukio haya ya mwisho na utimilifu wa Danieli kumi na moja. La kutuliza zaidi ni kuwa Dada White aliyataja matukio haya ya Danieli kumi na moja, na kisha akasema kuwa "harakati za mwisho zitakuwa ni za kasi mno." Kaka na Dada, matukio ya mwisho yaliyo ya kasi yanayosimuliwa katika Danieli 11:40-45 yalianza kutendeka mnamo 1989 pale Muungano wa Sovieti ulipovunjika. Huu ndio wakati wetu wa kuamka ili tushughulikie ishara za nyakati, ushuhuda wa unabii na hitaji la maandalizi ya kibinafsi!

> "Lakini ipo siku iliyopangwa na Mungu ya kuifunga historia ya ulimwengu huu. 'Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja.' Mathayo 24:14. Unabii unatimia upesi. **Mambo mengi, mengi zaidi, yafaa kusemwa kuhusu masuala haya muhimu.** Siku iko karibu ambapo hatima ya kila mtu itathibitishwa milele. Siku hii ya Bwana yaharakisha. Walinzi bandia wanasema kwa yowe, 'Yote yako shwari'; lakini siku ya Mungu yasogea upesi. Kelele ya hatua zake imefunikwa isisikike kiasi kwamba haiwaamshi walimwengu kutoka kwenye usingizi waliolala ufananao na kifo. Huku walinzi wakilia, 'Amani na usalama,' 'maangamizi ya ghafla yatawashukia,' 'wala hawataponyoka.' (1 Wathesaaloniki 5:3); 'kwa kuwa kama mtego unasavyo, ndivyo itakavyowajilia watu wote wakaao juu ya uso wa dunia nzima. Luka 21:35. Itamvamia mpenda raha na mwenye dhambi kama mwivi usiku. Wakati kila kitu huonekana kuwa salama, nao watu huenda kupumzika huku wametosheka, hapo ndipo mwivi wa usiku wa manane hunyemelea na kuvamia mawindo yake. Wakati watu wamechelewa sana kuuzuia uovu huo, ndipo wao hugundua kuwa mlango fulani au dirisha fulani halikuwa limefungwa vilivyo. Kwa sababu hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari; kwa kuwa katika saa msiyodhani Mwana wa Adamu yuaja. Mathayo 24:44. Watu sasa wanajipumzisha, wakijidhania kuwa salama chini ya makanisa yanayopendwa; lakini hebu wote na wajihadhari, kusije kukawa na nafasi iliyoachwa wazi kwa adui kuingilia. **Jitihada nyingi zafaa kufanywa ili kulidumisha suala hili mbele ya watu. Ukweli huu wa dhati sharti udumishwe sio tu mbele ya walimwengu, bali pia mbele ya makanisa yetu, ya kuwa siku ya Bwana itakuja ghafla, pasipo kutarajiwa.** Onyo hilo la kuogofya la unabii limetolewa kwa kila mtu. Mtu yeyote asije akajihisi kuwa yeye amekingwa na hatari hiyo ya kushangaza. Usiiache tafsiri ya mtu ya unabii ikupokonye kule kusadiki kwako kwa ufahamu wa matukio yanayoonyesha ya kuwa tukio hili limekaribia." *Fundamentals of Christian Education*, 335–336.

"Nimearifiwa ya kwamba yatupasa kuupatia umaarufu ushuhuda wa baadhi ya wafanya kazi wakongwe ambao sasa wameaga. Hebu na wazidi kuongea kupitia makala yao kama yanavyopatikana kwenye magazeti yetu ya mapema. Makala hayo yafaa kuchapishwa tena, ili kuwe na sauti iliyo hai kutoka kwa mashahidi wa Bwana. Historia ya ujuzi wa mapema katika ujumbe huu itakuwa ni nguvu ya kustahimili ubunifu stadi wa hila za Shetani. Agizo hili lilirudiwa hivi majuzi. Sharti niwasilishe mbele ya watu shuhuda za ukweli wa Biblia, na kuzirudia jumbe za kauli zilizopeanwa miaka iliyopita. Ningetamani kwamba mahubiri yangu niliyoyahubiri kwenye makambi na makanisani yaishi hata kuitenda kazi yaliyoteuliwa kuifanya." *The Publishing Ministry*, 31.

WAANZILISHI NA DANIELI KUMI NA MOJA

UPAPA NDIYE "MFALME WA KASKAZINI"

"Kunao msitari wa unabii wa kihistoria katika sura ya kumi na moja, ambapo ishara zimepeanwa, kuanzia wafalme wa Uajemi, na kufikia chini kupita Ugiriki na Roma, hadi wakati ule utawala huo utafikia mwisho wake, na hakuna atakayemsaidia. Ikiwa ile miguu na vidole kumi vya ile sanamu ya chuma ni Roma, ikiwa yule mnyama mwenye pembe kumi ambaye alitupwa ndani ya moto wa ile siku kuu ni mnyama wa Kirumi, ikiwa ile pembe ndogo iliyompinga Mfalme wa wafalme ni Roma, na ikiwa eneo na umbali sawa unapitiwa katika minyororo hii minne ya kiunabii, basi utawala wa mwisho wa sura ya kumi na moja, ambao 'utafikia mwisho wake na hakuna wa kumsaidia,' ni Roma." Mahubiri ya James White katika kikao cha General Conference mwaka wa 1878, *Review and Herald*, Octoba 3, 1878.

"NCHI YA UZURI" NI MAREKANI

"Ni katika nchi hii ya Marekani ambapo umati mkubwa wa Kanisa umeshiriki katika ushindi wake mtukufu na pia usitawi wake tangu 1798. Ni hapa ambapo nyika na pahali pa upweke vimefurahishwa nao, nalo jangwa limefurahi na kuchanuka kama ua la waridi. Ni hapa ambapo sauti kuu ya maandalizi, 'Tayarisheni njia ya Bwana,' imesikika zaidi. Kutoka nchi hii ya Marekani ujumbe wa Kurudi kwake umetangazwa kwa kila taifa, kabila, lugha na jamii. Nchi hii na watu wanatambuliwa kwa jina la Sayuni, na Yerusalemu, [Isaya 2:1-3; 41:9; Mika 4:1, 2] ambayo imeandikwa kuihusu, 'Sheria itatoka Sayuni, na neno la BWANA litatoka Yerusalemu.' Jambo hili sasa latimia halisi katika kuhubiriwa kwa Ujumbe wa Malaika wa Tatu, [Ufunuo 14:9-12] ambao wapendekeza udumishaji na ulazima wa zile amri kumi za Mungu, ambazo ni msingi wa serikali Yake….

"Tumeufikia wakati ulioteuliwa ambapo umati mkuu wa watu walio hai wanaokiri kuwa ni wa Mungu watapatikana katika nchi iliyoelezewa hapo juu; na hakuna watu au taifa duniani kwa wakati huu ambao wataingiana na maelezo yaliyopeanwa hapo juu, ila watu watu wa nchi hii ya Marekani.

"Nchi hii ya Marekani, kulingana na historia ya kale ya ulimwengu, daima imekuwa ni tupu na ukiwa; nyika iliyokuwa bado haijalimwa, yenye ukiwa, isiyotumika, isiyojulikana na ulimwengu wa maendeleo hadi wakati wa ahadi ulipokaribia, ambapo Mungu alielekea kulitimiza neno lake, na kuunyosha mkono wake tena mara ya pili ili kuwatoa masalio wa watu wake kutoka kwenye nchi ya utumwa wao, na kuwaleta kwenye jangwa la maandalizi. Ni katika wakati ufaao ambapo Mungu aliruhusu bara hili la Marekani kugunduliwa, na bila shaka Bwana alimtuma malaika wake kuivuruga roho ya Columbus ili ajihusishe na kazi hiyo, na kuliongoza jahazi lake kupitia bahari kuu isiyojulikana hadi akaugundua ulimwengu huo mpya.

"Mnyama huyo wa kuogofya na wa kutisha, (Danieli 7:7, 19) ambaye alitafuna na kuvunja vipande vipande, na kuyakanyaga mabaki kwa miguu yake, alifikiria pia kuifanya nchi hii ya Marekani kuihisi chapa yake ya chuma; lakini kwa wakati ufaao Mungu aliliondoa kwato hilo lake la shaba kwa kuzirejesha Serikali hizi za Muungano kutoka kwa upanga wakati wa mapinduzi ya Marekani kama ilivyotabiriwa na Ezekieli 38:8, na hivyo likafunguka hapa kimbilio la uhuru wa kiraia na kidini ambapo masalio wa watu wake wangekusanywa.

"Kulingana na hoja zilizotangulia, tumejifunza ukweli muhimu kuwa Mungu hakika huwakusanya masalio wa watu wake kutoka kwenye nchi nyingi ambapo wametawanyishwa, na kuwa kwa hakika yeye huwaleta kutoka nchi ya utumwa wao hadi nyika ya misitu, pahali pa kujiandaa kabla ya kuingia nchi ya Israeli, urithi wa milele ulioahidiwa wa dunia mpya.

"Ni baada ya ule wakati ulioteuliwa wa Yerusalemu ambao ulitimia A.D. 1798, ambapo sauti ya maandalizi inasikika nyikani ….

"Ijapokuwa masalio walikuwa wakusanywe kutoka sehemu mbalimbali za nchi zote walipotapakaa, na wakawa waletwe kutoka nchi ya utumwa wao hadi kwenye nyika ya maandalizi, swali huibuka, Je, nchi hiyo ya utumwa wao inao ukubwa kiasi gani? Jibu: Ilijumuisha milki ya Asyria ya kale au ya Babeli, Umedi na Uajemi, Uyunani, na Urumi: inajumuisha maeneo yote ambapo vile vichwa saba vya utawala wa Kimataifa vilikuwa na mamlaka, isipokuwa nchi ya Kanani; hivyo tunaongozwa kabisa kutoka bara la mashariki kuitafuta hiyo nyika ya maandalizi ambapo masalio wanakusanywa ili kuitayarisha njia ya Bwana, na kuyatengeneza mapito ya Mungu wetu jangwani; na kwa hivyo pasipo kukwepa, tunafungiwa kwenye bara hili la Marekani…

Kutokana na hayo yaliyotangulia ni dhahiri kwamba jangwa hili la maandalizi ndiyo ile nchi ya kupendeza inayotajwa na Danieli 8:9. Katika sura ya 11:41, 45, nchi ya uzuri, na mlima mtakatifu wa uzuri, au nchi njema, nchi ya kupendeza, au pambo." Hiram Edson, *Review and Herald*, February 28, 1856.

"Nchi Ya Uzuri" na Ule "Mlima Mtakatifu wa Uzuri" ni Vitu Tofauti

"Tumepata kuwa dunia sio hekalu, bali ni eneo tu ambapo hatimaye litawekwa; ya kuwa kanisa sio hekalu, bali ni waumini tu wanaohusiana na hekalu hilo; na kuwa nchi ya Kanani siyo hekalu, bali ni pahali ambapo hekalu la kimfano lilikuwa. J. N. Andrews, *The Sanctuary and the 2300 Days,* 33–45.

Fikira za Kuhitimisha

"Lakini kwa vile watu ni wakaidi, wasio na shukrani, wanajisi, kama walivyokuwa Waisraeli wa kale, muda umerefushwa ili wote wausikie ujumbe wa mwisho wa rehema ukitangazwa kwa sauti kuu. Kazi ya Bwana imekwamishwa, wakati wa kutiwa muhuri umecheleweshwa. Wengi bado hawajausikia ukweli. Lakini Bwana atawapa nafasi ya kusikia na kubadilika." *The Faith I Live By*, 288.

"Wale wanaosubiri kuja kwa Bwanaharusi watawaambia watu, 'Tazama Mungu wako.' Miale ya mwisho ya nuru ya huruma, ujumbe wa mwisho wa huruma kuwahi kupeanwa ulimwenguni, ni ufunuo wa tabia Yake ya upendo. Wana wa Mungu wanapaswa kudhihirisha utukufu Wake. Katika maisha yao wenyewe na katika tabia zao, wanapaswa kuonyesha kile ambacho neema ya Mungu imewatendea." *Christ's Object Lessons*, 414–415.

"Kristo anasubiri kwa hamu sana kudhihirishwa kwake ndani ya kanisa Lake. Wakati tabia ya Kristo itadhihirishwa kikamilifu ndani ya watu Wake, ndipo Yeye atakuja kuwadai kama watu Wake mwenyewe. Ibid, 69.

"Kazi ya Roho Mtakatifu ni kuuhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, haki na hukumu. Ulimwengu unaweza kuonywa tu kwa kuwaona wale waaminio ukweli wakitakaswa kupitia ukweli huo, wakitenda kuambatana na kanuni takatifu na za kiwango cha juu, na kuonyesha, kwa hali ya juu, msitari wa mpaka unaotenganisha kati ya wale washikao amri za Mungu, na wale wanaozikanyagia chini ya nyayo zao. Utakaso wa Roho Mtakatifu hudhihirisha tofauti kati ya wale walio na muhuri wa Mungu, na wale wanaoitunza siku bandia ya pumziko. Wakati jaribio litakuja, itaonyeshwa dhahiri alama ya mnyama ni nini. Ni utunzaji wa Jumapili. Wale ambao, baada ya kusikia ukweli, huendelea kuichukulia siku hii kama takatifu, wanayo sahihi ya yule mtu wa dhambi, ambaye alifikiria kuzibadili nyakati na sheria." *Bible Training School*, December 1, 1903.

"Hakuna hata mmoja wetu atakayeupokea muhuri wa Mungu huku tabia zetu zikiwa na doa hata moja au waa. Ni jukumu letu sisi kurekebisha kasoro zilizoko kwenye tabia zetu, kuisafisha hekalu la moyo kutokana na kila unajisi. Ndipo mvua ya masika itatunyeshea jinsi mvua ya awali ilivyowanyeshea wanafunzi mnamo Siku ya Pentekoste…

"Je, mwafanya nini, ndugu zangu, katika kazi hii kuu ya maandalizi? Wale wanaoshirikiana na ulimwengu wanaipokea tabia ya kilimwengu na kujitayarisha kwa alama ya mnyama. Wale wasioamini ubinafsi wao, wanaojinyenyekeza mbele ya Mungu na kuzisafisha roho zao kwa kutii ukweli, wanaipokea tabia ya mbinguni na kujitayarisha kwa muhuri wa Mungu vipajini mwao. Wakati makataa yatatolewa na chapa kupigwa, tabia zao zitasalia kuwa safi na zisizo na dosari hata milele." *Testimonies*, volume 5, 214–216.